

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha saba – Tarehe 6 Februari, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISILISHWA MEZANI

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunazo Hati za kuwasilisha Mezani.

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mtaala wa Elimu ya Awali (2005), Mtaala wa Elimu ya Msingi (2005) na Mtaala wa Elimu ya Sekondari (2005).

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu uwasilishaji wa nakala za mtaala za kufundishia kama ilivyofanywa hivi punde na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba tarehe 31 Januari, 2013 Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge aliwasilisha hoja binafsi kuhusu udhaifu uliopo katika sekta ya Elimu nchini.

Wakati mjadala huo ukiendelea Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge alilihakikishia Bunge hili kuwa ahadi ya kuleta nakala za mitaala kwa waheshimiwa Wabunge itatekelezwa kabla ya tarehe 8 Februari, 2013. Leo tarehe 6 Februari, 2013 Serikali imewasilisha nakala ya mitaala kama ilivyoahidi.

Waheshimiwa Wabunge, vile vile katika majadiliano hayo siku hiyo kulikuwa na wasiwasi kuhusu kutokuwepo kwa mtaala huo na kwamba huenda nakala itakayowasilishwa haitakuwa nakala halisi na rasmi. Kwa kuzingatia utaratibu wa Kibunge uhalali na uhalisia wa nyaraka yoyote inayowasilishwa Bungeni upo chini ya mamlaka ya Spika. Hivyo kwa kutumia Kanuni ya tano Kanuni ndogo ya kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge, nimeona ni vema kuteua Wabunge wachache watakao chunguza uhalisia wa nakala hiyo iliyowasilishwa leo. Naomba niwataje Wabunge hao.

Mwenyekiti atakuwa Mheshimiwa Margaret Sitta, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Huduma za Jamii, ni mwalimu wa siku nyingi na mtu ambaye amepata kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi siku za nyuma. Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu mwalimu wa siku nyingi, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa mtu mwenye uzoefu katika maeneo hayo hayo ya Elimu, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Israel Yohana Natse na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Aidha Mheshimiwa James Mbatia pamoja na wawakilishi toka Serikalini watashirikiana na Wajumbe hao katika kubaini uhalisia wa nyaraka tajwa. Baada ya kukamilisha kazi hiyo watatakiwa kuwasilisha taarifa yao kwa Mheshimiwa Spika si zaidi ya kesho tarehe 7 Februari, 2013 ili kama mitaala hiyo itakuwa sahihi iweze kugawiwa kwa Wabunge wote kama Serikali ilivyoahidi.

Waheshimiwa Wabunge ningependa kuwathibitishia kama wakimaliza kazi hiyo leo wakanithibitishia tutagawa mitaala hiyo leo. Hivyo wajumbe niliowateua mnaombwa kukutana mara baada ya kumalizika kipindi cha maswali hapa Bungeni katika ukumbi uliopo *basement*. (Makofi)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 83

Kuboresha Hospitali ya Kahama

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Kahama ni ya muda mrefu sana na sasa inahudumia watu wengi sana kutoka Wilaya ya Kahama, Mbogwe na Bukombe:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipanua na kuboresha Hospitali hii ili iendane na mahitaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi Hospitali hii iwe ya Mkoa na kuweza kuhudumia Wilaya zote za Mkoa?

(c) Je, Serikali ipo tayari kukipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Chela kuwa Hospitali Teule ya Wilaya au kujenga Hospitali nyingine katika eneo hilo ili kuhudumia wananchi wa Msalala?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kahama inayo Hospitali ya Wilaya ambayo inahudumia majimbo yote mawili likiwemo Jimbo la Msalala na Jimbo la Kahama. Mpango wa Serikali kwa sasa ni kuboresha Hospitali ya Kahama kwa awamu kadri fedha zinavyopatikana.

Katika mwaka 2011/2012, Halmashauri ilipatiwa shilingi 60,125,300/= ambazo zimetumika kujenga wodi moja, kukarabati maabara na kujenga nyumba moja ya watumishi (*two in one*) kwa mwaka 2012/2013 jumla ya shilingi 29,011,000/= zimetengwa kwa ajili ya kukarabati mfumo wa umeme kwa kuweka *transformer*, mfumo wa maji taka, njia ya kusafirishia wagonjwa toka wodi ya wanawake hadi chumba cha upasuaji mita 200 pamoja na ujenzi wa nyumba za watumishi (*two in one*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kahama inahudumia wananchi toka Halmashauri za Bukombe, mbogwe, Shinyanga vijijini, Urambo, Uyui na Kahama yenyewe lakini kwa sasa tayari Mkoa wa

Shinyanga unayo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga.

Hata hivyo, kutokana na Hospitali hii kuwa na eneo finyu, miundombinu na msongamano wa wagonjwa Mkoa umeweka katika mpango wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ambapo tayari eneo la hekari 100 zimepatikana. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 zimetengwa shilingi bilioni 1 ili kuanza ujenzi huo.

Vile vile kutokana na ukomo wa Bajeti Mkoa umeomba maombi maalum ya shilingi bilioni 4.0 ili kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje yaani *OPD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiona rai ya Mheshimiwa Mbunge, lakini hata hivyo Serikali inaendelea na mkakati wa kuimarisha vituo vya afya vilivyopo kikiwemo kituo cha Afya cha Chela ili viweze kuwahudumia wagonjwa wengi zaidi na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

Kwa mwaka 2011/2012 jumla ya shilingi 240,011,206/= zimetumika kuboresha Zahanati nne za Nundu, Buganzo, Mwanziba na Kalagwa zilizopo katika Jimbo la Msalala.

Hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na Wananchi inaendelea na ujenzi wa Zahanati 48 na vituo vya afya vinne. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imepanga kujenga nyumba za Watumishi (*two in one*) na Zahanati ya Ntobo B kwa gharama ya shilingi 40,542,772/=. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, swali la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa majibu mazuri. Nilikuwa na maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa sababu msingi wa swali unatokana na ukubwa wa Wilaya ya Kahama ambayo ina kata 55 na vilevile na wananchi wanaozidi milioni moja na wastani wa wananchi wanaohudumiwa kwenye Hospitali hii ya Wilaya ni zaidi ya milioni moja na nusu ukijumlisha na hao wanaotoka kwenye Wilaya jirani.

Nilikuwa nimependa kuomba kwamba, kwa sababu Wilaya tayari imekwisha kuanza jitihada za kuteua maeneo mengine ikiwemo kituo cha Afya cha Chela kuwa Hospitali teule ya Wilaya.

Je, Serikali itakuwa tayari kuungana na jitihada hizi za Wananchi wa Kahama sambamba na jitihada zinazofanyika katika ngazi ya Mkoa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa sababu kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa hakuondoi haja ya kuwa na Hospitali teule ya Wilaya itakayokuwa Chela? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba Wilaya ya Kahama kama nilivyosema ni kubwa, ina tatizo kubwa sana pia la usafiri kutoka kwenye vituo mbalimbali ambavyo viko mbali. Kituo cha Afya cha Isagehe kilikwisha kuomba muda mrefu kupatiwa gari la wagonjwa nilitaka

kujua upande wa Serikali. Je, maombi hayo yako tayari sasa angalau kuwapatia na wenyewe gari la wagonjwa?

NAIBU SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mkoa na serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaliona hili wazo. Hili wazo la Mheshimiwa Ezekiel M. Maige amelizungumza mara nyingi sana. Anazungumza kinachosemwa hapa ili tuelewane vizuri kule Chela kule, kule katika Wilaya yake ile katika eneo lile la Msalala yeye Mheshimiwa Mbunge anataka kupendekeza kwamba pale kwa sababu ya *population*.

Ni kweli mimi nimekwenda katika lile eneo, wako watu milioni moja, wako pale. Sasa lakini Hospitali ya mkoa inayozungumzwa hapa sasa tunazungumzia Mkoa mzima wa Shinyanga. Ambapo pale Hospitali ya Mkoa ilipo sasa hivi tunapozungumza hapa ni kweli pia kama anavyosema Mheshimiwa pako finyu, ni padogo yaani mkienda pale mkiangalia tena hata mkipita kwenye zile *corridor* mimi nimepita mle ndani ni padogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mkoa ulichofanya kupitia *Regional Consultative Committee* ambao pia Mheshimiwa Ezekiel M. Maige anaingia mle ndani,

umeamua kwamba unajenga eneo lingine limepatikana hekari 100 kwa ajili ya kujenga hiyo Hospitali ya Mkoa na Hospitali za Mkoa kwa Waheshimiwa Wabunge ndizo ambazo tumeziona sasa ziko kama *referral Hospital* kwa maana Wilaya zote zinakwenda pale.

Mheshimiwa Ezekiel M. Maige anachosema sasa, anasema habari ya kule Kahama hili sasa ni wazo jipya na hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu hawezi kusema sawa tunawaruhusu endeeleni kule, lazima turudi tena kwa mtiririko ule ule tuende tena kule Msalala, tuende Kahama tupitie katika *DDC* turudi tena kwenye *full council*, turudi tena kwenye *Regional Consultative Committee* tuseme *there is a new development*. Sasa tuhame kwenye mawazo haya ya hizi hekari 100 ambazo nimeshasema hapa kuna bilioni moja imeshatengwa na halafu kuna *projection* ya bilioni 4 tuhamie kwenye ile anayosema pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nasema tunalichukua kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, haya ni mawazo ya Mbunge lakini nasema kwamba huwezi ukaenda nje ya hiyo bila kutumia hivyo vikao halafu baadaye vitakwenda kwa Waziri mwenye dhamana tena tukishirikiana na Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili anazungumza habari ya gari, kwa vile sasa maswali ya hapa hakuelekeza hivyo alikuwa anazungumzia tu kwa ujumla nitakachotaka sasa ni kwenda ku-*chek* kwanza haya magari ambayo yamekwenda katika eneo lile. Mpango wa Serikali ni kwamba kila kituo kiwe na gari moja kwa ajili ya kusaidia Wagonjwa na tutaangalia sasa ili tuweze kuona kwamba

tumepanga lini kule tuweze kuona kwamba tunaweza tukasaidiana nao lakini kwa sasa nachelea kujibu.

NAIBU SPIKA: Nilikuona hapo kabla, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kunipa nafasi nimwulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni azma ya Serikali kujenga Hospitali kwa kila Wilaya na Wilaya ya Longido imeomba kwa muda mrefu kujengewa Hospitali ya Wilaya na kwenye Bajeti nadhani kila Bajeti tulikuwa tunaweka maombi ya kujengewa Hospitali ya Wilaya.

Je, Serikali katika Bajeti hii itatusaidia kujenga Hospitali ya Wilaya?

NAIBU SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael L. Laizer, kaka yangu na jirani yangu Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachosema ni kwamba *projections* zetu zinaonyesha kwamba katika Bajeti zimewekwa najua Mheshimiwa Michael L. Laizer anachokisema hapa na pana matatizo pale na wananchi kule wananisikiliza wakati mwingine wanakwenda Kibongoto kule kwangu, wakati mwingine wanakwenda

Sanya Juu kwa sababu ya matatizo waliyonayo kule na kunashida hasa. *May be* tutakachofanya hapa ni kwenda kuiangalia *the current* Bajeti inasema nini kwa sababu hapa siwezi kuja na Bajeti nyingine mpya. Kwa hiyo, tutashirikiana naye tuangalie Bajeti inasema nini kama ni suala la kupatikana kwa hela hizo sasa hicho ndicho ninachoweza kwenda kuangalia kwenye Bajeti *item* inasema nini ili tusukume tusaidie watoto na kina mama na wazee waweze kupata huduma na vijana waweze kupata huduma. (*Makofi*)

Na. 84

Changamoto Zinazokabili Kituo cha Afya Mzenga

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO aliuliza:-

Kituo cha Afya Mzenga ambacho kinahudumia wananchi wengi sana wa Tarafa ya Mzenga kinakabiliwa na Changamoto nyingi kama vile ukosefu wa wodi maalum ya wazazi na gari la wagonjwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi maalum ya wazazi kwenye Kituo hicho?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia Kituo hicho gari la wagonjwa kuhudumia wagonjwa na kinamama wajawazito?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Mzenga kinakabiliwa na ukosefu wa wodi ya wazazi pamoja na gari kwa ajili ya kubebea wagonjwa. Kituo hiki kina wodi ndogo ya wazazi ambayo ina chumba kwa ajili ya kujifungulia na chumba kingine chenye uwezo wa kulaza watu watano kwa ajili ya kupumzisha akina mama baada ya kujifungua.

Aidha ni kweli kwamba kituo hiki kinahudumia wagonjwa wapatao 10,199 idadi ambayo ni kubwa kuliko uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa kushirikisha nguvu za wananchi inaendelea na ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha Afya cha Maneromango ili kuboresha huduma za uzazi katika Wilaya ya Kisarawe. Ujenzi wa kituo hiki upo katika hatua za ukamilishaji (*finishing*).

Aidha Serikali inakusudia kutenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa ajili ya kupanua wodi ya wazazi katika kituo cha afya cha Mzenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe katika mwaka 2012/2013 imefanikiwa kununua magari mawili (2) ya wagonjwa katika mwaka huu na kufanya idadi ya magari ya kubebea wagonjwa kuwa matatu (3).

Magari hayo yamepelekwa katika Vituo vya Afya vya Masaki, Maneromango na katika Zahanati ya Masanganya. Kituo cha Afya cha Mzenga kinahudumiwa na gari la wagonjwa lililoko katika kituo cha Afya cha Maneromango ambacho kipo umbali wa kilometa 30 kutoka Mzenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma za afya zinaimarishwa katika Kituo cha Afya Mzenga zikiwemo usafiri pamoja na huduma za akinamama wajawazito kadri Bajeti ya Serikali itakavyoruhusu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, swali la nyongeza.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilipenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza yafuatayo.

Kwa kuwa kituo cha Afya cha Mzenga kwa mujibu wa majibu na kwa mujibu wa Bajeti ya mwaka huu 2012/2013 kuna mpango wa kupanua wodi ile ya wazazi na kwa kuwa katika kituo cha Afya cha Maneromango kupitia mfuko wa Jimbo tunajenga hiyo wodi ya wazazi ambayo sasa hivi tuko katika *finishing*.

Je, Serikali iko tayari sasa kutusaidia vifaa hasa vitanda kwa ajili ya kina mama kwa ajili ya kujifungulia?

Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe ndiyo inapokea wagonjwa kutoka katika vituo hivyo vya Afya Maneromango, Mzenga na Chole lakini kwa kuwa Hospitali

hii ya Wilaya ina changamoto kubwa sana na Mheshimiwa Naibu Waziri unajua wazi, mwaka jana ulinijibu hapa kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Wilaya pamoja na ujenzi wa mochwari.

Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutembelea Hospitali ya Kisarawe ili mradi kwa pamoja kwa sababu tumeleta ombi maalum la shilingi bilioni moja na milioni mia tatu (1,300,000,000/=) iweze kupata nguvu kwa ajili ya utekelezaji katika mwaka huu wa fedha? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa ajili ya rekodi kwa sababu sisi tumekwenda kule tumeona huyu Mheshimiwa Mbunge anayeuliza swali hili hela za kwake zilizopelekwa za *Constituency Development Catalysit Fund* yaani ule mfuko wa Maendeleo huyu mwanaume amezisukuma amezipeleka katika hivi vituo. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Waziri Mkuu kumpongeza sana Mbunge huyu kwa jinsi anavyofanya kazi yake ya Ubunge vizuri. *(Makofi)*

Hicho kituo cha Manarumango ambacho kimefanyiwa hiyo kazi inayofanyika pale, kwa asilimia 100 kazi iliyofanyika pale amefanya Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo. Kwa hiyo tunapenda kumpongeza sana. Na yako maeneo mengine ambayo ameyafanyia kazi hapa yuko *concern* na hili eneo na tunapenda kumpongeza sana.

Sasa yeye anazungumza habari sasa kwamba kwa vile tulishafanya kazi hiyo na kwa vile kazi kubwa imeshafanyika.

Je, tunafanyaje kuhusu sasa vitanda na vile vifaa vingine vilivyoko pale kwa maana ya kwamba kazi fulani imeshafanyika sasa nitakwenda kuangalia kwenye ile Bajeti ili kuona kwamba je, tunaweza sasa tukarebisha ili tusaidie hiki kituo anachokizungumzia kiweze kupata vitanda na kadhalika? Tutaenda kuangalia wote ili tuweze kuona nini cha kufanya.

(b) Hili linalozungumzwa la ukarabati, ukarabati tulimpeleka Naibu Katibu Mkuu, Bwana Kidata ndiyo alipelekwa pale akaenda kuangalia pale na yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge na Mbunge wa Viti Maalum alikuwa anashughulikia jambo hili na kazi kubwa imefanyika pale.

Kimsingi tumeshawaandikia barua na tukawaambia kwamba haya maombi tumeyaona na haya mambo tutayafanyia kazi sasa ni suala la ufuatiliaji kwa sababu hela hizi zote lazima tuwasiliane pia na Hazina ili kuweza kuona kama hii imekwenda kama *special request* na haikuingia kama Bajeti. (Makofi)

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri na pongezi zilizotoka kwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi, ameelezea umuhimu wa Serikali inavyoona kwamba ni lazima wananchi wake wapate huduma ya afya iliyokuwa bora.

Lakini kuna matatizo katika vituo mbalimbali vya afya na zahanati na kwa kuwa mama Mjamzito anapoenda kujifungua, haijulikani mama yule atajifungua mchana, asubuhi au usiku na inapotokea usiku, mama yule mjamzito hulazimika kujifungua kwa vibatari au kwa mwanga wa simu.

Je, Serikali iko tayari kuzisaidia Halmashauri ili ziweze kununua *solar* na kupeleka kwenye hospitali au vituo vya afya vilivyokuwa katika wilaya ya Kisarawe, Mkuranga, na wilaya nyingine zote za mkoa wa Pwani pamoja na wilaya nyingine zote nchini Tanzania? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi ya Mheshimiwa Waziri inataka kuwa *fair*, huyu Mbunge anayezungumza hapa ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani, kama amebadilisha aniambie kama wamebadilisha mkoa wa Pwani naomba unilinde Mheshimiwa Naibu Spika.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Sijabadilisha Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa hata hii *mission* ambayo tumefanya na hizi barua zote pia na yeye tumemwandikia kwa sababu ya jitihada zake katika mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mbunge amekuwa anafanya kazi kubwa sana na amekuwa na mawazo mazuri na ya kusaidia na

hata mara ya mwisho alikutana na Mheshimiwa Kidata pia wakazungumzia jambo hili. Kwa hiyo, tunapenda kumpongeza yeye kwa kazi nzuri inayoendelea katika mkoa wake. (Makofi)

Sasa kuhusu hii huduma ya kinamama na watoto na kuhusu kuweka *solar system* katika eneo hili, ndiyo mpango ambao tunao kama Serikali. Kwa kweli mpango huo ni kwa maeneo yale yote ambayo yanaonekana kwamba yako pembeni na umeme hauwezi kufika katika muda mfupi ujao kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Hili jambo analosema hapa ni jambo *sensitive* na wakati mwingine tumepoteza watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tumepoteza akinamama kwa sababu ya masuala haya ya umeme. Serikali ndicho inachosema ndicho juzi nimetoka Katavi na Rukwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jimbo lake la uchaguzi amefanya kazi ya kupeleka *solar system* katika zahanati zote na katika vituo vya afya zote na katika shule za sekondari ili kusaidia katika eneo hili.

Kwa hiyo, sisi tunaomba Wabunge tuige mfano ule na yeye ametumia ile *Constituency Development Catalyst Fund* kwa ajili ya kusaidia jambo hili. Napenda kusema kwamba ni wazo zuri linakuja sasa ni suala la Bajeti kuweza kujua kwamba tunafanyaje fanyaje ili tuweze kusaidia lakini tunakwenda kuangalia ili tuone kwamba tuna nini kule ili kuweza kuona jinsi tutakavyosaidia. (Makofi)

Kufa kwa Uwanja wa Ndege Moshi Mjini

MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO aliuliza:-

Uwanja wa ndege wa Moshi Mjini ndiyo mlango wa watalii wanaokuja kupanda Mlima Kilimanjaro, lakini kwa zaidi ya miaka kumi (10) Serikali imeutekeleza uwanja huo na kufa kabisa kwa kukosa matengenezo maalum hasa kwenye *run way*, kiasi cha kusababisha *Precision Air*, kukatisha huduma zao pamoja na ndege nyingine ndogo zilizokuwa zinaleta watalii Moshi.

(a) Je, ni sahihi kwa Serikali kuuwa uwanja wa ndege huo ambao ndiyo mlango wa kupanda Mlima Kilimanjaro?

(b) Je, ni sababu zipi zimefanya Serikali itelekeze uwanja huo ambao ni hazina kwa nchi?

(c) Serikali imeshawahi kutoa taarifa kwamba fedha za matengenezo ya uwanja huo zimeshatengwa lakini hadi leo hakuna kilichofanyika. Je, Serikali inasema uongo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye maswali (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina dhamira ya kukiua kiwanja cha ndege cha Moshi kutokana na

umuhimu wake katika kukuza utalii hapa nchini hususan kuhudumia watalii wanaopanda mlima Kilimanjaro na wanaokwenda kwenye mbuga za wanyama yaani *KINAPA*.

Kiwanja hiki pia kina umuhimu katika jamii kwani hutumika katika kuwasafirisha wagonjwa wanaotaka kupata huduma za matibabu ya haraka kutoka katika hospitali ya Rufaa ya *KCMC* au katika hospitali nyingine na ndani ya nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijatelekeza kiwanja cha ndege cha Moshi. Kwa sasa kiwanja cha Moshi kinaendeshwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanda vya Ndege Tanzania na kina wafanyakazi sita.

Serikali kupitia *TAA*, yaani mamlaka ya viwanja vya ndege imekuwa ikitenga shilingi milioni 190 kila mwaka fedha hizi hutumika katika kugharimia uendeshaji, utunzaji na matengenezo madogo madogo ya kiwanja hiki ikiwa ni pamoja na njia ya kuruka na kutua ndege ili kukifanya kiendeleo kuwa salama kwa watumiaji.

Kulingana na takwimu za miruko ya ndege na abiria kumekuwa na ongezeko la wastani wa asilimia 12.4 kwa miruko ya ndege kutoka miruko ya ndege 491 katika mwaka 2009 hadi miruko ya ndege 638 katika mwaka 2012.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la abiria waliotumia kiwanja hicho cha wastani asilimia 37.5. Katika mwaka 2009 kilihudumia abira 575 ikilinganishwa na mwaka 2012 kilipohudumia abira 1355.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha ndege cha Moshi, ni moja kati ya viwanja vya ndege kumi ambavyo Serikali imepanga kuboresha kupitia mkopo kutoka benki ya dunia, Fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.2 tayari zimepatikana kutoka Benki hiyo na usanifu wa kina kwa viwanja kumi kikiwemo kiwanja cha ndege cha Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hii kukamilika, kitakachofuata ni ukarabarati wa viwanja hivyo kikiwemo kiwanja cha Moshi. *(Makofi)*

MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ya Naibu Waziri yanaonyesha kweli Serikali inakijali kiwanja cha Moshi, lakini ukweli ni kwamba siyo kweli mimi ningemwomba Waziri aje Moshi na anitaarifu ili aweza kuona hali halisi ya kiwanja kile. Kama ni kweli kwa kipindi cha miaka kumi shilingi milioni 190 zinatengwa kwa ajili ya kukarabati kiwanja hiki hata angalau one-way kweli kiwanja kile kingekuwa kinatumika kwa ndege hata *precision*.

Lakini si kweli pesa hizi hazipo na kwa kuwa zimeshatajwa zinakuja mimi ningeomba aje ili tuweze kuhakikisha hizi pesa zimepelekwa wapi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimefika katika uwanja wa ndege wa Moshi na nilienda mahususi kuona uwanja huo kwa sababu hizi hizi za kusemekana kwamba uwanja ule umetelekezwa.

Kwa hivyo si kweli kwamba majibu tuliyotoa siyo ya kweli. Fedha hizo hutengwa na fedha milioni 190 kwa uwanja wa ndege siyo hela nyingi sana zinatumika kufanya

matengenezo madogo madogo lakini ukarabati wa *run way* ambalo ndilo jambo limefanya ndege nyingi ziache kwenda pale uwanja ule umejengwa kwa tabaka linaloitwa *surface* liseni sasa kwa sababu kimejengwa muda mrefu sana na kimeanza kuchoka na kwa hivyo zile kokote nyingi zimekuwa *lose*. Kwa hivyo ndege *JET* haziendi kwa kuogopa ndege nyingine kuingia kwenye *engine*.

Lakini ndege zingine bado zinatumia *tube propelid engine* zinakwenda pale wanatumia ule uwanja na ndiyo maana katika taarifa hii inaonekana kwamba ziko ndege zinatumia uwanja wa Moshi na abiria wanatumia uwanja huo. Nikubaliane tu naye kama anaona iko sababu ya Waziri au mimi kwenda huko nitapanga nitawasiliana naye nitakwenda tena katika uwanja huo. (*Makofi*)

MHE. MOZA ABEID SAIDY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa viwanja vingi vya ndege vimeweza kutekelezwa hapa nchini na wala ndege haziwezi kutua tena. Mathalani katika kiwanja cha Kondoa, kiwanja kile kiko pale kimetekelezwa wala hakina kiwango chochote cha kuweza kutua ndege ambazo zinaweza kuwavutia watalii na pale ni kitovu cha watalii ili waweze kuja kutua na ndege zao kwa ajili ya kuja kutalii katika eneo letu la Wilaya ya Kondoa.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuitengeneza Wilaya ya Kondoa nayo kuwa na hadhi katika hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja katika wilaya nyingi tu hapa nchini zinatumiwa kwa kiwango kidogo sana ikiwamo kiwanda hiki cha wilaya ya Kondo. Serikali kama nilivyosema katika jibu langu la msingi inakwenda kwa awamu sasa hivi tunataka kuanza kuhudumia viwanja kumi hivi vya mikoa ambavyo tunadhani kwamba umuhimu wake kiuchumi na kijamii ni mkubwa zaidi. Kadri fedha zitakavyopatikana basi nadhani tutaingia kwenye *program* ya kuboresha viwanja vilivyoko katika wilaya.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Kabla hatujaendelea napenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu huyupo leo Bungeni yuko Arusha kikazi na anayekaimu sasa ni Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. (*Makofi*)

Na. 86

Utafiti wa Mbegu ya Mpunga Aina ya “Siro 5”

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA aliuliza:-

Matokeo ya utafiti wa mbegu bora aina ya “SARO 5” kwa zao la Mpunga uliofanywa na Kituo cha Utafiti cha *KATRIN*, Ifakara yameonyesha mafanikio makubwa kwa kuweza kuzalisha wastani wa gunia 37 (zenye ujazo wa kg.100 kwa kila ekari moja).

Je, ni lini Serikali itaanza kutumia matokeo haya ya utafiti huu wa mbegu bora ya zao la mpunga kwa kusambaza mbegu hizo kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji katika mashamba yao.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Ulanga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mbegu bora ya mpunga aina ya “SARO 5” iliyotolewa na Kituo cha utafiti wa KATRIN mwaka 2002 ina sifa ya kuzaa sana na pia ina harufu nzuri ya kiasi kwa maana ya semi-aromatic hivyo inapendwa sana na walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari inaendelea kuyatumia matokeo haya ya utafiti kwa mfano mbegu mama za SARO 5 zimekuwa zikizalishwa katika kituo cha KATRIN kwa ajili ya Wakala wa Uzalishaji wa Mbegu za Kilimo (ASA). Katika kipindi cha miaka mitano KATRIN imeweza kuzalisha zaidi ya tani 30 za mbegu mama ambazo ASA ilizitumia kuzalisha jumla ya tani 244 ya mbegu za daraja la msingi. Ili kuhakikisha wakulima wanapata na kutumia mbegu hii bora ya mpunga ASA ikitumia shamba lake la Kilangali na kwa kushirikisha taasisi za Serikali kama vile Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na vikundi vya wakulima imekuwa ikizalisha mbegu za daraja zilizothibitishwa ubora (*certified seeds*) kwa ajili ya kuzisambaza kwa wakulima nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika kipindi cha miaka mitano kilichoanzia 2008 hadi 2012 uzalishaji wa mbegu hizi umekuwa ukiongezeka kama ifuatavyo: mwaka

2008 jumla ya SARO 5 iliyozalishwa ni tani 245, mwaka 2009 tani 460, mwaka 2010 tani 631, mwaka 2011 tani 930 na 2012 (mwaka jana) tani 1440.

Kwa kutumia wadau mbalimbali mbegu hizi za mpunga wa SARO 5 zinasambazwa karibu kila Mikoa hapa nchini. Sehemu kubwa ya mbegu hizi husambazwa katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Shinyanga, Mwanza, Iringa, Rukwa, Tabora, Manyara, Kilimanjaro na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha utafiti *KATRIN* na Wakala wa Mbegu (ASA) wanaendelea kuzalisha mbegu hii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kadri inavyowezekana kwa lengo la kuhakikisha kwamba hii inasambaa kwa wakulima wengi iwezekanavyo.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri na vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza watafiti wa chuo cha *KATRIN* Ifakara kwa kazi nzuri wanayofanya kufumbua mbegu hii nzuri ya zao la mbuga. Nina maswali mawili.

Kwa kuwa, imethibitika majibu ya Waziri inaonyesha kwamba mbegu inaweza ikanyanyua uzalishaji wa zao la mpunga sasa swali langu kwanini sasa Serikali wasiwasaidie wakulima wa Ulanga kuifanya mbegu hii kuingiza katika ruzuku au mfumo ule wa mbegu ya ruzuku?

Taarifa hizi njema aidha zimebaki tu kwenye vyo lakini wakulima wenyewe pamoja na maafisa wa ugani nafikiri hawana taarifa hii ya hili zao la SARO 5 kama linaweza likawasaidia wakulima hawa hadi kufikia magunia 37 kwa heka moja. Je, Serikali wana utaratibu gani au wana

mpango gani madhubuti kufikisha elimu na taarifa kwa wananchi ili wabadilishe zao lao kwa kutumia mbegu hii bora?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia naomba nitumie fursa hii kuungana na Mheshimiwa Mbunge kuwapongeza sana watafiti wa kituo chetu cha *KATRIN* pale Ifakara, kwa kubuni mbegu maana utafiti huu umetambuliwa na taasisi mbalimbali za Afrika kama hii ni mbegu bora sana mpaka imefikia hatua ya kupatiwa ufadhili wa mbegu ya dunia.

Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba kwa sasa nadhani changamoto tuliyokuwa nayo ni kwamba ni kweli kwa Serikali mpaka sasa hivi kwa jitihada hizi tulizokuwa tunafanya kupitia wakala wa mbegu *ASA* tumeweza kuzalisha mwaka jana kufikia tani 1500.

Lakini tani 1500 kwa mahitaji ya Tanzania bado ni uwezo mdogo. Kwa hiyo kitu tulichokusudia kufanya kwanza ni kupata sekta binafsi kuingia kwenye uzalishaji wa mbegu kwa maana *seed multiplication* lakini la pili kupata taasisi hizi kubwa ambazo yana maeneo makubwa kama magereza na kadhalika nayo kuona kwamba hii ni fursa ya kibiashara kubwa na jitihada hizo zinafanywa kwa kuwasiliana na taasisi nyingine. Tunaelekea huko kwenye kuweza kuzalisha *SARO 5* kwa kiasi kikubwa zaidi ambayo itatuwezesha kutenga sehemu ya mbegu hii kuifanya iwe mbegu ya ruzuku kwenye maeneo ya uzalishaji mkubwa ya mbunga kama maeneo ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la elimu kwa umma ni kweli mbegu hii imewatoa wakulima wanaozalisha

mbegu hii ya mpunga, kutoka kwenye tani moja, tani moja na nusu kwa hekari wanaopanda vizuri kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam wanapata mpaka tani sita kwa hekari. Kwa hiyo, nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tayari tumejipanga kuwa na elimu ya Umma kwa mbegu hii ambayo itahusisha watafiti na watumishi wenyewe wa KATRIN na wataalam wengine ili wakulima wapate ufahamu mzuri zaidi zaidi wa ubora wa mbegu hii.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunichagua. Moja ya tafiti zinazotakiwa ili kutimiza azma ya kilimo kwanza ni lazima tufahamu aina ya udongo wa mahali fulani, aina ya mbolea na aina ya mbegu inayotakiwa.

Katika Jimbo langu la Karatu, imefanyika tafiti kuhusu udongo, mbolea na mbegu. Tafiti zimeonyesha kwamba, mbolea aina ya Mijingu haifai kwa ardhi ya Karatu.

Swali, kwa nini wananchi na wakulima wangu kwa kipindi hiki wamenyimwa kupata pembejeo, walioomba watu arobaini na tatu elfu na sabini na saba, na waliopata ni mia mbili hamsini tu. Je, Serikali ina dhamira ya kweli katika kuendeleza kilimo kwanza?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utafiti wa *soil fertility* kwa maana ya mazingira ya udongo imefanywa na vituo mbalimbali vya Tanzania, vikiongozwa na kituo cha Ilonga na vituo vingine, tuna kituo kingine kule Tanga, ambacho wamefanya utafiti wa kujua ubora wa udongo wa Tanzania nzima.

Sasa hii mbolea ya Mijingu ambayo imetolewa mwaka huu, siyo Minjingu *phosphate* ni Minjingu *NPS plus*, ambayo inaitwa Mijingu Mazao ambayo ni *direct substitute* ya *DAP*, kwa maana ya *chemical ingredients* zake zinafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo mbolea unayosema wewe, kwa mfano Mheshimiwa Mbunge anasema tungempatia pembejeo, pembejeo ipi? Hii Minjingu Mazao ilichofanya, imekwenda kubadilisha mbolea ya *DAP* ambayo zinafanana kwa virutubisho vyake, isipokuwa moja inatengenezwa Tanzania na ni gharama nafuu zaidi kuliko ile nyingine ambayo tunaleta kutoka nje, in gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ya kwamba hii mbolea ya Minjingu haifai kwa Wilaya ya Karatu, maana yake hata hiyo *DAP* na zingine wanazotaka hazifai. Sasa tufanye utafiti mwingine wa kujua wewe unataka mbolea ya aina gani.

Lakini hiyo ni kazi ya wataalam wetu na kwa wataalam hatukutoa mbolea isipokuwa kwamba tumefata ushauri wa kitaalam kutoka kwa hawa Mabingwa wa Utafiti wa Kilimo Tanzania. (*Makofi*)

Na. 87

Sheria Mpya ya Madini

MHE. TUNDU A. M. LISSU (K.n.y. MHE. KABWE ZUBERI ZITTO) aliuliza:-

Kufuatia taarifa ya Kamati ya Bomani, Bunge lilitunga sheria ya Madini 2010 na mabadiliko ya sheria ya fedha kuwezesha nchi kufaidika na rasilimali ya madini.

(a) Je, leseni mpya iliyotolewa kwa kampuni ya *North Mara Gold Mines Ltd.*, imezingatia matakwa ya sheria mpya ya madini?

(b) Je, Serikali imetoa leseni ya uchimbaji wa uranium katika mradi wa Mkuju; na kama ndiyo je, imezingatia matakwa ya sheria mpya?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kuwa uhuishaji (*renewal*) wa leseni *SML 17/96* na *SML 18/96* za kampuni ya *North Mara Gold Mines Ltd.*, umezingatia matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

Uhuishaji wa *Special Mining Licence (SML)* hufanyika kwa mujibu wa kifungu Na. 45 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na mchakato wa uhuishaji wa leseni kwa ajili ya mgodi wa *North Mara* ulizingatia ipasavyo kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na matakwa ya kisheria uhuishaji wa leseni hizo umezingatia kukamilika kwa mchakato wa masuala ya mazingira na leseni hizo zimetolewa kwa muda wa miaka 15 kulingana na makadirio ya mashapo ya dhahabu yaliyopo kwa sasa. Iwapo kampuni itagundua mashapo zaidi siku za usoni baada ya muda huo itabidi iombe tena kuhuishwa kwa leseni kwa ajili ya mgodi huo kuweza kuendelea na uchimbaji.

Aidha, majadiliano yamefanyika na kampuni kuhusu kufanya mabadiliko ya vipengele katika Mkataba wa Uendelezaji Madini *MDA* ili uendane na mabadiliko ya Sheria ya Madini, 2010 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2012, hususan kulipa mrabaha kwa kiwango cha asilimia 4 ya *Gross Value (GV)* badala ya asilimia 3 ya *Net Back Value (NBV)* ilivyokuwa hapo awali.

Baadhi ya vipengele vya *MDA* vilisharekebisha hapo nyuma. Mfano kuondoa kipengele cha nyongeza ya asilimia 15 kwenye mtaji ambao haujakombolewa.

Maeneo mengine ambayo mazungumzo yanaendelea ni pamoja na *service levy* kulipwa kwa kiwango cha 0.3% ya *turnover* badala ya US\$ 200,000 inayolipwa kwa sasa. Lengo la majadiliano hayo ni kuhakikisha kuwa Serikali inapata manufaa zaidi kutokana na shughuli za mgodi huo kwa mazingira ya sasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali haijatoa leseni ya uchimbaji wa madini ya urani kwa ajili ya mradi wa Mto Mkuju. Utoaji wa leseni maalum ya uchimbaji madini

yaani *Special Mining Licence (SML)* hufanyika kwa mujibu wa kifungu Na. 42 cha Sheria ya Madini, 2010.

Hii inaenda sambamba na utekelezaji wa kifungu Na. 10 cha sheria hiyo kwa ajili ya kujadili mkataba wa uendelezaji wa madini (*Mining Development Agreement (MDA)*) kwa ajili ya mradi husika.

Hivyo, napenda kumwondolea wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuwa utoaji wa leseni kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya Urani kwenye mradi wa Mto Mkuju utazingatia ipasavyo matakwa ya sheria ya madini ya mwaka 2010.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali 3 ya nyongeza. Moja, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mchakato wa uhuishaji wa leseni ya Mgodi wa *North Mara*, umezingatia masuala ya kimazingira.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba, Kampuni ya *Barrick Gold* imetengeneza vyanzo vipya vya maji safi na salama kwa ajili ya wananchi wa Nyamongo?

Mbili, kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba, majadiliano yamefanyika kuhusiana na malipo ya tozo ya huduma, *Service levy* ya asilimia 0.3 badala ya US\$ 200,000 zinazotolewa sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aliambie Bunge kwa nini Serikali hailazimishi kampuni hii ilipe hii tozo ya huduma ambayo imekwa kwa mujibu wa sheria na Sheria ya Fedha za Mamlaka za Mitaa, badala yake inaiachia inalipa US\$ 200,000 ambayo haipo kisheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ni maswali mawili tu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu, kwamba tangu mwezi wa tano mwaka jana, Kampuni ya uchimbaji dhahabu ya *ABG* katika mgodi wake wa *North Mara*, imefanya kazi kubwa, ya kuhakikisha huduma za jamii zinawafikia wananchi wote wa maeneo ya Nyamongo, Kelende, Nyangoto na maeneo mengine yote yanayozunguka mgodi ule, yapatayo vijiji saba.

Mimi mwenyewe nifanya ziara mara kadhaa kukagua miradi ya maendeleo ambayo wanaifanya, ikiwa ni sehemu ya masharti ya kuwapa leseni mpya kwa maana ya *ku-renew* tuliwaagiza kwamba lazima wahakikishe mikataba yote waliyoingia na wananchi wa eneo la Nyamongo wanaitekeleza kabla hatujawapa leseni mpya.

Ninayo furaha kueleza Bunge lako Tukufu kwamba, shule ambazo zinazungumziwa kujengwa zinaendelea kujengwa, visima vya maji kama alivyouliza Mheshimiwa Mbuga, vinaendelea kuchimbwa na mimi mwenyewe nilienda kukagua zoezi hilo ili kuweza kuwapa leseni hiyo. Kwa hiyo, shughuri hizo zinaendelea kufanywa na tutaendelea kusimamia zinatekelezwa.

Swali la pili, anauliza kwa nini Serikali haiwaagizi, mgodi wa kampuni ya *ABG* kulipa *US\$ 200,000*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *US\$ 200,000* hizi, zinalipwa kulingana na mkataba ambao walifunga wakati ule

wanaanza. Moja ya kazi kubwa ambayo Serikali inafanya, ni kuhakikisha inarekebisha kasoro zote zilizopo kwenye mikataba ya zamani, mikataba ambayo ilifahamika mikataba mibovu, ili kuhakikisha Taifa linanufaika zaidi.

Kwa kufanya hivyo, tumeanza na migodi mingine, Migodi wa Nzega, umelipa madeni ya nyuma yote ambayo walikuwa hawalipi, zaidi ya bilioni mbili na nusu imelipwa kwenye Halmashauri ya Nzega.

Migodi wa GGM umelipa madeni yote ya *service levy*, zaidi ya *US\$1.4 million* kwa Halmashauri ya Wilaya Geita. Migodi ya ABG kwa sababu inahusisha Halmashauri nyingi, na wao walifunga katika mkataba wao, hicho kipengele cha kulipa *US\$ 200,000* kama *flat rate*, ndiyo tuko kwenye mazungumzo sasa ya kutengua mkataba ule na wakubaliane sasa kuendana sambamba na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa 1982, ili waanze kulipa asilimia 0.3 ya *turnover*.

Nitoe wito kwa Halmashauri zote nchini, Halmashauri zimekuwa zikiongeza eneo hili bila kufuata Sheria ya Fedha ya mwaka 1982 na kupandisha malipo mpaka asilia 5 baadhi ya maeneo. Sheria yenyewe iko wazi, inaelekeza kwamba *service levy* italipwa asilimia 0.3 ya *turnover* kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea na majadiliano ya *MDA* zote zinazosimamiwa na migodi wa Kampuni ya ABG na wala siyo *North Mara* peke yake. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Sera ya Madini ya mwaka 2009, pamoja na Sheria ya Madini ya mwaka 2010, inatambua ushiriki wa Watanzania katika umiliki wa hii migodi mikubwa.

Moja kati ya vitu vilivyoainishwa ni moja, Serikali kuwezesha haya Makampuni makubwa ya madini kujisajili katika soko la hisa la ndani. Pili ni kwa madini ya Vito kumilikiwa na Watanzania kwa asilimia mia moja ama kwa asilimia 50 pale ambapo uwekezaji mkubwa unahitajika.

Nilitaka Naibu Waziri aniambie, ni kwa kiwango gani haya maswala mawili yameanza kutekelezwa na Serikali?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Sheria ya Madini ya mwaka 2010 pamoja na sera yake ya mwaka 2009, inaelekeza kwamba, katika uwekezaji wowote mpya ambao utanza nchini, ni lazima Serikali itapata *shares* ambazo zinafahamika *Free Carry Interest*, ambazo, hakuna *standard* ya kidunia kwamba *Free Carry Interest* lazima iwe asilimia ngapi.

Kinachofanyika pale kwenye majadiliano ya mkataba wa madini ndipo pale timu yetu kwa upande wa Serikali na timu a upande wa wawekezaji wanajadili kuweza kupata muafaka wa asilimia ngapi Serikali inaweza kupata *shares* katika uwekezaji wa madini na hiyo inazingatia hali halisi ya kifedha na masoko, kwa maana ya *financial models* na hali ya *ki-commercial*, kwa maana ya mradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi ambayo ipo katika majadiliano kwa sasa ni pamoja na mradi wa *Uranium* ambao ni wa Mkuju.

Serikali inaendelea kujadiliana kuhusiana na mkataba wa madini na sehemu ambayo tunajadiliana kwa kina ni *shares* za Serikali, kwa maana ya *Free Carry Interest* ni asilimia ngapi serikali itapata na kuweza kushiriki katika maamuzi na kushiri katika bodi na ikiwezekana kwenye *managemant* katika migodi husika. Timu zinaendelea kufanya hiyo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba tunazingatia kipengele hicho cha sheria.

Kwenye sheria ya madini ya vito, ni kweli inatamka wazi kwamba madini ya vito yachimbwe na Watanzania na pale inapobidi, Mtanzania anapohitaji mtaji zaidi ama kampuni ya Kitanzania inapohitaji teknolojia zaidi kutoka nje, sheria inatoa ruhusa kwa kushiriki au kumkaribisha mwekezaji wa kigeni kwa asilimia 50 kwa 50.

Hilo tumelifanya katiaka mgodi wa *Tanzanite* ambako Serikali hivi sasa imeweza kuchukua asilimia 50 ya uwekezaji katika Mgodi wa *Tanzanite One* kule Arusha Mererani, na tunaendelea na majadiliano ya namna gani ule muundo sasa wa kushirikiana utafanya kazi baina ya mwekezaji na Serikali.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA. Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika Sera ya Taifa, Sera ya Taifa kwa ujumla inazungumzia habari ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo wa madini.

Mpaka sasa bado sijaona hatua yoyote inayoendelea hasa katika maeneo ambapo wachimbaji wadogo walipo. Kwa mfano kule Geita, sehemu za Rwamuagasa na Nyarugusu. Kwa kweli wachimbaji hao wanauliza sasa ni lini serikali itaanza kuawapa mitaji na kuwawezesha wachimbaji hawa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba, kwamba Serikali inafanya mipango gani ya kuwazesha wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo Tanzania ni wale wenye leseni na wapo watu wengine ambao wanafanya shughuri za uchimbaji katika maeneo yenye leseni za watu wengine, nao tunawaita wachimbaji wadogo.

Serikali ilitambua kwamba, wachimbaji hawa, walikuwa hawako *organized* na walikuwa hawako *formalized* sasa kazi ya kwanza, kabla hujaanza kuwapa misaada lazima uwatambue, uwa-*organise*, uwa- *formalize* kazi ambayo tumeifanya na Mheshimiwa Mbunge anatambua, mwezi kumi na mbili mwaka jana, tarehe 6 tulikuwa na kikao hapa Dodoma cha wachimbaji wadogo wadogo. Kwa maana ya kwamba serikali imeunda chama cha Wachimbaji wadogo wadogo rasmi, kunzia ngazi ya chini ya Kata na Rwamgasa ikiwa ni eneo husika, ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Tunao uongozi sasa wa Wachimbaji wadogo wadogo na tuna *data base* ya wachimbaji wadogo.

Hatua hiyo tulipoimaliza, hatua inayofuata sasa ni kuyatambua mahitaji yao na kuanza kuwatekelezea kuwapa.

Kwa kuyatambua mahitaji yao, tumeanza kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo, ambayo ilikuwa ni kilio cha muda mrefu. Tumetenga eneo maeneo ya Mgusu kule Geita, tumewapatia leseni wachimbaji wadogo vikundi vipatavyo 20. Kuna maeneo kule Chunya, kuna Kikundi cha Mtundasi tumewapatia maeneo na tunaendelea kuangalia maeneo mengine, kutenga maeneo mengine kadri tunavyoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya wachimbaji wadogo, zamani walikuwa wakipewa tu. Sasa tumeamua mikopo hii tutaielekeza benki, kupitia *TIB* ili wachimbaji wadogo waweze kutunza *record* zao za shughuli zao, kiasi gani wanapata, *cash flow* tuione, ili waweze kulipa kodi na sisi tutawapa mikopo; ambaye hatunzi *record*, ambaye halipi kodi, hata *qualify* kupata mkopo.

NAIBU SPIKA: Tuendeleo na Wizara ya Fedha Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Amina M. Mwidau.

Na. 88

Deni la Taifa

MHE. AMINA M. MWIDAU aliuliza:-

Deni la Taifa limekuwa likiongezeka kwa kasi kikubwa mwaka hadi mwaka. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na deni hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM)
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maluum, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabaliana na ukuaji wa Deni la Taifa, Serikali imeandaa na inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Madeni (*National Debt Strategy*) ambayo inazingatia na kukopa zaidi kutoka kwenye vyanzo vyenye masharti nafuu kama vile Mashirika ya Fedha ya Kimataifa na Nchi wahisani na kuhakikisha kwamba tunalipa deni na riba iliyoiva kulingana na makubaliano katika mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ni pamoja na Serikali kuchambua athari zinazotokana na mkopo mipya kabla ya kukopa; na kukopa kwa kuzingatia viashiria vya uvumilivu wa Deni la Taifa.

Pia mikopo yenye masharti ya kibiashara inakopwa kwa ajili ya maeneo maalumu yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi. Vile vile, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wadeni wa *Non Paris Club* ili kutufutia madeni na riba zilizoiva.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 ilisimamisha utoaji wa dhamana kwa Taasisi na Mashirika ya umma, kutoa dhamana kwenye miradi itakayochochoea ukuaji wa uchumi kwa haraka na pia imesitisha utoaji wa dhamana kwa taasisi binafsi isipokuwa kwa miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 4 Januari, 2013, Taasisi moja isiyo ya Kiserikali inayojishughulisha na masuala ya deni la Taifa na Maendeleo, ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari, ikiikosoa Serikali kwa matumizi mabaya ya pesa za umma na vilevile ilionyesha wasiwasi mkubwa sana kutokana na deni la taifa linavyokuwa, sasa hivi liko shilingi trilioni 22 na Serikali ilijibu kupitia Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Mbene, kuwa, bado Tanzania inakopesheka na inaamikia na Taasisi za Kimataifa, *World Bank* na *IMF*. Vilevile Tanzania ina rasilimali nyingi ambazo inaweza ikazitumia kwa ajili ya kuweka rehani ili iweze kupata mkopo huo. Naomba Kauli ya Serikali, atuhakikishie hapa Bungeni, kuweka rehani huko kunakofikiriwa kwa rasilimali za Watanzania wa sasa na kizazi kijacho, hakutakuwa na madhara yoyote kwa nchi? Wasiwasi wangu nchi isije ikauzwa sasa!

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Bunge ni Mhimili mmojawapo wa dola na ni kazi mojawapo ya Bunge kuisimamia Serikali iliyoko madarakani, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kuwa sasa hivi ni wakati

mwafaka wa kuleta Muswada Bungeni itakaotunga sheria itakayoitaka Serikali kutokopa mahali popote pale mpaka ipate ridhaa ya Bunge, kwa kuwa mikopo mingine haina faida kwa Watanzania, inawaongezea mzigo? Ahsante. (Makofi)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kutoa shukrani kwamba hii ni nafasi kwa Taifa zima kufahamu hali halisi ya deni la Taifa. La kwanza Mheshimiwa Mbunge anataka tumwondolee wasiwasi kulingana na hali ilivyoelezwa na Taasisi fulani binafsi kwamba mwenendo wa deni la Taifa siyo mzuri, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wabunge wote na kwa kupitia Bunge hili, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao katika hali halisi ya deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Taifa, tumefanya tathmini ya kutosha na kufikia tarehe 31 Oktoba mwaka uliopita, miezi miwili iliyopita, tulikuwa na jumla ya thamani ya deni la Taifa ya *13.7 billion dollars* na hii ni sawa na hela ya Tanzania *21.0 Trillions* na katika hili deni, *10.5 billion dollars*, ni *external debts*, yaani ni hela ya thamani tuliyokopa nchi za nje, wakati *3.2 billion dollars* ni *domestic debts*, hii ikiwa sawa na *Tshs. 5.1 Trillion* ni *domestic debts* na *15.9 Trillions* ni *external debts*, jumla ni *21.0* kwa thamani ya Tanzania. Deni hili ni nyongeza ya *456.1 million dollars* ukilinganisha la *position* ya nchi ilivyokuwa Oktoba 31, 2011, ongezeko hili siyo kubwa sana!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliguna kutokubaliana na kauli ya Waziri kuwa deni siyo kubwa sana)

WAZIRI WA FEDHA: Nitaeleza, ni ongezeko la 4.6 *billions*. Sasa nitakupa tathmini, tuna utaratibu ambao tunapima uhimilivu wa deni kwa kukubaliana na takwimu za Kimataifa na katika hilo tunapima vipimo vya aina mbili, kipimo cha kwanza ni cha uhimilivu wa deni la Taifa kwa muda mrefu yaani *solvency* na tunachukua vipimo vitatu na tunakaguliwa Kimataifa. Sasa kwa tarehe hiyo ambayo nimewaeleza, miezi miwili iliyopita, tunapima vipimo vitatu kwa uhimilivu wa deni la Taifa na kuji-*benchmark* na *limits* za Kimataifa. Kwa hivyo, kipimo cha kwanza, tunachukua thamani ya deni kwa leo, ni asilimia ngapi ya *GDP*, ambapo, hali ya deni la Tanzania ilikuwa iko 18.9% na *limit* ambayo ni *benchmark* ni 50% kwa hiyo, tuko *still very low*.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)

WAZIRI WA FEDHA: Naomba nimalizie, kipimo cha pili, ni thamani ya deni, ukilinganisha na *GDP* yaani pato la Taifa, ambapo tulikuwa asilimia 56.2 wakati kipimo cha mwisho tusivuke asilimia 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha tatu cha *solvency*, ni kipimo cha thamani ya deni kwa leo ukilinganisha na mapato ya Taifa, ambapo tulikuwa asilimia 111.3 na *limit* yake ni asilimia 300, hiki ni kipimo cha ustahimilivu wa Taifa katika muda mrefu, lakini kipimo cha pili cha tunachopima ni *liquidity position* yaani ukwasi wa Kitaifa wa deni. Kwa hiyo, kipimo cha kwanza tunapima uwezo au hali yaku-service madeni ambayo tunalinganisha na mapato ya nchi za nje, ambapo ilikuwa 2.5% lakini tunatakiwa tusizidi asilimia 25 ya mapato yetu ya Kitaifa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waziri, naona pamoja na majibu yako bado kuna maswali mengi tu ya nyongeza. Mheshimiwa Richard Ndasa na swali la mwisho la nyongeza atauliza Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kwa kifupi sana.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na maelezo marefu ya Waziri ya darasani lakini naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, pamoja na maelezo yako, wapo wazabuni wa ndani wengi wanadai zaidi ya miaka mitatu, minne, Serikali ina mikakati gani ya kulipa madeni hayo? *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, tunapokopa ni lazima tulipe, hili ni sahihi kabisa, sasa hivi karibu tunamalizia, linafanyiwa *debt stop position* ya deni la ndani na Serikali iko katika kuhitimisha ukaguzi ili kuthibitisha ukweli wa kila deni tunalodaiwa. Hatua ya pili tunatengezeza *program* ya ulipaji, kwa hivyo, inapomalizika kuthibitisha kila deni ambalo tumekopa, ambalo tunadaiwa kama Serikali, sasa tanakwenda katika hatua ya pili ya kutengeneza mkakati yaani *programming* kwa ajili ya kulipa hayo madeni yote, ahsante.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali hili.

Kwa kuwa majibu ya Serikali na aliyotoa Waziri ni ya kitaaluma mno au *too academic* kwa wananchi kuelewa namna ya majibu yake, lakini kwa kuwa pia, jibu la msingi la Serikali limezidi kutatanisha kutokana na swali kamili

lililoulizwa, je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza deni la Taifa. Kwa mujibu wa majibu ya Serikali, ni kwamba moja kati ya mkakati huo katika kukabiliana na ukuaji wa deni la Taifa, inazingatia kukopa zaidi kwenye Mashirika ya Kimataifa yenye masharti nafuu. Lingine kutegemea kusamehewa hilo deni, ambalo imedanganya zaidi. Mimi swali langu liko hapa, Mashirika gani hayo ya Kimataifa ambayo ndiyo mkakati wa Serikali kukopa zaidi kwenye Mashirika ya Kimataifa yenye masharti nafuu, masharti gani hayo nafuu ambayo hayana riba? Ni namna gani...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, swali moja tu.

NAIBU WAZIRI, WIZARA YA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakopa katika Mashirika ya Kimataifa, *World Bank, IMF, African Development Bank* na Mashirika mengine, Mashirika hayo ndiyo kwa sasa ambayo yanatoa masharti ya mikopo nafuu, *concessionary loans, concessionary loans by definition* ni kwamba, kunakuwa kuna *25% ya grants elements within that loans*, kwa hivyo, bado tutaendelea kukopa huko kwa sababu ndiyo Mashirika ambayo yanatoa mikopo nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo, hiyo ilikuwa ni *conventional, ni tradition way of borrowing*, Serikali sasa tuko katika mchakato kufanya *credit rating, sovereign credit rating* ambayo, itatusababisha sasa twende katika masoko mengine ya fedha, ambayo ni zaidi ya *IMF, World*

Bank, African Development Bank, OPEC Fund for International Development. Kwa hiyo, bado tutaendelea kukopa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mohamed Mnyaa alikuwa akilalamika sana, kwamba majibu yanayotoka Wizara ya Fedha ni magumu sana. Tunaendelea na Wizara hiyo, Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 89

**Mafao ya Waliokuwa Wafanyakazi wa
Mashamba ya Mkonge Nchini**

MHE. ZAINAB R. KAWAWA aliuliza:-

Tangu kubinafsishwa kwa Mashamba ya Mkonge mwaka 1998, watumishi wa mashamba hayo hawajalipwa mafao yao:-

Je, ni lini watumishi hao watalipwa mafao yao?

NAIBU WAZIRI, WIZARA YA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, si kweli kwamba tangu kubinafsishwa kwa Mashamba ya Mkonge, mwaka 1998, Watumishi wa

mashamba hayo hawakulipwa mafao yao. Ukweli ni kwamba, watumishi wote walilipwa mafao yao lakini kulikuwa na mapunjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba, 2010, Wizara yangu kupitia *Consolidated Holdings Cooperation* ilipokea madai ya mapunjo ya watumishi wa Mamlaka ya Mkonge yanayofikia shilingi bilioni 2.187 na kwamba, mwezi Novemba, 2010, Serikali iliunda Kamati Ndogo iliyowashirikisha maofisa kutoka *CHC* na Bodi ya Mkonge Tanzania kufanya uhakiki wa kina wa madai hayo. Baada ya uhakiki kufanyika, ilibainika kuwa kulikuwa na mapunjo ya kiasi cha shilingi bilioni 2.18. Taarifa ya Kamati iliwasilishwa Serikalini kwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Mei, 2012, Serikali kupitia Wizara yangu ilitoa jumla ya shilingi bilioni 2.18 yaani kiwango chote kilichokuwa kinadaiwa kwa ajili ya mapunjo ya wafanyakazi 10,700 kulingana na mapendekezo ya taarifa ya uhakiki. Malipo yote yaliyohakikiwa yalianza kulipwa mwanzoni mwa mwezi Julai, 2012 na yaliratibiwa na *CHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, malipo ya madai ya mirathi yanatarajiwa kuanza kulipwa mwezi huu wa Februari 2013, baada ya wawakilishi au wasimamizi wa mirathi kukamilisha taratibu za kisheria za mirathi.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali lingine la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, tatizo la madai ya mapunjo ya waliokuwa watumishi wa mashirika ambayo yalibinafsishwa na Serikali limekuwa la kihistoria sasa, kwanza, kumekuweko na ucheleweshwaji mkubwa sana wa kulipa madai hayo. Nitayataja baadhi tu ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa ambayo mpaka sasa kuna malalamiko ya aina mbalimbali ya waliokuwa watumishi ambao ama wanadai mapunjo ama hawajalipwa stahiki zao mpaka sasa. Mfano, *NAFCO* Mbalari, *SPM* Mgororo, Polyester, Mtibwa na Kilombero, kwa uchache wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie, Serikali haioni haja sasa ya kufanya *general assessment* ya mashirika yote ambayo yamebinafsishwa ili kubaini ni kiasi gani cha jumla, ambacho waliokuwa watumishi wanadai, ili iweze kutenga fungu na hatimaye kulipa ili kuondokana na mgogoro huu ambao umekuwa endelevu siku hadi siku, nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, WIZARA YA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE) Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa ushauri, kwa kweli kumekuweka na ucheleweshwaji kutokana na kuwa lazima malipo haya yafanyiwe uhakiki na haswa yale yanayohusiana na mapunjo, pamoja na stahiki mbalimbali ambazo zilikuwa zimesalia, nyingi zikiwa ni za mashirika ya *pension*, malipo ya *pension*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa, sasa hivi *CHC* wako katika mchakato wa kuhakiki madeni kamili tunayodaiwa Serikalini kwa ajili ya kufanya mkakati

wa kuyalipa na hili ni zoezi ambalo limekuwa likiendelea kwa muda lakini sasa hivi tutaendelea kulishinikiza lifanywe kwa haraka sana, nashukuru sana.

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wamesimama kuomba nafasi ya kuuliza swali la nyongeza)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya sana, muda uliobaki ni mdogo kwelikweli na nina maswali karibu saba, bado robo saa, kwa hiyo, naomba mniwie radhi sana.

Na. 90

Ujenzi wa Barabara ya Nzega-Tabora

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Nzega - Tabora kwa kiwango cha lami haujakamilika:-

(a) Je, ni lini ujenzi huo utakamilika na kwa nini pesa za malipo ya awali kwa Makandarasi zinachelewa?

(b) Je, kwa nini Mkandarasi hajengi barabara ya huduma wakati akiendelea na ujenzi wa barabara yake?

(c) Je, kwa nini wananchi waliobomolewa nyumba zao hawajalipwa fidia wakati barabara iliwakuta?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Nzega-Tabora yenye urefu wa kilomita 114.9 kwa kutumia fedha za ndani (GOT) unaendelea kutekelezwa kimkataba na umegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya Nzega-Puge yenye urefu wa kilomita 58.8 inatakiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2014 na Sehemu ya Puge-Tabora yenye urefu wa kilomita 56.1 inatakiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2014.

Kuhusu malipo ya fedha za awali, Makandarasi wote wawili wamelipwa malipo yote ya awali ya asilimia 15 ya gharama ya mradi, ambapo Mkandarasi wa sehemu ya Nzega-Puge amelipwa kiasi cha shilingi 1,445,788,294.10 na dola za Kimarekani 6,060,077.32 na Mkandarasi wa sehemu ya Puge-Tabora amelipwa kiasi cha shilingi 1,574,645,735.79 na dola za Kimarekani 4,707,355.55. Malipo yalifanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba, Mkandarasi anatakiwa kuifanyia matengenezo njia ya mchepuo kwa kipindi chote inachotumika ili iwe inapitika vizuri. Haya ni matakwa ya kimkataba na pale ambapo Mkandarasi hafanyi hivyo, anatakiwa kuchukuliwa hatua za kimkataba. Wakala wa barabara itahakikisha Mkandarasi anazingatia hitaji hili la kimkataba.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wananchi waliokuwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara mita 22.5

katika vijiji vya Nkiniziwa na Busondo. Mnamo mwezi Februari mwaka 2012, walipewa notisi ya kuvunja nyumba zao wenyewe bila kulipwa fidia yoyote kwani nyumba zao zilikuwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara ya mita 22.5, kinyume na matakwa ya Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na walitii na kuvunja nyumba zao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wananchi ambao wanastahili kulipwa fidia katika sehemu ya Nzega Puge, kazi ya uthamini imekamilika na kiasi cha shilingi milioni 858,555,505/= kitalipwa baada ya taratibu za malipo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu ya Puge - Tabora fidia yenye kiasi cha shilingi milioni 42,478,288.69 imelipwa kwa eneo la Tabora Mjini. Pia, kiasi cha shilingi milioni 367,302,949.10 kitalipwa kwa wananchi wanaostahili baada ya Serikali kukamilisha taratibu za malipo ya fidia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla swali la nyongeza!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, niseme si sahihi kwamba barabara za mchepuo zimetengenezwa lakini zimekuja kutengenezwa juzi hapa baada ya Mheshimiwa Rais kuwa anakuja Nzega. Sasa naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mimi nashindwa kuelewa ni kwa nini wananchi wa vijiji vya Nkiniziwa na Busondo wanavunjiwa nyumba zao kwa kisingizio kwamba wamejenga katika eneo la hifadhi ya barabara wakati ninavyofahamu mimi na pale kuna

Babu yangu ambaye nyumba yake pia itavunjwa, alikuwepo pale kabla nchi hii haijapata uhuru na akajenga nyumba yake pale kabla hizi sheria wanazosisema hazijakuwepo, yeye alikuwepo pale, lakini leo hii inasemekana nyumba yake ivunjwe kwa sababu amejenga kwenye eneo la hifadhi ya barabara. Hili sikubaliani nalo na ninaomba nipatiwe majibu ya uhakika ambayo yataweza kuwashawishi wananchi wa Kata ya Nkiniziwa, Busondo na maeneo mengine ambapo kuna tatizo kama hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kumbukumbu za *Hansard* wakati barabara hii ikifanyiwa upembuzi yakinifu, Mheshimiwa Mbunge aliyenitangulia Ndugu Lucas Lumambo Seleli, aliomba kilomita 10 za lami zijengwe pia katika Mji wa Nzega kama ambavyo sheria zinataka, na hili lilikubaliwa na Serikali lakini hii leo hakuna kinachoonyesha kwamba mji wa Nzega patajengwa kilomita 10 za lami.

NAIBU SPIKA: Sasa swali!

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGWALLA: Sasa Serikali inasemaje kuhusiana na hili? Nakushukuru!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Dkt. Kigwangalla, majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi! Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, karibu sana Bungeni!

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ndiyo majibu halali ya Serikali lakini pili, tumeeleza katika jibu letu la msingi kwamba wananchi watakaohusika kulipwa fidia ni wananchi waliopo katika eneo la Nzega ambapo tunatengeneza *diversion* ya barabara ya kutoka Nzega

kwenda Puge hadi Tabora haitapita Mji wa Nzega na itapita pembeni mwa barabara kama kilomita 4 – 5 na wale wahusika wote watalipwa fidia ya shilingi milioni 858.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kwamba Babu yake amekuwepo kabla ya kupata uhuru, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwamba sheria hii imeanza kabla ya kupata uhuru. Sheria hii ilianza tangu mwaka 1932 ikafanyiwa *amendment* mwaka 1949, ikafanyiwa *amendment* mwaka 1954 na ikafanyiwa *amendment* nyingine kupitia CAP.167 ya mwaka 1967 na upana wa barabara ulikuwa unazungumzia mita 22.5 kila upande. Lakini imefanyiwa marekebisho mengine kupitia Sheria Namba 13 ya mwaka 2007 na ikapitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi pamoja na Mbunge Kigwangalla kuwaelimisha wananchi wajibu wa kutekeleza sheria na jukumu la Serikali ni kuhakikisha kwamba wale wanaofuatwa na barabara wanalipwa fidia na wale wanaoifuata barabara watabomolewa. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wamesimama kuomba nafasi ya kuuliza swali la nyongeza)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata kama nilivyosema kwa sababu ya muda, swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga.

Na. 91

Ujenzi wa Barabara ya Kyaka – Bugene

MHE. ELIZABETH N. BATENGA aliuliza:-

(a) Je, ni lini kazi ya ujenzi wa barabara ya Kyaka – Bugene iliyoko Karagwe itaanza rasmi?

(b) Je, fedha kiasi gani kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Kyaka – Bugene Kilomita 59.1 ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 64,969,980,429. Kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 15 Desemba 2010 na zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014.

Mpaka sasa kazi zifuatazo zimefanyika:-

- (i) Kuinua tuta la barabara kilomita 11.8
- (ii) Ujenzi wa tabaka la kwanza la msingi (*Sub Base*) kilomita 7.9
- (iii) Ujenzi wa daraja la Mwisu 25%
- (iv) Ujenzi wa makalvati makubwa (*box culverts*) 7
- (v) Ujenzi wa makalvati madogo (*pipe culverts*) 44

Aidha, maendeleo ya jumla ya mradi hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2012 yalikuwa 23.4%.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2012/2013 kiasi cha shilingi bilioni 4.572 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niseme kwamba wananchi wa Mkoa wa Kagera wamepokea kwa shukrani ujenzi wa barabara hii lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba barabara hii imepangwa kujengwa katika kipindi cha miaka mitatu na nusu au minne hivi lakini sasa hivi kipindi kilichobaki ni mwaka mmoja na nusu tu. Je, naomba nielezwe mikakati ambayo Serikali inayo au Wizara ya Ujenzi inayo ili kuhakikisha kwamba barabara hii itakamilika katika muda uliopangwa yaani mwezi Juni, 2014?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, barabara hii inayojengwa ni nzuri lakini pengine na ndivyo ilivyo kwamba itakidhi haja sana kama sehemu sasa ya barabara ya Begene - Kasulu itajengwa na ambayo itakuwa imeunganisha nchi tatu za Afrika Mashariki yaani Burundi, Rwanda, Tanzania na Uganda. Naomba nijibiwe.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, naomba niwahakikishie wananchi wa Kagera kwamba barabara hiyo itakamilika kwa muda uliopangwa kwenye mkataba. Hatukubali kisingizio chochote cha kuchelewesha kazi. Wakati tunatoa kazi kwa wakandarasi kwanza huwa tunapima uwezo wao wa kujenga, wataalamu na vifaa pamoja na uwezo wa kukopesheka kifedha. Kwa hiyo, mkandarasi asije akachelewesha kazi kwamba sijui *certificate* imechelewa, hiyo sababu haikubaliki! Kwa hiyo, kazi hii itamalizika kwa muda uliopangwa na kama atachelewesha basi hatua zinazostahili zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu wazo lake la kwamba barabara ijengwe ya mpaka Kasulu, naomba niseme kwamba wazo hilo tunalipokea na Serikali itaangalia namna gani tunaweza tukatekeleza mawazo hayo.

Na. 92

Jeshi la Wananchi Kutumika Kuzuia Maandamano

MHE. KHALIFA S. KHALIFA aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilitumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuzuia maandamano:-

(a) Je, ni sahihi ikizingatiwa kuwa Jeshi hilo haliko Kikatiba kufanya kazi hiyo?

(b) Je, uamuzi huo si sawa na kuligombanisha Jeshi na raia kwa kuwa Jeshi limefundishwa kuua na siyo kuzuia maandamano?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 147 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 21 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa, namba 192 ya mwaka 2002, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaruhusiwa kushirikiana na Mamlaka za Kiraia kudumisha amani na usalama hapa nchini. Kwa msingi huo, Jeshi linapodhibiti maandamano yenye sura ya kuhatarisha amani linafanya hivyo kwa kuzingatia Katiba ya nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania limefundishwa kuua kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Mbali na majukumu ya ulinzi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania pia limepewa mafunzo maalum ya kukabiliana na vurugu bila kuleta madhara makubwa kwa raia na mali zao. Kwa mantiki hiyo, ni sawa kulitumia Jeshi ili kukabiliana na vurugu pamoja na uvunjifu wa amani na wala kufanya hivyo hakuligombanishi Jeshi la Wananchi wa Tanzania na raia kwa sababu linafanya hivyo ili kutekeleza wajibu wake kwa Taifa letu.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaonekana *Brother* wangu viti vikubwa vinamnukia, Mungu amjaalie apate kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, inakubalika bila ya swali kuwa Jeshi ndiyo msuli wa mwisho katika nchi yoyote wa kuonyesha nguvu ya dola na kwa kuwa, imezuka tabia hivi karibuni Jeshi letu linatumika katika kuzuia hata maandamano ya wanafunzi. Sasa napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, hii ndiyo utekelezaji wa hiyo Ibara ya 147 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama alivyosema? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sote tunaelewa na wengi tunaelewa kuwa Polisi na vikosi vingine vinafundishwa kukabiliana na ghasia ndogondogo yaani *anti-riot squats* lakini Jeshi dunia nzima linafundishwa kupambana na maadui wa nchi nyingine *and they are trained to kill*. Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ameweka *categorically* kuwa si kweli Jeshi limefundishwa kuua, je, Mheshimiwa Waziri ana hakika na kauli yake hiyo? (*Kicheko*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Jeshi la Wananchi wa Tanzania pale inapobidi, yanapotokea maandamano na hasa wanaporidhika kama maandamano hayo yanaweza kuhatarisha ulinzi, usalama na utulivu wa nchi yetu kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa, namba 192 ya mwaka 2002, Jeshi hilo linaweza kutumika. Sasa kama maandamano yenyewe ni ya wanafunzi wa shule au kama maandamano yenyewe ni ya Madaktari au maandamano

yenye ni ya wakulima, hilo si jambo la msingi. Jambo la msingi ni kwamba maandamano hayo yana dhamira gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, amesema nina uhakika kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeelimishwa au limefunzwa kuua. Jeshi linaua pale ambapo wanadhani kwamba ni lazima kufanya hivyo na siyo kila wakati Jeshi la Wananchi wa Tanzania linafanya hivyo. Sisi wenyewe hapa ni mashahidi, kuna wakati Jeshi hilihili la Wananchi wa Tanzania tunalitumia katika kusomba mazao kutoka Mikoa mbalimbali, Jeshi hilihili! Lakini yanapotokea maafa, Jeshi hilihili ambalo tunaambiwa limefunzwa kuua linatumika katika kukabiliana na maafa, kuwasaidia wananchi kwa kutekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la kuua linategemea umekabiliana na tishio la kiasi gani, hata raia wanaua na wala hawakufundishwa kuua. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wamesimama kuomba nafasi ya kuuliza swali la nyongeza)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa ni swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha. Waheshimiwa Wabunge ni kwa sababu ya muda, mniwie radhi sana, kweli!

Sare za Jeshi Kutumiwa na Wezi

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha sare za Jeshi letu ili kudhibiti wimbi la uhalifu kwa kuvaa mavazi hayo unaofanyika kirahisi zaidi na kulidhalilisha Jeshi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salim Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya sare za Jeshi yanayofanywa na wahalifu hayatokani na sare hizo kukosa ubora bali yanatokana na namna sare hizo zinavyodhibitiwa. Kwa mantiki hiyo, Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kudhibiti wimbi la uhalifu unaofanywa na watu wanaovaa mavazi ya kijeshi. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Jeshi la Wananchi linawahimiza Wanajeshi kuzitunza vizuri sare zao ili zisivaliwe na watu wasiohusika;

(ii) Jeshi la Wananchi hufanya doria katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti uvaaji wa sare za Jeshi kwa watu wasiohusika na wanaokamatwa hufikishwa kwenye vyombo ya sheria;

(iii) Jeshi la Wananchi linawakataza wafanyabiashara wa mitumba na maduka ya nguo kuagiza na kuuza mavazi yanayofanana na sare za Jeshi; na

(iv) Jeshi la Wananchi linayakataza Makampuni ya Ulinzi yasitumie sare zinazofanana na sare za Jeshi la Ulinzi.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu kidogo ambayo hayajaniridhisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa majuzi tu kuna tukio lilitokea kwa Waheshimiwa Wabunge wawili yaani Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Nassari waliweza kumfuatilia mtu kwa ndani kabisa, wakapiga naye picha na wakabaini kuwa mtu yule alikuwa kavaa sare ya Jeshi la Wananchi kwa takribani miaka mitatu. Je, sasa Serikali haioni kwamba kuna watu wengine ambao wako kama walewale na wakifuatilia kwa kina humo ndani ndani watakuta kuna watu kama wale?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sare za Jeshi la Wananchi zimekuwa zikiuzwa kwenye maduka na hata wasanii kutumia sare hizi katika kuimba muziki yao. Je, Serikali haioni kama pia ni tatizo kwa Wanajeshi wetu?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, ni kwamba hairuhusiwi kwa watu wasiohusika kuvaa sare za Kijeshi. Sasa kama anavyosema ni kweli wako watu wamebainika kwamba kwa muda wa miaka mitatu wakizitumia sare hizo, nafikiri hii ni taarifa ambayo inatufaa sisi kama Serikali kuifanyia kazi. Lakini bado tunasisitiza kwamba tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali na bado ninapenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea

kufanya hivyo kwa sababu sare hizi zikiendelea tu kuzagaa zinaweza kuwa ni chanzo kikubwa sana kinachoweza kuwasaidia wahalifu kuendelea kufanya vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, wapo wasanii ambao wamekuwa wakitumia sare ambazo zinafanana sana na sare za kijeshi. Narudi tu kusema kwamba ni marufuku kwa watu wasiohusika kuendelea kutumia sare ambazo zinafanana na mavazi ya Kijeshi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuwasaka na wale ambao tutaridhika kwamba wana mavazi ambayo yanafanana na sare za Kijeshi hatutasita kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria.

Na. 94

Kuboresha Idara ya *Physiotherapy*

MHE. CYNTHIA H. NGOYE aliuliza:-

Idara ya *Physiotherapy* inaendelea kuwa na umuhimu mkubwa kila siku kutokana na sababu nyingi ikiwemo kuongezeka kwa ajali, maradhi ya kiharusi n.k:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Idara hiyo kitaalum, vifaa na majengo?

(b) Je, kuna vyuo vingapi Kitaifa vinavyotoa mafunzo ya wataalam wa *physiotherapy*?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za *Physiotherapy* ni huduma muhimu sana hasa kwa wakati huu ambapo magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanaongezeka zikiwemo ajali. Serikali kwa kutambua hilo, inaendelea kuboresha huduma za *Physiotherapy* katika hospitali zake ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vinavyohitajika kutolea huduma hizo. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuzipandisha hadhi Hospitali zote za Mikoa kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa. Ngazi hii mpya itaziwezesha hospitali hizo kupatiwa wataalam wanaohitajika kutoa huduma hizo.

Aidha, Wizara inapitia michoro ya majengo katika vituo vya huduma ili kuhakikisha kuwa Idara muhimu zikiwemo zile za *Physiotherapy* zinapata nafasi ya kutosha ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kipo chuo kimoja tu cha Serikali kinachotoa mafunzo ya wataalam wa *Physiotherapy* ngazi ya Stashahada. Chuo kipo KCMC Moshi, kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 30 kwa mwaka. Kilianza mwaka 1980, kufikia mwaka 2012 jumla ya wahitimu wa fani ya *Physiotherapy* ni 343. Kwa sasa chuo kina uwezo wa wanafunzi 69, mwaka wa kwanza hadi wanne.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya *Physiotherapist* nchini ni zaidi ya wataalam 10,000 kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani ambapo kila asilimia 10 ya watu wanaohitaji huduma ya *Physiotherapy* na *Physiotherapist* mmoja anatakiwa kuhudumia watu 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Makumira (Kilimanjaro *Christian Medical University College*), kinatoa Shahada ya *Physiotherapy* (*Bsc Physiotherapy*) kikishirikiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha KCMC. Kozi ya Shahada ya *Physiotherapy* ilianza kutolewa mwaka 2004, Chuo kikiwa na uwezo wa wanafunzi 25 kwa mwaka. Kuanzia mwaka 2004 hadi 2012, wanafunzi waliohitimu ni 36, yaani mwaka 2008 (wanafunzi 8), 2009 (5), 2010 (7) na 2012 (9). Muda wa mafunzo ni miaka mitatu (3) kwa walioko kazini na miaka minne kwa wanaojiunga baada ya kuhitimu kidato cha sita.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ametwambia kwamba mahitaji ya wataalam wa *Physiotherapy* hapa nchini ni zaidi 10,000 na tulionao ni wataalam 343 tu, takwimu ambazo mimi naona kwamba bado Serikali haijaona umuhimu wa Idara hii. Je, ni kwa nini basi kutokana na takwimu hizo ndogo namna hiyo isianze kufikiria hivi sasa kuanzisha Idara ya mafunzo kama hayohayo pamoja na jitihada za hivyo Vyuo vingine pale Chuo Kikuu cha Tiba cha Afya Muhimbili, kwa nini wasianze kufikiria hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ina mkakati gani hivi sasa kuanzia kupeleka wataalam kujenga majengo katika hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya kutokana na ongezeko kubwa sana la ulemavu ambao unazidi kuongezeka hivi sasa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na ajali nyingi zinazotokea na wengi sana wapo katika vijiji. Je, mkakati huo utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:
Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia ya dhati ya kuongeza wataalam hawa na ndiyo sababu Chuo Kikuu cha *KCMC* kimeongeza kozi ya Shahada. Lakini vilevile bado tutaendelea kuuangalia uwezekano wa kuongeza kozi za Stashahada ili kuongeza idadi kwa kasi zaidi ya upatikanaji wa wataalam hawa katika vyuo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza majengo kwa maana ya kuweza kupata fursa ya wataalam hao kutoa huduma zao, kwa sasa lengo ni kuziboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa kama nilivyoeleza katika jibu la msingi na kazi hiyo itakuwa inaendelea kwa makusudio ya kupata eneo. Kwanza mchoro, kupata eneo, kupata vifaa na hao wataalam wenyewe wakawepo katika hospitali zetu za Mikoa na baada ya pale fedha kuteremka kufika katika hospitali za Wilaya.

Na. 95

Tatizo la Mabaraza ya Ardhi Nchini

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY aliuliza:-

Serikali ilipojibu Swali Na.337 kwenye Kikao cha Nne katika Bunge la 10 kuhusu Mabaraza ya Ardhi Nchini iliahidi kuanzisha Mabaraza hayo kwenye Wilaya zote nchini licha ya kwamba uendeshaji wa madai ya mashauri ya ardhi kwenye Mabaraza hayo yameendelea kuwa tatizo sugu na sehemu nyingi imeshindikana kuanzisha Mabaraza hayo na kwenye Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi kimevunjwa na madai ya ardhi kusikilizwa na Majaji wote:-

Je, kwa nini Serikali isiamue kuvunja Mabaraza ya Ardhi na kuwa na chombo kimoja chenye kuamua mashauri -Mahakama?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kuwa wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi, nililijulisha Bunge lako Tukufu, nia ya Serikali ya kuanzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwenye Wilaya zote nchini. Napenda kuthibitisha kuwa nia hiyo bado ipo kama ilivyothibitishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010. Changamoto inayotukabili kwenye utekelezaji wa maelekezo hayo ni upungufu wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Mabaraza. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushirikiane ili kuhakikisha kuwa Mabaraza hayo yanapewa kipaumbele kwenye bajeti ijayo ili tuweze

kufikia lengo tulilowekewa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kuanzisha Mabaraza Kumi 10 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaanzishwe mwaka 2004, yamepunguza migogoro ya ardhi na nyumba iliyokuwepo kwa muda mrefu na inayofunguliwa, inashughulikiwa ndani ya miezi miwili. Kwa sababu hiyo, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuyavunja Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na kurejesha mamlaka za Mahakimu kusikiliza na kutolea uamuzi mashauri ya ardhi na nyumba. Hii ni kutokana na sababu iliyopelekea kuanzishwa kwake Mabaraza hayo ambayo ilikuwa ni kukabiliana na changamoto za mfumo uliokuwepo kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi ya Na. 2 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa baadhi ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yamekuwa na mapungufu yaliyosababisha yasitekeleze wajibu wake ipasavyo, uchunguzi tuliofanya kufuatia malalamiko ya wananchi moja kwa moja na wengine kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge ulibainisha kuwa chanzo cha mapungufu hayo ni udhaifu wa baadhi wa Wenyeviti wahusika. Baadhi ya Wenyeviti wamekuwa wakichelewesha maamuzi ya mashauri wanayosikiliza na wengine walighafilika katika kutoa haki kwa wateja wao. Baada ya uchunguzi huo, Serikali ilichukua hatua zifuatazo ili kurekebisha mapungufu hayo na kuhakikishia kuwa Mabaraza yanatenda kazi zao kwa mujibu wa Sheria.

(a) Wenyeviti wa Mabaraza wawili waliothibitika kukiuka maadili ya kazi zao wameachishwa kazi;

(b) Wenyeviti wa Mabaraza wanne na Afisa mmoja wa Makao ya Kitengo cha Usajili wa Mabaraza wanaendelea kuchunguzwa na uchunguzi utakapokamilika hatua stahiki zitachukuliwa ikiwa itathibitika kuwa wamekiuka maadili ya kazi zao; na

(c) Wenyeviti wa Mabaraza tisa wamehamishwa vituo vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana wananchi na Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa taarifa kwetu juu ya utendaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwani ilituwezesha kufanya uchunguzi na kubaini mapungufu yaliokuwepo na kuyarekebisha. Nawaomba wananchi wote waendeleo kushirikiana na Serikali yao kwa kutoa taarifa pale ambapo wataona kuwa kuna dalili za kunyimwa haki. Kwa upande wake, Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha Mabaraza yaliyopo na kuanzisha mapya kadiri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo kuu hapa ni kuondoa migogoro ya ardhi baina ya wananchi, badala ya kuongeza majengo na kuongeza Wenyeviti wa Mabaraza, je, Serikali inaonaje kuleta huduma ya kupata haki karibu na wananchi ili waweze kumiliki ardhi na kuondoa kumiliki ardhi ambayo haina hatimiliki hasa kwa kutumia mradi wa MKURABITA?

La pili, kwa kuwa, Serikali imeng'angania sasa kuwa Mabaraza haya; na kwa kuwa Wilaya ya Mbulu wananchi wake wanahangaika kusafiri umbali wa maili 130 kufuata Baraza hilo Babati, je, Serikali ina mpango wa kujenga au kuanzisha Baraza hilo haraka iwezekanavyo pale Wilayani Mbulu?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninakubaliana naye kwamba kupanga matumizi ya ardhi, kupima na kuwamilikisha wananchi, itakuwa ni suluhisho la kudumu la kuweza kupunguza au kuondoa kabisa migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, mapendekezo yake kwamba tushirikiane na MKURABITA kwa ajili ya kuweza kutoa huduma hiyo nimelipokea na nitalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwake na Waheshimiwa Wabunge wote ni kwamba tushirikiane kwanza kuhamasisha wananchi wawe tayari kwa ajili ya kukubali kushiriki katika mchakato wa kupanga matumizi ya ardhi, kupima pamoja na kuwamilikisha na wawe tayari kuchangia gharama za upimaji pale ambapo mipango itakapokuwa imekamilika.

La pili, kuhusu Wilaya ya Mbulu kupatiwa Baraza la Ardhi na Nyumba, napenda tu kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tatizo lililopo katika Baraza la Babati ni kwamba limekuwa na Mwenyekiti mmoja. Katika marekebisho haya ambayo nimeyataja katika majibu ya swali la msingi tutampeleka Mwenyekiti wa pili pale Babati ili kuweza kuongeza uwezo wao wa kutoa huduma kwa kutembelea Wilaya ya Mbulu na kufanya maamuzi kule badala ya wananchi kutoka Mbulu kwenda Babati.

Tunauomba uongozi wa Wilaya ya Mbulu wakishirikiana na Mheshimiwa Mbunge watenge chumba kwa ajili ya kazi hiyo.

NAIBU SPIKA: Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Mwanjelwa!

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Mkoa wa Mbeya, ninamshukuru sana Mungu afya yangu inaimarika na sasa nipo kazini.

Na. 96

Umri wa Kuolewa Mtoto wa Kike

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA aliuliza:-

Ili kutoa muda kwa watoto wa kike kusoma na kukua kiakili:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kubadilisha Sheria ya Ndoa ili umri wa kuolewa utoke miaka 14 na kuwa miaka 18?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, mwanaume mwenye umri chini ya miaka 18 na mwanamke mwenye umri chini ya miaka 15 hawaruhusiwi kufunga ndoa na mtu yeyote. Kifungu cha 13(2) kinaipa Mahakama baada ya maombi kuwasilishwa mbele yake, mamlaka bila kujali sharti la kifungu cha 13(1) kutoa kibali cha kufunga ndoa kwa watu wenye umri chini ya uliowekwa na kifungu cha 13(1). Mahakama inaweza kutoa kibali hicho endapo waombaji wamefikisha umri wa miaka 14 na Mahakama ikiridhika kwamba yapo mazingira maalum yanayohitaji wenye umri huo kufunga ndoa. Vilevile, kifungu cha 17(1) kinampa fursa mtoto wa kike mwenye umri chini ya miaka 18 kupata ridhaa ya kuolewa kutoka kwa mzazi wake au mlezi wake endapo baba au mama watakuwa wamefariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa watoto wengi wa kike wamekuwa wakiolewa chini ya umri uliowekwa na Sheria na mara zote hatua za kisheria zimekuwa zikichukuliwa dhidi ya wazazi, walezi na wanaume wanaooa wasichana hao. Tunatambua pia kuwa, kumekuwepo na mijadala mingi juu ya umri stahiki wa mtoto wa kike kuolewa. Kwa kutambua madhara wanayoyapata watoto wa kike kuolewa wakiwa na umri mdogo, Serikali ina nia ya dhati ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa kwa kukusanya maoni yatakayoweza kuboresha sheria hiyo ili kukidhi mahitaji ya jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu

Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza yenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ni mbaya sana, baadhi ya makabila yamekuwa na mila potofu ya kuwakandamiza watoto wa kike katika ndoa za utotoni tena bila ridhaa ya binti hawa na hii yote ni kwa ajili ya tamaa tu kupata mahari. Je, Serikali ina mkakati gani katika kudhibiti jambo hili?

(b) Kwa kuwa hiki kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana sana, Serikali haioni kwamba sasa hivi inachangia kuongezeka kwa vifo hasa ukizingatia katika ile MDG namba *four and five* juu ya *early pregnant* pamoja na hizi mimba za utotoni maana yake madhara yake ni makubwa sana au nilete rasimu ya Sheria yenye hoja binafsi katika mapendekezo juu ya umri wa mtoto chini ya miaka ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu ya msingi, Waraka wa Serikali juu ya kufanyia marekebisho Sheria ya Ndoa upo katika hatua za mwisho, unaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la ndoa, umri wa kuolewa linagusa mila, desturi na imani pia za dini. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iandae Waraka ambao utakusanya maoni ya Watanzania wote, wanawake, wanaume, Waislam, Wakristo wasio na dini ili tuweze kupata muafaka wa umri stahiki wa kumuoza mtoto wa kike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua mtoto wa chini ya umri wa miaka 18 kuolewa inaleta changamoto katika kusababisha mimba za utotoni na pia katika kuacha masomo na vifo pia vya wanawake wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilithibitishie Bunge lako na Watanzania kwa ujumla, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeagizwa na Ilani ya Uchaguzi, Aya 186, kifungu (f) kufanyia marekebisho Sheria zote kandamizi na hili litafanyika kabla ya mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ila kama unavyojua tupo katika agenda nyingine kubwa ya kuandaa Katiba Mpya. Kwa hiyo, tutakapoenda kwa wananchi tunawauliza masuala ya Katiba Mpya *at the same time* tunawaambia masuala ya Sheria ya Ndoa, tutakuwa tunawachanganya. Ni matarajio yangu kwamba Katiba Mpya pia kifungu cha 13 kinachokataza ubaguzi kitaenda mbali na kusema Sheria zote zinazokandamiza wanawake na watoto zitakuwa ni batili. Kwa hiyo, kwa kutumia Katiba Mpya tutaweza kuwahamasisha Sheria hiyo iondoke, lakini pia kwa kutumia Waraka ambao tunauandaa tutahakikisha kwamba tunawalinda watoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize, wanaume jiulizeni kama ni sahihi kumuoa binti wa umri wa chini ya miaka 18, haiwezekani na si busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAUBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli muda hauko upande wetu, na swali la mwisho la Mheshimiwa Amina Andrew Clement nilitaka niliahirishe; lakini naliona ni fupi, naomba mnivumilie tulichukue hilo swali.

Na. 97

Tatizo la Wazazi Kutupa Watoto

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT aliuliza:-

Nchi yetu imeshuhudia matukio mbalimbali ya kuokotwa kwa watoto wanaotupwa na mama zao, jambo ambalo linawanyima haki za msingi za kuishi watoto hao:-

Je, Serikali inalitambua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, kwa kuwa leo ni Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Vitendo vya Ukeketaji, nitumie Bunge lako Tukufu kuwapongeza wasichana wote hasa walioko Tarime waliokataa kufanyiwa vitendo vya ukeketaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wasichana hawa ni mashujaa na nawathibitishia kwamba kuolewa bila ya kukeketwa inawezekana. Ni muhimu sasa hivi watie mkazo katika elimu yao, wakimaliza masomo, wanaume wenye

sifa na vigezo wako wengi na wako tayari kuwaoa wasichana ambao hawajakeketwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haijashindwa kupambana na vitendo vya ukeketaji, tutatumia sheria kuhakikisha wote wanaofanya vitendo hivi wanachukuliwa hatua stahiki. Lakini tutatumia mkakati wa kuelimisha jamii hasa wanaume na wanawake kuachana na vitendo vya ukeketaji dhidi ya watoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement - Mbunge wa Koani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa vitendo vya kutupwa kwa watoto, na ni kweli kuwa vitendo hivi vinawanyima haki yao ya msingi ya kuishi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto kipengele cha 99(i) nukuu isiyo rasmi inasema kwamba: “Mtoto ana haki ya kuishi, kutambulika utu wake, kuheshimiwa, kuthaminiwa, kufurahia utoto wake, uhuru wa kucheza, kupewa huduma za afya, elimu na malazi kutoka kwa wazazi wake.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada mbalimbali kupunguza au kutokomeza kabisa tatizo la watoto wanaotupwa ikiwemo:-

(i) Kuelimisha umma kuhusu haki za mtoto kupitia Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 na Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008;

(ii) Kutoa adhabu kwa wahusika punde wanapobainika kutupa watoto; na

(iii) Kuwapelekea watoto waliotelekezwa katika uangalizi maalum kwenye Vituo vya Kulelea Watoto na kuwaunganisha na wazazi au walezi wanapojitokeza ili watoto warudi kuishi na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa viongozi wa dini, Watanzania wote pamoja na wadau wengine kuendelea kufanya jitihada za kujenga maadili ya msingi kwa vijana wetu na kukemea vitendo hivi vya ukatili dhidi ya watoto.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeweka Vitengo vya Uzazi wa Mpango chini ya Wizara ya Afya na huduma hizo huwa zinatolewa bure, lakini wananchi hawazioni. Wakienda kupata huduma hizo na wanabakia kuzaa ovyo na kuwatupa vichanga hao. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika kuwakamata watu hao watakaotupa vichanga waliokuwa hawana hatia na kuwawekea sheria kali dhidi yao? Pia sheria hiyo iambatane na kifungo cha maisha.

La pili, katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, Serikali inaelimisha umma kupitia Sheria ya Mtoto Namba 21, lakini elimu hii bado haijasikika ipasavyo hasa vijijini. Je, kwa nini Serikali isiamue hivi sasa kuwatumia

Maofisa Maendeleo wa Jamii wa Kata ili sheria hii na elimu hii ipatikane nchi nzima mpaka vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba utupaji wa watoto kwa kiasi kikubwa pia unachangiwa na mimba zisizotarajiwa au wanawake ambao wanazaa nje ya ndoa. Kwa hiyo, kubwa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni suala la kuelimisha jamii juu ya suala la uzazi wa mpango, na wenzetu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi kubwa katika kuelimisha jamii juu ya uzazi wa mpango.

Pia nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 imetoa adhabu kali kwa wanawake ambao wanakutwa na kesi za kutupa watoto. Adhabu ni faini isiyozidi Shilingi milioni tano au kwenda jela kwa muda wa miezi sita. Kwa hiyo, sheria iko makini. Nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge watusaidie katika kutoa taarifa wanapoona watoto wametupwa.

Nakubaliana na swali la pili kwamba elimu ni lazima ifike vijijini. Ni kweli tuna Maofisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata. Kwa hiyo, tutapokea ushauri wa kuhakikisha kwamba na wenyewe pia wanatoa mchango katika kuelimisha jamii juu ya masuala ya kutupa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Lakini kama mtakavyoona, kwa kweli leo tumekwenda kweli kweli kwa sababu maswali ni mengi. Ni maswali 12, mengi ni marefu na baadhi ya maswali majibu yake vilevile ni marefu. Mtaona karibu nusu ya maswali hatukuwa na maswali ya nyongeza, lakini bado tumekwenda nusu saa zaidi ya muda wa kawaida. Kwa hiyo, tuvumiliane.

Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto alikuwa ananikumbusha kwamba leo ni siku ya masuala ya ukeketaji. Waliwahi kuja ujumbe wa akina mama Jimboni kwangu. Sisi tuna mila hiyo na walitoka mbali kwa mguu wakawa wananishawishi; kama Mheshimiwa Mbunge, kwa nini usiende kuwaelimisha Wabunge wakaelewa umuhimu wa ukeketaji? Mnaweza mkajua ugumu nilioupata wa kuwajibu, lakini nashukuru Serikali inashughulikia.

Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na wageni tulionao Bungeni. Kwanza tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni ndugu Esaka Mugasa, Kamishna Msaidizi wa Polisi, karibu sana. Ndugu Justus Mulokozi - Mwanasheria, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Zaituni Sasha - huyu anatoka Azimio na ndugu yetu Gatrude Ndibalema ni Mdau wa Azimio.

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Dodoma. Wanafunzi wa CBE, karibuni sana, ninyi ni majirani zetu. Karibuni sana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Wanafunzi 50 kutoka Shule ya *Independence School* Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi kutoka Dar es Salaam na mtapata Maofisa wa Bunge baadaye kidogo kuwaelezea zaidi kuhusu Bunge na kama mna maswali mtayauliza huko. (*Makofi*)

Wageni wawili kutoka *Rex Solar Energy Contractors* Dar es Salaam ambao ni Ndugu Francis Kibhisa - Mkurugenzi Mkuu na Ndugu Francis Jones - Mkurugenzi Mwendeshaji. Wamekuja kuonesha umuhimu wa vifaa vya *solar energy*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni wa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe - Kiongozi wa Upinzani Bungeni kutoka *Lyamungo Corporative* ambao ni ndugu Gabriel Ulomi. Ahsante sana. Ndugu Elinaike I. Lema, ahsante; Ndugu Zamdoc Ntenga na Ndugu Charles Malya. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mary Michael Nagu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji na Uwekezaji) ni ndugu Yona Moses kutoka Gairo, karibu sana; Ndugu Lucas Hando, Ndugu Samweli Eli na Ndugu Sideti Muhindi, Mwenyekiti wa CCM Lehandu, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, ni ndugu Michael Andrea Lekule - Mwenyekiti wa *TLP* Kilaracha. Ahsante sana Mwenyekiti. Kule kijijini kwa Mheshimiwa Mrema kuna kijiji maarufu cha Kilaracha.

Mgeni wa Mheshimiwa Susan Lyimo ni ndugu Elias Nyagabona kutoka Tarime, yeye ni Mjumbe wa Mkutano

Mkuu wa Taifa wa CHADEMA. Karibu sana popote pale ulipo.

Mgeni wa Mheshimiwa Bernadetha Mushashu ni ndugu Tryphone Paulo Nyerere, ni mkulima kutoka Karaawe Kagera. Karibu sana Ndugu Paulo. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Suzan Kiwanga na Mheshimiwa Cecilia Paresso, ni Mheshimiwa Lucas Mwakambaya, Diwani Kata ya Mtibwa Morogoro. Karibu sana Mheshimiwa Diwani kutoka Mtibwa.

Wageni wa Mheshimiwa Luhaga Mpina, ni wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara CBE Dodoma. Natumaini nilikwishawatambulisha.

Wageni wa Mheshimiwa Waride Bakari Jabu ni vijana 17 wa Timu ya Mpira wa Mbweni Kiembesamaki Zanzibar wakiongozwa na Ndugu Ibrahim Mbaraka Ramadhani. Karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wako wageni wangu ambao ni kutoka Shule ya Sekondari ya *Saint John* Kilimatinde Manyoni Singida pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni ambao ni Mwalimu Mariam Katala. Mwalimu Katala karibu sana; Mwalimu Samweli Sefu karibu sana; Mwalimu Paul Modest, karibu na Mwalimu Jemrua Cheleo, karibu sana. Lakini vilevile wamefuatana na wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya *Saint John* Kilimatinde. Karibuni sana wanafunzi kutoka *Saint John*, hii ni moja ya sekondari inayofanya vizuri sana kutoka katika Mkoa wa Singida katika eneo la Kilimatinde kule Manyoni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo ya kazi. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Mheshimiwa Andrew Chenge - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane katika ukumbi wa Pius Msekwa saa 5.00 asubuhi baada ya matangazo haya.

Mheshimiwa Joseph Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi hii ukumbi wa Msekwa (B).

Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kukutana kuanzia saa 5.00 katika ukumbi Na. 219 Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa *TWPG* anawaomba Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kwamba leo Jumatano kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wanawake kwa ajili ya kutoa mrejesho kuhusu maoni ya *TWPG* kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Mbona mmechelewa ninyi? Kikao hicho kitafanyika mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge leo asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa David Mwakyusa, Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji

wakutane saa 7.00 mchana. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi ulioko hoteli ya *Fifty Six* saa 7.00 mchana.

Mwisho, Waheshimiwa Wabunge asubuhi ya leo mtakumbuka wakati natoa maelekezo ya ufafanuzi kuhusu uwasilishaji wa nakala ya mitaala ya kufundishia iliyowekwa Mezani na Mheshimiwa Waziri wa Elimu niliwataja Wajumbe wa timu itakayotusaidia kwenda kuangalia jambo hili Mheshimiwa Margareth Sitta bado hajafika, lakini yuko njiani anakuja.

Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Bernadetha Mushashu ataanza shughuli hiyo na Wajumbe wengine kama nilivyowataja Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ambao ndiyo Wajumbe wa hiyo timu ningeomba sasa wawe tayari kuondoka na kwa upande wa Serikali kadri watakavyoona inafaa. Lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Kamishna wa Elimu, Mwanasheria wa Wizara na hao Maafisa wengine ambao mnaona ni muhimu kwa jambo hili nao wakawepo huko. Ukumbi ambao utatumiwa nilisema ni *basement* lakini sasa nawaomba mwende ukumbi wa Mikutano wa Mheshimiwa Spika, Jengo la Utawala.

Kwa hiyo, vitabu vile vilivyowekwa hapa ni Mtaala wa Elimu ya Msingi, Elimu ya Awali na Mtaala wa Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Mushashu, nakuomba kama upo uteremke sasa hivi uje akukabidhi. Nakuomba karibu sana.

(Hapa Mheshimiwa Mushashu alikwenda mbele ili kuvipokea vitabu vya Mitaala)

NAIBU SPIKA: Kama nilivyoeleza, Mheshimiwa James Mbatia anaomba vilevile kutoa ushirikiano katika zoezi hilo. Wajumbe wa Kamati mkimaliza kazi hiyo leo, ni vyema; lakini mwisho si zaidi ya kesho, lazima muwe mmetupatia mrejesho kwa Ofisi ya Spika ili Bunge liweze kufahamu kinachoendelea.

KAULI ZA MAWAZIRI

Kauli kuhusu Taarifa ya Mbunge wa Ukerewe - Mheshimiwa Salvatory Machemli, Mbunge wa CHADEMA, kwamba askari kutoka Kenya na Uganda wamevuka mpaka wa Tanzania na kuingia katika Kisiwa cha Ukerewe kuwapiga na kuwanyanyasa wananchi

NAIBU SPIKA: Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kutoa kauli yake, naomba nimwite Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kuendelea na shughuli zilizo hapa.

(Hapa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu alikalia Kiti)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Spika aliyoyatoa tarehe 5 Februari, 2013 kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu taarifa ya Mbunge wa Ukerewe - Mheshimiwa Salvatory Machemli,

Mbunge wa CHADEMA, kwamba askari kutoka Kenya na Uganda wamevuka mpaka wa Tanzania na kuingia katika Kisiwa cha Ukerewe kuwapiga na kuwanyanyasa wananchi. Naomba kutoa kauli ya Serikali kuhusu taarifa hiyo kwa mujibu wa kanuni Na. 49 ya kanuni za Bunge toleo la mwaka 2007 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Kenya, Tanzania na Uganda ambazo zinapakana katika Ziwa Victoria zimekubaliana kufanya operesheni za pamoja za kukomesha uchafuzi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kupambana na uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi wanaotumia nyavu zenye matundu madogo maarufu kama kokoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano hayo yanafanyika chini ya Taasisi ijulikanayo kama *Lake Victoria Fisheries Organisation*. Hivi sasa wanachama wa Taasisi hii wanaendesha oparesheni ya pamoja Mkoani Mwanza iliyotanguliwa na mafunzo ya nadharia kuanzia tarehe 21 – 30 Januari, 2013. Operesheni hii inawashirikisha Maafisa mbalimbali wa uvuvi kutoka nchi za Kenya, Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya suala hili ni kwamba mnamo tarehe 31 Januari mwaka huu, Maafisa wa Uvuvi wa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda waliandaa operesheni maalum ikiwa ni sehemu ya mafunzo ya vitendo katika maeneo ya Wilaya ya Ukerewe iliyokadiriwa kufanyika kwa muda wa siku saba. Operesheni hii ilikuwa na lengo la kuwakamata wavuvi wanaotumia nyavu zenye matundu madogo. Maafisa hawa waliwashirikisha askari wa Jeshi la Polisi wa Tanzania kwa

sababu operesheni hii isingeweza kufanyika kirahisi bila ya ulinzi wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa operesheni za namna hii zinachukiwa sana na wavuvi waramu, mnamo tarehe 4 Februari, 2013 kulijitokeza kikundi cha watu katika Kijiji cha Buzegwa waliotaka kuzuia operesheni hiyo isifanyike. Askari wa Jeshi la Polisi walilazimika kutumia mabomu ya kutoa machozi kwa lengo la kuwatanya watu hao na kwa bahati nzuri operesheni hiyo iliendelea vizuri bila madhara yoyote kwa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo niliyoyatoa hapo awali, siyo kweli kwamba kuna askari kutoka nchi jirani walioingia nchini na kuwanyanyasa wananchi kama Mheshimiwa Mbunge alivyoliambia Bunge lako Tukufu. Ukweli ni kwamba, operesheni inayoendelea katika Wilaya ya Ukerewe ni sehemu ya mafunzo maalum ya vitendo ambayo yanafanyika kihalali. Serikali ya Wilaya ya Ukerewe imeridhia operesheni hiyo yenye manufaa kwa nchi hizi tatu, yaani Kenya, Tanzania na Uganda. Hali kadhalika Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa David Mathayo naye anaifahamu operesheni hii na ameiridhia. Vilevile Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza wanazo taarifa za kufanyika kwa operesheni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kutangaza humu Bungeni taarifa ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kutosha ni jambo la hatari sana. Taarifa za namna hii zinaweza kusababisha uhusiano mbaya kati ya Tanzania, nchi ambayo tunaipenda sana na nchi jirani lakini, pia kunaweza kumtia aibu Mheshimiwa

Mbunge mwenyewe kwa kutangaza habari zinazoupotosha umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sifa kuu ya utukufu wa mwanadamu ni kuwa na akili inayomwezesha binadamu kufikiri, kufanya uchambuzi na kutathmini mambo mbalimbali kabla ya kuyasema. Binadamu ambaye haitumii akili yake ipasavyo, kutafiti na kutafakari mambo, anapoteza sifa ya kuaminiwa na wanadamu wenziwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Mao Tse Tung aliwahi kusema maneno yafuatayo na naomba kunukuu: “Iwapo hujalifanyia utafiti jambo unalotaka kulizungumza, basi usilizungumze jambo hilo kabisa.” Kwa msingi huo, siyo busara hata kidogo Waheshimiwa Wabunge, viongozi ambao wanaaminiwa sana na wapigakura na wananchi kwa ujumla kusema ndani ya Bunge mambo ambayo hawajayafanyia utafiti wa kutosha. Tukifanya hivyo tutaipoteza heshima yetu mbele ya umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania linazielewa vyema taarifa za kuendeshwa kwa operesheni ya pamoja ya kukamata wavuvi wanaotumia nyavu haramu hata kabla zoezi hili halijaelezwwa hapa Bungeni. Jeshi letu lipo imara wakati wote kuhakikisha kwamba hakuna askari yeyote kutoka nje ya nchi atakayevuka mipaka ya nchi yetu na kuwanyanyasa au kuwapiga raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mwongozo!

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) na Kanuni 49(2). Napenda kulithibitisha Bunge lako Tukufu kwamba kauli za Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwanza ni za kudhalilisha kwa kuniita Mbunge kwamba sina akili wakati wapiga kura wangu ambao leo nasimama hapa katika Bunge lako Tukufu kuwatetea baada ya kuwa wamedhalilishwa kwa vitendo nilivyovisema humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushahidi wa kutosha kabisa kwa kauli nilizozitoa hapa katika Bunge lako Tukufu. Ninao majeruhi wengi wasiopungua 20 ambao wamepigwa na baadhi yao wamevunjwa miguu na viungo vingine. Majeruhi hawa wametishiwa kwamba kwa kuwa walikuwa wanaendesha uvuvi haramu, sasa wasiende kushtaki na hata wakienda Polisi hawapewi PF3 kwa ajili ya kwenda kutibiwa. Kwa hiyo, wapo nyumbani wanaugulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba niwataje baadhi ya majeruhi ambao nina uhakika nao. Kata iliyotajwa katika kijiji kilichotajwa naomba nirekebishwe; Kijiji kilichotajwa na Mheshimiwa Waziri, Kijiji cha Buzegwe wala hakina majeruhi hata mmoja. Pale walirusha bomu. Majeruhi wanatoka katika Kata ya Ngoma Kijiji cha Debuye na ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza ni Atlas Yasin, amevunjika mguu wa kulia; wa pili ni Ali Manywele, amevunjika mguu; watatu ni Rwigy Kayala, amevunjika mguu; huyu amepigwa mgongo na hawezi kusimama anaitwa Ikwala Kanyangwa; yupo Ndalahwa; yupo Samson Mussa na Amos ambaye ni dereva wa boda boda. Huyu alikutwa akiwa amembeba abiria akiwa na samaki mmoja kama kitoweo, akapigwa akatozwa Sh. 100,000/= na yule aliyekuwa na samaki wa kitoweo akatozwa Sh. 100,000/=. Mwingine ni mama mjamzito anaitwa Pendo Tungaraza, huyu ni wa kijiji cha Sambu. Alipigwa akiwa na ujauzito na ana hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli za Waziri wa Ulinzi siyo sahihi, pamoja na kunidhalilisha mimi Mbunge ninayewakilisha watu waliojeruhiwa. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba taarifa niliyotoa hapa ni sahihi na naendelea kuisimamia kwamba maaskari kutoka nchi ya Kenya na Uganda wako Ukerewe na wanaendesha operesheni ambayo inavunja haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kwa kuwa kauli ya Waziri siyo sahihi na inaleta utata, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili kauli hii kwa sababu waliojeruhiwa ni wananchi wa Ukerewe na ni wananchi wa Tanzania na wamepigwa na askari kutoka nje kwa taarifa walizozitoa. Kauli kama hii ya Waziri iliwahi kuleta utata katika pesa za Rada na likajadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili kauli hii ijadiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge ameomba Mwongozo wa Kiti. Kiti kimepokea maelezo yake na Kiti kitatoa Mwongozo baadaye. Tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

**Azimio la Bunge la Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa
wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia
(*International Convention for the Suppression
of Acts of Nuclear Terrorism, 2009*)**

**Azimio la Bunge la Kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na
Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya
Kimataifa Pamoja na Wakala wa Diplomasia
(*Convention on the Prevention and Punishment
of Crimes Against Internationally Protected
Persons, Including Diplomatic Agents 1973*)**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, una Maazimio mawili na una muda wa dakika 30 tu. Jipange uyasome yote kwa muda unaoruhusiwa kikanuni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kuwasilisha Bungeni Azimio la Pendekezo la Kuridhia na Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Nyuklia.

(International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism, 2005)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio lililopo mbele yetu linahusu mapendekezo ya Tanzania kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya ugaidi na matumizi ya nyuklia vina madhara makubwa kwa binadamu, mali na mazingira kwa ujumla. Mashambulio ya kigaidi yametokea katika nchi nyingi ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo mwaka 1998 na vimeendelea kuwepo na kuongezeka. Matukio kama haya yameifanyia Jumuiya ya Kimataifa kubaini kuwepo kwa hatari kubwa ya vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia madhara ya ugaidi, nchi mbalimbali duniani, zikiongozwa na Mikataba ya Umoja wa Mataifa dhidi ya vitendo vya ugaidi zimechukua hatua mbalimbali za kupambana na ugaidi. Kati ya hatua hizo ni pamoja na kutungwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia *(International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism, 2005)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba mingine ya Kimataifa dhidi ya ugaidi ni:-

- Mkataba wa Makosa na Vitendo vya uhalifu vinavyotendeka katika Ndege *(Convention of Offences and Certain Acts Committed on Board Aircraft) (1963);*

- Mkataba kuhusu Udhhibiti wa Utekaji Nyara Ndege (*Convention for the Suppression of Unlawful Seizure of Aircraft*) (1970);

- Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Utekaji Nyara (*United Seizure of Aircraft Against the Taking of Hostages*) (1979);

- Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Vitendo vya Uhalifu kuhusu Usalama wa Anga (*Convention for the Suppression of Unlawful Acts Against the Safety of Civil Aviation*) (1971);

- Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Vitendo vya Uhalifu kuhusu Usalama wa Usafiri wa Majini (*Convention for the Suppression of Unlawful Acts Against the Safety of Maritime Navigation*) (1988);

- Mkataba wa Kimataifa wa Uwekaji Alama Kwenye Milipuko ya Plastiki kwa lengo la Utambuzi (*Convention on the Marking of Plastic Explosives for the Purpose of Detection*) (1991);

- Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Ufadhili wa Ugaidi (*United Nations Conventions for Suppression of Financing of Terrorism*) (1999);

- Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia Ugaidi wa Kutumia Mabomu (*United Nations Convention for the Suppression of Terrorism Bombing*) (1997).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu una lengo la kudhibiti vitendo vya ugaidi wa kutumia nyuklia na unatambua haki ya kila Taifa ya kuendelea na kutumia nishati ya nyuklia kwa manufaa ya nchi husika na siyo kwa

matumizi yanayohatarisha amani na usalama duniani. Ili kukabiliana na ugaidi na madhara yake, Bunge hili lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi Na. 21 ya mwaka 2002 kwa lengo la kuweka mfumo wa udhibiti dhidi ya vitendo vya ugaidi na kuongeza ushirikiano na nchi nyingine katika mapambano dhidi ya vitendo vya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa matumizi mabaya ya nyuklia yanaweza kuleta madhara kwa binadamu, mali na mazingira, Bunge hili pia lilitunga Sheria ya Nguvu za Atomiki Na. 7 ya mwaka 2002 kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya mionzi ya nyuklia na kuendeleza matumizi salama ya mionzi hiyo.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana na Mataifa mengine katika kupambana na vitendo vya ugaidi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejiunga na kuridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa dhidi ya vitendo vya ugaidi kama nilivyoitaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mikataba hii haikujumuisha vitendo vya ugaidi wa kutumia nyuklia, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimeshindwa kushirikiana katika kukabiliana na ugaidi wa kutumia nyuklia. Kwa kutambua upungufu huo, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ziliamua kuunda Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia wa mwaka 2005. Mpaka sasa jumla ya nchi 141 ama zimetia saini, zimeridhia, zimejiunga au kuthibitisha Mkataba huu kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa nchi jirani zilizokwisharidhia Mkataba huu ni pamoja na Kenya, Malawi, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Mkataba huu tayari una nguvu ya kisheria kuanzia tarehe 7 Julai, 2007 baada ya kutimizwa kwa sharti lililowekwa na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kuridhia Mkataba huu linatokana na kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo madini ya *uranium* (urani) yamegunduliwa. Ingawa kuwepo kwa madini haya nchini kutasaidia kuinua maendeleo ya uchumi wa nchi. Vilevile kuwepo kwa madini hayo kunaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi ambazo zinaweza kulengwa na magaidi katika kuyapata na kuyatumia madini hayo katika vitendo vya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu umekusudiwa kubainisha vitendo vya matumizi ya nyuklia au vifaa vya nyuklia ambavyo ni makosa ya jinai. Masuala haya hayakushughulikiwa ipasavyo katika Mikataba ya Kudhibiti ugaidi iliyotajwa hapo juu. Hivyo, Mkataba huu unaongeza nguvu na jitihada katika vita dhidi ya ugaidi sambamba na Mikataba ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania imeridhia mkakati wa Kimataifa wa Kupambana na Ugaidi (*Global Counter Terrorism Strategy*), kujiunga na Mkataba huu kutapanua wigo wa kupambana na vitendo vya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vipengele muhimu katika Mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

- Aina ya makosa yanayozingatiwa na Mkataba;

- Mazingira ya kutumika kwa Mkataba;
- Utaratibu wa kushughulikia makosa yaliyotajwa katika Mkataba huu;
- Ushirikiano wa Mataifa wanachama katika kuzuia ugaidi wa nyuklia;
- Utaratibu wa kurejesheana watuhumiwa wa uhalifu;
- Namna ya kutatua migogoro inayohusiana na tafsiri au matumizi ya Mkataba huu; na
- Utaratibu wa kujiunga na kuanza kutumika kwa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepitia vipengele vyote vya Mkataba huu na kujiridhisha kuwa vinakubalika na havikinzani na maslahi ya Taifa isipokuwa katika eneo la ibara ya 23 (1). Ibara hii inahusu kutumika kwa Mahakama ya Kimataifa ya Haki (*International Court of Justice*) katika utatuzi wa migogoro baina ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inakusudia kujiunga na Mkataba huu kwa shaka (*Reservation*) ili kutoa nafasi kutumia njia za majadiliano na usuluhishi katika kutatua migogoro itakayojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba huu badala ya kupeleka migogoro baina ya Tanzania na nchi nyingine katika Mahakama ya Kimataifa ya haki bila ridhaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya matokeo yanayotarajiwa kutokana na kujiunga na Mkataba huo ni pamoja na:-

- Kupanua wigo wa Kisheria katika kuzuia ugaidi wa kutumia nyuklia;
- Kuimarisha ushirikiano katika kubadilishana uzoefu na taarifa za uhalifu wa ugaidi;
- Tanzania kudhihirisha utashi wa kisiasa katika kulinda usalama wa ndani na nje ya mipaka yake;
- Kuwa na haki ya Kisheria ya kumkamata na kumshitaki mtu yeyote anayejaribu kufanya au kutishia kufanya ugaidi wa kutumia nyuklia; na
- Tanzania inaweza kupambana na ugaidi wa kutumia nyuklia kwa pamoja na nchi nyingine wanachama hususan nchi jirani za Kenya, *DRC* na Burundi ambazo tayari zimejiunga na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa naomba kutoa hoja ya kuwa Bunge lako lijadili na kuridhia Azimio la kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa kutumia nyuklia. (*International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism, 2005*).

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa kutumia nyuklia wa mwaka 2005;

NA KWA KUWA, Mkataba huu una lengo la kudhibiti vitendo vya ugaidi wa kutumia nyuklia pamoja na kutambua haki ya kila Taifa kuendeleza na kutumia nishati ya nyuklia kwa manufaa ya nchi husika na si kwa matumizi yanayohatarisha amani na usalama duniani;

NA KWA KUWA, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa pamoja na kuchukuwa hatua mbalimbali za kupambana na ugaidi ikiwa ni pamoja na utungaji wa Sheria za kuzuia vitendo vya ugaidi wa kutumia nyuklia zimeshindwa kushirikiana katika kukabiliana na ugaidi wa kutumia nyuklia kutokana na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa dhidi ya vitendo vya ugaidi kutojumuisha vitendo vya ugaidi wa kutumia nyuklia;

NA KWA KUWA, hadi hivi sasa idadi ya nchi zilizokwisharidhia, kusaini, kujiunga au kuthibitisha Mkataba huu ni 142 zikiwemo nchi jirani za Kenya, Malawi, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

NA KWA KUWA, kuridhia kwa Mkataba huu kutaiwezesha Tanzania kushirikiana na nchi nyingine wanachama ambazo tayari zimesharidhia Mkataba huu wa kupambana na ugaidi unaotokana na matumizi ya nyuklia;

NA KWA KUWA, msimamo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwa haitafungwa na masharti ya Ibara ya 23 aya (1) ya Mkataba huu inayoweka masharti kuwa migogoro baina ya nchi wanachama kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba huu itatatuliwa kwa njia ya majadiliano na usuluhishi na kama zitashindwa kuafikiana, nchi mojawapo itaupeleka mgogoro husika katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu kwa Tanzania na kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sasa linaazimia kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia (*International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism, 2005*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Azimio la pili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Bungeni Azimio la Mapendekezo ya Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa kidiplomasia (*Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, including Diplomatic Agents, 1973*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio lililopo mbele yetu linahusu mapendekezo ya kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia. Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa una majukumu ya kudumisha amani na usalama, kuhamasisha

ujirani mwema pamoja na kuimarisha urafiki na ushirikiano baina ya Mataifa wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu hayo, mwaka 1973 Umoja wa Mataifa uliunda Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia. Mkataba huu unakusudia kuzuia na kuadhibu makosa dhidi ya watu wenye kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia kwa madhumuni ya kuimarisha usalama wao na kuboresha ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mkataba huu, ipo Mikataba mingine ya Umoja wa Mataifa inayotoa masharti ya jumla juu ya Kinga na Usalama wa Wanadiplomasia. Mikataba hiyo ni Mkataba wa Vienna wa Mahusiano ya Kidiplomasia (*Vienna Convention on Diplomatic Relations*) (1961) na Mkataba wa Vienna wa Mahusiano ya Kibalozi (*Vienna Convention on Consular Relations*) (1963) ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeiridhia.

Hata hivyo, Mikataba hiyo haijaweka masharti maalum ya kuyatambua na namna ya kuyaadhibu makosa dhidi ya watu wenye kinga ya Kimataifa na wanadiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 27 Machi, 2012 Mkataba huu ulikuwa na nchi wanachama 173. Nchi za Afrika ambazo ni mwanachama wa Mkataba huu ni 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ni wanachama wa Mkataba huu. Mkataba huu tayari una nguvu ya Kisheria kuanzia tarehe 20 Februari, 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusudio ya Mkataba huu ni kuweka mfumo wa mashirikiano wa kuwalinda watu wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia dhidi ya vitendo vya uhalifu vinavyohatarisha usalama wao.

Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na mwenyeji wa jumuiya mbalimbali za Kimataifa. Nchi mbalimbali zina Balozi zake hapa nchini. Hali hii inasababisha Tanzania kupokea watu kutoka nchi za nje wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia ambapo Serikali ina wajibu wa kuwahakikishia usalama wao. Vile vile, Tanzania ina Balozi katika nchi mbalimbali na raia wake wanafanya kazi kwenye Mashirika ya Kimataifa na katika Balozi hizo. Hawa nao wanahitaji kulindwa dhidi ya vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi mbalimbali kumekuwepo na matukio ya uhalifu yakiwemo ya kigaidi yanayolenga kudhuru Balozi, Maafisa wa Ubalozi, Wakala wa Kidiplomasia na mali zao. Mwaka 1998 Tanzania ilikuwa mhanga wa tukio la kigaidi kwenye Ubalozi wa Marekani hapa nchini ambalo lilisababisha vifo na majeruhi kwa Watanzania na wafanyakazi wa Ubalozi. Tukio hili pia lilisababisha uharibifu wa mali ikiwemo kuungua kwa jengo la Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti uhalifu wa aina hii tunahitaji juhudi za pamoja baina ya Mataifa. Mkataba huu umekusudiwa kufanikisha jambo hili. Hivyo, kujiunga na Mkataba huu kutaiwezesha Tanzania kuwa na mfumo wa ushirikiano na nchi nyingine wanachama wa Mkataba huu katika kuwalinda watu wenye kinga ya Kimataifa na

Wakala wa Kidiplomasia waliopo nchini dhidi ya vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipengele muhimu vya Mkataba huu ni pamoja na:-

- Aina ya makosa ya jinai dhidi ya watu wanaolindwa katika Mkataba huu na adhabu zake pamoja na wajibu wa nchi wanachama kuharamisha makosa hayo;
- Ushirikiano wa Mataifa wanachama katika kuzuia uhalifu;
- Utaratibu wa kushughulikia makosa yaliyotajwa katika Mkataba huu;
- Namna ya kutatua migogoro inayohusiana na tafsiri au matumizi ya Mkataba huu;
- Utaratibu wa kujiunga na kuanza kutumika kwa Mkataba huu; na
- Utaratibu wa namna ya kujiondoa katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matokeo yanayotarajiwa kutokana na kujiunga na Mkataba huu ni pamoja na:-

- Kuwa na mwongozo maalum wa hatua zifaazo katika kuzuia na kuadhibu uhalifu dhidi ya watu wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia;

- Kupanua wigo wa Kisheria katika kuzuia na kuadhibu uhalifu dhidi ya watu wenye kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia;
- Kupanua wigo wa ushirikiano baina ya Tanzania na Mataifa mengine wanachama katika kuzuia na kuadhibu uhalifu dhidi ya watu wenye kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia;
- Tanzania kudhihirisha utashi wa kisiasa katika kulinda usalama wa watu wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia; na
- Kuimarisha na kudumisha mahusiano ya Kimataifa baina ya Tanzania na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza hapo mwanzo, Mkataba huu uliundwa mwaka 1973 tangu muda huo. Tanzania haikuwahi kutia saini au kujiunga. Mkataba huu unaihusu Tanzania kwa kuwa ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa, ni mwanachama katika Mikataba mingine dhidi ya uhalifu wa Kimataifa kama vile ugaidi na pia inao watu wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa kidiplomasia wanaohitaji kulindwa chini ya Mkataba huu. Hivyo basi, Mkataba huu unaletwa mbele ya Bunge lako Tukufu chini ya masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ili Tanzania iweze kujiunga rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepitia vipengele vyote vya Mkataba huu na kujiridhisha kuwa havikinzani na maslahi ya Taifa isipokuwa Ibara ya 13(1). Ibara hii inahusu kutumika kwa Mahakama ya Kimataifa ya Haki

(*International Court of Justice*) katika utatuzi wa migogoro baina ya nchi wanachama. Tanzania inakusudia kujiunga na Mkataba huu kwa shaka ili kutoa nafasi kutumia njia za majadiliano na usuluhishi katika kutatua migogoro itakayojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba huu badala ya kupeleka migogoro baina ya Tanzania na nchi nyingine katika Mahakama ya Kimataifa ya haki bila ridhaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja ya kuwa Bunge lako lijadili na kuridhia Azimio la kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia (*Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, including Diplomatic Agents, 1973*). (Makofi)

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa na imekuwa ikichangia michango mbalimbali ya Uanachama, ikiwa ni pamoja na michango ya Mabaraza ya Ulinzi na Usalama ya Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA, Umoja wa Mataifa una majukumu ya kudumisha amani na usalama, kuhamasisha ujirani mwema pamoja na kuimarisha urafiki na ushirikiano baina ya Mataifa wanachama;

NA KWA KUWA, katika kutekeleza majukumu hayo, mwaka 1973 Umoja wa Mataifa ulitunga Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa

Kidiplomasia, kwa madhumuni ya kuimarisha usalama wao na kuboresha ushirikiano wa Kimataifa;

NA KWA KUWA, Tanzania ni mwanachama na mwenyeji wa jumuiya anuai za Kimataifa, ambapo nchi nyingi mbalimbali zimefungua Balozi zake hapa nchini na hivyo kusababisha Tanzania kupokea watu wenye kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia ambapo Serikali inawajibika kuwalinda; Aidha, Tanzania ina raia wake wenye kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia wanaofanya kazi nchi za nje ambao nao wanahitaji ulinzi dhidi ya vitendo vya uhalifu;

NA KWA KUWA, kuridhia Mkataba huu kutaiwezesha Tanzania kuwa na mfumo wa ushirikiano na nchi nyingine wanachama wa Mkataba huu katika kuwalinda watu wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia waliopo nchini dhidi ya vitendo vya uhalifu na pia kuwezesha raia wa Tanzania wenye kinga ya Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia waliopo katika Mataifa mengine nao pia kupewa ulinzi dhidi ya vitendo vya uhalifu;

NA KWA KUWA, kwa kuridhia Mkataba huu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitafungwa na masharti ya Ibara ya 13(1) ya Mkataba huu inayoweka masharti kuwa migogoro baina ya nchi wanachama kuhusu tafsiri au matumizi ya Mkataba huu itatatuliwa kwa njia ya majadiliano na usuluhishi na kama nchi wanachama zitashindwa kuafikiana, nchi mojawapo inaweza kupeleka mgogoro huo katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (*International Court of Justice*).

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu kwa Tanzania na kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sasa linaazimia kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia, yaani *“Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, including Diplomatic agents, 1973”*.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mwenyekiti au Msemaji wa Kamati.

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwashukuru Viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi Taifa katika kuiteua katika kugombea nafasi Kuu ya CCM NEC mwaka 2012. Nawashukuru Viongozi wangu wa UWT Taifa na Mkoani Kilimanjaro kwa kupitisha jina langu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, samahani mna maoni mawili na muda wenu ni nusu saa. Sasa ukianza kushukuru sana...!

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Nawashukuru pia Wajumbe wote

wa Mkutano Mkuu wa UWT Taifa wakiongozwa na Wajumbe kutoka Mkoa wa Kilimanjaro kwa kunichagua kuwa Mjumbe wa NEC. Nasema ahsanteni sana, na heri ya Mwaka Mpya na Mwenyezi Mungu awajaze Baraka tele mwaka huu na miaka ijayo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia vitendo vya Ugaidi kwa kutumia nyuklia, (*International Convention for Suppression of Acts of nuclear Terrorism*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa fasili ya 4(a) ya Kifungu cha (8) ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya kifungu cha (9), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilishughulikia Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa na Bunge ulio chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika kutekeleza Jukumu hilo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 114(9) kuhusu kuwaalika wadau. Kamati iliwaalika wataalamu kutoka Asasi za Serikali, Asasi za kiraia (AZISE) na wadau wengine kwa ajili ya kupata maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 23 Januari, 2013 Kamati ilikutana Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam kwa ajili ya kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Mkataba huu.

Aidha, siku hiyo Kamati ilialika wadau wafike kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo haya ya Serikali. Utaratibu huu wa kuwaalika wadau kutoa maoni yao kuhusu

mapendekezo ya Serikali mbali na Miswada ya Sheria, ni wa msingi na muhimu kwa Jamii ya Kidemokrasia kama Tanzania. Ni utaratibu unaolisaidia Bunge kuendelea kuwa chombo halisi cha wananchi kinachojikita kukidhi matarajio yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha kwanza kwa ajili ya kusikiliza maoni, wadau waliomba kuongezewa muda ili nao wapate muda wa kutosha kutafakari na kutoa maoni yenye tija na yatakayolisaidia Bunge katika kujadili mapendekezo haya. Kamati iliafiki ombi hilo na kukubaliana na wadau kukutana tena tarehe 01 Februari, 2013 katika Ofisi ya Bunge Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e), Kamati ilitumia njia mbalimbali za kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo Mezani leo. Njia hizo ni pamoja na kuangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, baadhi ya Sheria za Bunge zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa, uzoefu wa nchi nyingine katika masuala muhimu ya Mkataba huu pamoja na kutafakari kuhusu hasara au faida na kiwango cha manufaa au madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia au kutokuridhia Mkataba huu kama ulivyo au kwa kuahirisha baadhi ya vifungu vya Mkataba (*Ratifying with reservation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwenye kikao cha tarehe 23 Januari na tarehe 01 Februari, 2013, Kamati ilichambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele yake. Aidha, Kamati ilipitia tovuti ya Umoja wa Mataifa ili

kujiridhisha kuhusu Mataifa yaliyosaini mwanzoni (*signatories*), yaliyojiunga baadaye (*accession*) na yaliyoridhia Mkataba huu (*ratification*). Mantiki ya kufanya hivyo ni pamoja na kutafakari uzoefu wa wenzetu kuhusu ibara mbalimbali za Mkataba huu.

Aidha, uelewa wa sababu zinazotolewa kwa baadhi ya nchi kuridhia kwa kuahirisha uridhiaji wa ibara moja au zaidi unaweza kusaidia nchi inayoridhia baadaye kupima na kutathmini sababu hiyo kwa upande wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko na asili ya wazo la Mkataba huu ni miongoni mwa mambo muhimu yanayosaidia kufanya uamuzi wa kuridhia. Historia ya Mkataba huu imeoneshwa katika tovuti ya Umoja wa Mataifa ambapo inaelezwa kuwa Kamati iliyoanzishwa kwa Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa Na. 51/210 la tarehe 17 Desemba, 1996 inahusika na asili ya Mkataba huu. Jambo linalojitokeza ni wasiwasi kuhusu silaha na zana za kinyuklia kuwepo katika mikono ya magaidi.

Wasiwasi huo umeendelea kuishughulisha Jamii ya Kimataifa kiasi cha kutafuta makubaliano ya pamoja katika kukabiliana na hatari iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mikataba ya Kimataifa iliyokwepo awali haikuwa na wigo wa kutosha kukabiliana na hatari ya ugaidi wa kutumia nyuklia. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo kwenye tovuti ya Umoja wa Mataifa, hali hii pamoja na mambo mengine iliisukuma Kamati ya Baraza la Umoja wa Mataifa (*Ad Hoc Committee established by General Assembly*) kuandaa rasimu ya Mkataba wa Kimataifa uliopitishwa na Baraza la Umoja wa

Mataifa tarehe 13 Aprili, 2005 na kuanza kusainiwa tarehe 14 Septemba, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mtoa hoja, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu hali iliyofikiwa katika Makataba huu kwa kuangalia umoja wa Mataifa unavyoeleza kwenye Tovuti yake na kubaini kama ifuatavyo:-

(i) Mkataba huu ulipata nguvu ya kisheria tarehe 7 Julai, 2007 kwa mujibu wa Ibara ya 25 (1) inayotamka;

(ii) Mkataba ulisajiliwa tarehe 7 Julai, 2007 na kupewa Namba 44004;

(iii) Idadi ya nchi zilizosaini awali (*Signatories*) ni 115 ambapo nchi zinazohusika (*Parties*) ni 83 tu;

(iv) Kwa mujibu wa Ibara ya 24(3), Mkataba huu unaruhusu nchi nyingine yoyote ambayo haikuwemo awali kusaini Mkataba huu. Ibara hiyo inatamka: *“This convention shall be open to accession by any state. The instruments of accession shall be deposited with the Secretary-General of the United Nations.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kulinganisha na misimamo ya nchi hizi kwa mustakabali wa Jumuiya yetu na ushirikiano wetu, ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti rahisi umebaini kuwa taarifa za Umoja wa Mataifa kwenye tovuti yake zinaonyesha nchi tatu kati ya tano ambazo ni wanachama

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizosaini Mkataba huo. Nchi hizo ni:-

(i) Kenya iliyosaini mwanzoni, tarehe 15 Septemba, 2005 na kuridhia baadaye tarehe 13 Aprili, 2006;

(ii) Burundi iliyosaini tarehe 29 Machi, 2006 na kuridhia tarehe 24 Septemba, 2008; na

(iii) Rwanda iliyosaini tarehe 06 Machi, 2006 lakini haijaridhia kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kwenye Tovuti hadi tarehe 4 Februari, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Uganda na Tanzania hazioneshwi kwenye orodha ya nchi zilizosaini mwanzo (*signatories*) au zilizokubali kusaini baadaye (*accession*). Hata hivyo, kwa kuzingatia ruhusa ya kusaini baadaye inayotolewa chini ya Ibara ya 24(3), Kamati ilitaka kujua kama Tanzania ilisaini Mkataba huu baadaye.

Kinachojitokeza hapa ni kuwa Serikali ya Tanzania haijasaini Mkataba huu, bali inaomba ridhaa ya Bunge ili nchi ijiunge na Mkataba huu.

Kwa maana hiyo, hili ni Azimio la Bunge la Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia [*International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism*].”

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ugaidi na madhara yake linafahamika nchini Tanzania. Moja ya Matukio yanayokumbukwa nchini ni lile la tarehe 7 Agosti, 1998 ambapo Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania ulilipuliwa na

kusababisha vifo na majeraha, wengi wao wakiwa Waafrika. Aidha, uwepo wa madini ya *uranium* nchini ni jambo linalohitaji tahadhari ya Taifa kwa masuala ya Ugaidi wa kutumia Nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri, pamoja na faida zinazoweza kupatikana kwa kuridhia Mkataba huu ikilinganishwa na hasara kwa kutokuridhia, Kamati ilizingatia pamoja na mambo mengine, majadiliano yaliyojitokeza katika Mkutano Mkuu wa *Interpol* uliofanyika tarehe 5 Novemba, 2012 na kujiridhisha kuhusu Ibara za Mkataba husika moja baada ya nyingine. Aidha, Katiba na Sheria mbili zilizotungwa na Bunge lako Tukufu zilizorejewa. Sababu ya rejea hizo ni kuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja baina yake na baadhi ya Ibara za Mkataba huu. Sheria hizo ni:-

(i) Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002 (*The Prevention of Terrorism Act, 2002*);

(ii) Sheria ya Kubadilishana Wakosaji, Sura ya 368 iliyojadidiwa Mwaka 2002 (*The Extradition Act, Cap. 368, Revised Edition, 2002*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mambo yote niliyoyaeleza Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuhusu madhara ya vifungu vilivyotumika katika Mkataba. Ibara ya 2(1) na 2(2) inaeleza jambo linalohesabika kuwa kosa kwa mujibu wa Mkataba huu. Maneno yaliyotumika kueleza ni pamoja na:

“...any person commits an offence within the meaning of this convention if that person unlawful or internally;...”

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya neno *unlawfully* katika Ibara ya 1(1) na 1(2) (b) yanaacha utata kwa kutotolewa tafsiri ya nini hasa ni *unlawfully* kama inavyotumika katika Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Watanzania wanaofuatilia Mkutano huu, naomba kunukuu Ibara ya 26(1) inayoeleza:-

“A state party may propose an amendment to this convention. The Proposed Amendment shall be submitted to the depositary, who circulates it immediately to all states parties.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, athari ya Ibara ya (5) na (6) za Mkataba katika Sheria za Nchi. Ibara ya (5) na (6) ya Mkataba unaopendekezwa Kuridhiwa, zinatoa wajibu kwa nchi kuyahesabu makosa yote yalioanishwa chini ya Ibara ya (2) ya Mkataba kuwa makosa ya jinai. Ni maoni ya Kamati kuwa Sheria zetu kuhusu makosa hayo zinahitaji kurekebishwa. Marekebisho yafanywe kwa sheria zinazohusu makosa yenyewe (*Substantive Laws*) na zinazohusu utaratibu wa kushughulikia makosa hayo (*Procedural Laws*). Kamati inashauri kuwa mara baada ya Kuridhia Mkataba huu, Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002 (*The Prevention of terrorism Act, 2002*) ifanyiwe marekebisho ili kujumuisha makosa yote yaliyotajwa katika Mkataba huu. Aidha, Sheria nyingine za nchi zinazoguswa na Mkataba huu zitahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, hatari ya kuwaweka hatiani wasio na makosa. Ibara ya 7(2) ya Mkataba huu inazitaka Nchi Wanachama (*State Parties*) kuchukua hatua zinazofaa kwa mujibu wa Sheria za Mataifa hayo katika kulinda usiri (*confidentiality*) wa Taarifa zinazopokelewa kutoka nchi nyingine, kwa mujibu wa Mkataba huu. Kamati inatambua na kuthamini umuhimu wa usiri uliozingatiwa katika Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, usiri huu ukizidi na kuwa usiri wa moja kwa moja (*absolute confidentiality*) unaweza kutumika kuwatia hatiani raia wasio na hatia yoyote. Kamati inashauri kuwa baada ya kuridhia Mkataba huu, Serikali iangalie uwezekano wa kutumia Ibara ya 26 ya Mkataba ili kupendekeza mabadiliko kwenye Ibara ya 7(2). Ruhusa ya kupendekeza marekebisho inasomeka:-

“A state party may propose an amendment to this convention. The proposed amendment shall be submitted to the depositary, who circulates it immediately to all state parties.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kubadilishana Wakosaji (*Extradition of Offenders*). Ibara ya 13 ya Mkataba inahusu kubadilishana Wakosaji. Ibara hii inataka makosa yaliyotajwa katika Ibara ya (2) ya Mkataba kujumuishwa kwenye makosa yanayohusika na ubadilishanaji wa Wakosaji miongoni mwa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kubadilishana Wakosaji (*Extradition Treaty*).

Kamati inajiuliza kuhusu vigezo vya kuzingatiwa na nchi kabla ya kuingia Mkataba wa aina hiyo. Ni vema Serikali ikazingatia Sheria ya Kubadilishana Wakosaji, Sura ya 368,

iliyojadidiwa Mwaka 2002 (*The Extradition Act, Cap. 368 Revised Edition of 2002*) pamoja na mambo mengine kabla ya kuafiki Ibara hii ya 13 ya Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kusigana kwa Mkataba na Sheria ya Nchi. Kwa kuzingatia kuwa Uridhiaji wa Mkataba wa Kimataifa hufanyika pale inapoonekana tija, katika hatua hii nchi inayoridhia haipaswi kuacha mgongano baina ya Sheria zake na Vifungu vya Mkataba unaoridhiwa. Ibara ya 15 ya Mkataba huu inaonekana kusigana na Kifungu cha 17 cha Sheria ya Kubadilishana Wakosaji, Sura ya 368. Wakati Ibara hii inakataa makosa yaliyotajwa katika Ibara ya (2) ya Mkataba kutohesabiwa kuwa makosa ya Kisiasa (*Political Offence*) au makosa yanayohusiana na makosa ya kisiasa (*Offence connected with a political offence*) au makosa yanayohusiana na msukumo wa kisiasa (*Offence inspired by political motives*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 17 cha Sheria, Sura ya 368 ni tofauti na ufafanuzi unaotolewa katika Ibara ya 15 ya Mkataba. Kamati inashauri kuwa kwa Kuridhia Mkataba huu Kifungu cha 17 cha Sheria, Sura ya 368 kinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla, Mkataba huu ni mzuri katika kupambana na ugaidi. Ni mkataba unaozingatia kuhitajika kwa juhudi za Mataifa mengi, Tanzania ikiwemo. Hata hivyo, ni vizuri Bunge lako Tukufu likajulishwa yafuatayo:-

(1) Serikali inapendekeza Bunge liridhie Mkataba huu kwa kuahirisha Uridhiaji (*ratification with reservation*) wa Ibara ya 23(1) kwa hoja zilizotolewa. Suala la Msingi hapa ni

kuwa iwapo Bunge litaridhia kama inavyopendekezwa na Serikali, ikitokea kutoelewana baina ya nchi yetu na nchi nyingine Mwanachama wa Mkataba huu na kwamba majadiliano (*negotiation*) yatashindikana na usuluhishi (*arbitration*) hautafanikiwa kupata ufumbuzi wa shauri lililopo, ni njia ipi itaweza kutumika.

(2) Tangu Mkataba huu uanze kusainiwa kwa mara ya kwanza, imekaribia miaka saba sasa hivi ndipo Bunge linaletewa mapendekezo ya kutaka kuridhia kujiunga na Mkataba huu. Ni wazi kuwa yapo mambo yaliyosababisha pendekezo hili lisije kabla ya mwaka huu. Itakuwa ni vizuri iwapo Serikali itaeleza sababu zilizosababisha kutoleta mapendekezo hayo kabla ya sasa. Aidha, ni muhimu kufahamu kilichojitokeza kwa sasa na kusababisha mapendekezo haya kuwasilishwa leo na sio kabla.

(3) Kwa kuwa Serikali imeonesha kuwa ni muhimu kwa Tanzania Kuridhia Mkataba huu na kwa vile Uridhiaji huu utakuwa na maana iwapo Sheria zetu zitaendana na Mkataba unaoridhiwa, ni vizuri Serikali ikabainisha itachukua muda gani kuoanisha sheria zetu na wajibu unaochukuliwa na nchi kwa kujiunga na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa kutumia Nyuklia. Namshukuru pia Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Wataalam wa Wizara hiyo, kwa kutoa ufafanuzi uliohitajika wakati wa Vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niwashukuru Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Chuo cha Ulinzi wa Taifa na Chuo cha Diplomasia kwa ushirikiano walioipatia Kamati. Nikiri kuwa majadiliano yaliyojitokeza katika kikao cha Kamati kujadili Azimio hili, yalipata mchango mkubwa na mzuri kutokana na maoni ya Wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa mchango yao mizuri na naomba kuwatambua kwa Majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa John Z. Chiligati, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Muhammed Seif Khatib, Mjumbe; Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mjumbe na Mheshimiwa Eugene E. Mwaiposa, Mjumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mjumbe; Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Muhammed Ibrahim Sanya, Mjumbe; Mheshimiwa John M. Shibuda, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe; Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mjumbe; Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mjumbe na mimi mwenyewe Betty E. Machangu, Mjumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Ndugu Athuman Hussein na Ramadhani Issa, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati. Nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kasilillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuridhia nchi ijiunge na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi wa Kutumia Nyuklia. *(International Convention for Suppression of Acts of Nuclear Terrorism)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru, Msemaji au Mwenyekiti wa Kamati.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA (K.n.y MHE. EDWARD N. LOWASA-MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasoma, naomba taarifa hii ichukuliwe kwenye *Hansard* kama ilivyo kwa sababu sitaweza kuisoma yote kutokana na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia *(Convention*

on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, Including Diplomatic Agents, 1973).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kifungu cha 8(4) na Kifungu cha 9(2)(b), uliipatia kazi Kamati hii kushughulikia Azimio la Bunge la kuridhia kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Pamoja na Wakala wa Kidiplomasia. Mara tu baada ya kupata kazi hii, Kamati ilialika wadau kufika kwenye kikao cha Kamati cha tarehe 23 Januari, 2013 kilichofanyika katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam ili watoe maoni yao. Kamati ilifanya hivyo kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 114(9) na kuzingatia dhima na dhamira ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 63(3)(e) iliyorejewa katika maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi inahusu madaraka ya Bunge kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Hata hivyo, namna yalivyoandikwa mapendekezo ya Azimio la Bunge inajieleza kuwa Bunge linaombwa ridhaa ili Serikali iwezeshe Tanzania kujiunga na Mkataba huu kwa sasa. Si jambo lililozoeleka kwa Bunge kuridhia kujiunga kabla ya kusaini badala ya kuridhia baada ya Serikali kuwa imesaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Kamati, Serikali na Wadau kilichofanyika tarehe 23 Januari, 2013, Wataalam kutoka Asasi za Serikali, Asasi za Kiraia (AZISE) na wadau wengine walioalikwa waliomba muda zaidi ili waweze kujiandaa na kutoa maoni yanayozingatia ipasavyo misingi na taratibu ya kuridhia mikataba ya

Kimataifa (*Ratification*). Kwa kuzingatia kuwa Bunge ni chombo halisi cha wananchi na kwamba kinazingatia matarajio yao, Kamati iliafiki maombi hayo na kukubaliana na wadau kukutana tena, Ofisi ya Bunge Dodoma ili kusikiliza maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 1 Februari, 2013 Kamati ilikutana na kusikiliza maoni ya wadau. Naomba kukiri mbele ya Bunge hili kuwa utaratibu wa kusikiliza maoni ya wadau (*Public Hearing*) umekuwa wa manufaa makubwa katika dhana ya Demokrasia na ushirikishaji wananchi kwenye uamuzi wa Bunge. Kupitia utaratibu huo, yapo mambo ya msingi na muhimu yaliyojitokeza na kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Mkataba; tarehe 1 Februari, 2013, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa maelezo kuhusu mapendekezo ya Serikali kwamba, Bunge liridhie kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na Wakala wa Kidiplomasia. Pamoja na maelezo hayo wadau walipewa nafasi ya kutoa maoni yao, utaratibu ulioiwezesha Kamati kuzingatia dhima na mwelekeo wa Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo ya Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na maoni ya wadau waliofika kwenye kikao cha Kamati, wajumbe walijadili kwa kina maudhui ya Mkataba unaohusika kujiunga pamoja na dhana nzima ya kuzuia na kuadhibu uhalifu dhidi ya watu wenye kinga ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo, lilikuwa ni kuona kama kuna tija kwa kujiunga na Mkataba huu pamoja na kujiridhisha kuhusu faida au hasara na mafanikio au madhara ya kutojiunga na Mkataba huu. Ili kufanikisha azma ya Bunge katika uridhiaji wa Mikataba ya Kimataifa, Kamati ilifanya mambo yafuatayo:-

(a) Kupitia Ibara zote za Mkataba tangu Ibara ya 1 inayohusu tafsiri kwa mujibu wa Mkataba hadi Ibara ya 18 inayohusu utaratibu wa kufuata kwa nchi inayotaka kujitoa;

(b) Kuchambua na kutafakakri kuhusu maoni ya wadau na maelezo ya mtoa hoja;

(c) Kupitia baadhi ya Sheria zinazohusiana na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa na hasa Sheria ya Kubadilishana Wakosaji, Sura ya 368 (*The Extradition Act, Cap. 368*);

(d) Kupitia tovuti ya Umoja wa Mataifa na kuona maelezo yanayotolewa kuhusu asili ya Mkataba, nchi zilizosaini mwanzoni, nchi zilizosaini baadaye, nchi zilizoridhia na nchi ambazo hazijaridhia; na

(e) Kupembua faida na hasara kwa madhumuni ya kulishauri vema Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hizo Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu Mkataba huu. Makubwa miongoni mwa hayo ni mambo yafuatayo:-

(i) Kwa mujibu wa maelezo ya Umoja wa Mataifa kwenye Tovuti yake, Mkataba huu unatokana na mwakilishi wa Kudumu wa Uholanzi (*The permanent Representative of the Netherlands*) kwa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa akionesha wasiwasi kuhusu kushambuliwa kwa wawakilishi wa Kidiplomasia sehemu mbalimbali duniani. Barua hii ilipelekwa kwa Rais wa Mahakama ya Kimataifa (*International Court of Justice – ICJ*) na Mwenyekiti wa Tume ya Sheria ya Kimataifa (*International Law Commission - ILC*).

Mwaka 1971 Tume iliwasilisha taarifa tatu zenye mapendekezo (*drafts*) kuhusu kuzuia na kuadhibu makosa hayo. Mwezi Novemba, 1972, Kamati ya Baraza la Umoja wa Mataifa (*UN General Assembly*) ilipitia mapendekezo hayo. Tarehe 14 Desemba, 1973, Baraza hilo lilipitisha Azimio kwa makubaliano (*By consensus*);

(ii) Mkataba huu ulipata nguvu ya kisheria tarehe 20 Februari, 1977 na jumla ya nchi zilizosaini mwanzoni ni 173 na zote tayari zimeridhia;

(iii) Mkataba unaorodhesha watu wenye Kinga ya Kimataifa kuwa ni Mkuu wa Nchi, Mkuu wa Serikali au Waziri wa Mambo ya Nje na Wanafamilia wanaowasindikiza. Aidha, Mkataba unajumuisha Maafisa wa Serikali au Wawakilishi wa Nchi au Taasisi ya Kimataifa yenye sura ya *Intergovernmental Character*;

(iv) Nchi Wanachama zinatakiwa kuhesabu makosa kadha dhidi ya watu wenye Kinga kama Kosa chini ya Sheria za Nchi hizo. Makosa hayo ni Uuaji, Utekaji Nyara, au Shambulio lingine dhidi yao; na mengineyo. Aidha,

Mkataba unaweka masharti ya nchi kutekeleza Kisheria Mkataba huu;

(v) Nchi nyingi zimeridhia Mkataba kwa kuahirisha Kuridhia Ibara ya 13. Ibara hiyo inahusu nchi Wanachama kutatua tatizo linalotokana na utekelezaji au tafsiri ya Mkataba huu baina yao kwa kujadiliana au kukubaliana. Iwapo nchi hizo hazitafanikiwa ndani ya Miezi Sita, moja kati ya nchi hizo inaweza kupeleka shauri hilo kwenye Mahakama ya Haki ya Kimataifa (*International Court of Justice – ICJ*). Miongoni mwa nchi hizo zimo nchi za Afrika kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ghana na Malawi; na

(vi) Katika orodha ya nchi zilizosaini awali, zilizosaini baadaye, zilizosaini na Kuridhia au zilizosaini lakini hazijaridhia, Tanzania haijaorodheshwa kwenye Tovuti ya Umoja wa Mataifa inayoonekana na Dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo ya Serikali, Bunge linashauriwa Kuridhia Tanzania ijiunge na Mkataba huu, lakini kwa kuahirisha Kuridhia Ibara ya 13 ya Mkataba huo. Kuhusu mapendekezo hayo, jambo hili lilikuwa na mjadala mrefu ili kuzingatia vema maslahi ya nchi yetu. Wapo walioona kuwa Kuridhia kwa kuahirisha Ibara ya 13 hakuna maana yoyote kwa kuwa Ibara hiyo haijaridhiwa na sehemu kubwa ya nchi Wanachama zikiwemo nchi za Afrika kama vile Ghana, Burundi, Ethiopia, DRC, Algeria na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika majadiliano hayo yalipatikana maoni kuwa takriban 90% ya Nchi Wanachama hazijaridhia Ibara ya 13 na kwamba kwa

Tanzania Kuridhia au kutoridhia Ibara hiyo hakuna athari yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatimaye Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu Ibara hii. Mantiki ya uamuzi huo ni kuwa hakuna athari yoyote kwa kutokuridhia Ibara ya 13 kwa sasa, jambo ambalo hakuna mwenye maoni tafauti na hilo. Aidha, haki ya kuahirisha kuridhia Ibara yoyote ya Mkataba wa Kimataifa ni ya msingi kwa nchi Wanachama wa Mkataba huo. Kutumia haki iliyopo ni jambo la maana na hasa pale inapotakiwa kutafakari mambo muhimu kwa maslahi ya Taifa husika.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; yapo maoni mahususi na mengine ya jumla kuhusu pendekezo la Serikali Kuridhia kujiunga na Mkataba huu. Maoni ya jumla ni pamoja na yafuatayo:-

Kwanza, Mkataba huu ni wa Mwaka 1973, Miaka 40 leo wakati Serikali inapendekeza kuwa Bunge liridhie Mkataba huu. Hali hii inahitaji ufafanuzi wa kina kuhusu masuala mbalimbali ya msingi kabla ya kuridhia. Kwa mfano, kwa Bunge kuombwa Kuridhia kujiunga leo kuna mambo gani yaliyosababisha Tanzania isitake kujiunga na Mkataba miaka iliyopita. Ni kitu gani kilichozuia Bunge kuombwa ridhaa ya kujiunga na Mkataba huo wakati huo na sasa hakipo tena ili Bunge liridhie.

Pili, Serikali inashauri Bunge liridhie kujiunga na Mkataba huu kwa kuahirisha Ibara ya 13. Hoja hapa ni kwamba iwapo nchi itaridhia Mkataba huu kwa kuahirisha kuridhia Ibara ya 13 ambayo nchi nyingi nazo zimefanya hivyo, ikitokea kutoelewana kuhusu tafsiri au utekelezaji wa

Mkataba baina ya nchi yetu na nchi nyingine Mwanachama na tukashindwa kuelewana kwa majadiliano (*negotiation*) au usuluhishi (*arbitration*) ikiwa tumejiunga na kuridhia Mkataba huu, njia gani tunaweza kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na maoni ya jumla kuhusu mapendekezo ya Kuridhia Mkataba huu, Kamati ina maoni mahususi katika maeneo mawili ya Mkataba huu:-

(a) Wajibu wa Mahakama ya Nchi kutumia uwezo wake katika makosa yaliyotajwa chini ya Ibara ya 2 ya Mkataba huu; Ibara ya 3 ya Mkataba huu inataka Mahakama yetu kuwa na uwezo (*Jurisdiction*) wa kushughulikia makosa yaliyotajwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba huu. Ili Kuridhia kujiunga na Mkataba kuwe na maana, mara baada ya kujiunga na kuridhia, Sheria za Nchi zizingatie masharti ya Ibara ya 3 ya Mkataba huu na kuzipa Mahakama uwezo wa kushughulikia makosa husika kwa mujibu wa Ibara ya 3.

(b) Kubadilishana Wakosaji (*extradition*); Ibara ya 8 ya Mkataba huu inahusu kubadilishana Wakosaji (*extradition*) miongoni mwa Nchi Wanachama na masharti yake. Makosa yanayohusika ni yale yaliyotajwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba huu. Ni muhimu kwetu kuwa na Sheria za Nchi zinazowezesha masharti ya Ibara ya 8 ya Mkataba huu. Kamati inashauri kuwa Sheria ya Kubadilishana Wakosaji, Sura ya 368, *The Extradition Act, Cap. 368* na Sheria nyingine zifanyiwe kazi kabla ya kuiingiza nchi yetu katika wajibu unaoelezwa katika Ibara ya 8 ya Mkataba.

(c) Kubainisha muda utakaochukuliwa kuoanisha Sheria na vifungu vya Mkataba huu, kwa kuwa Serikali imeonesha kuwa ni muhimu kwa Tanzania Kuridhia Mkataba huu na kwa vile Uridhiaji huu utakuwa na maana iwapo Sheria zetu zitaendana na Mkataba unaoridhiwa, ni vizuri Serikali ikabainisha itachukua muda gani kuoanisha sheria zetu na Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, napenda kuchukua nafasi kukushukuru kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Pamoja na Wakala wa Kidiplomasia. Namshukuru pia Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Wataalam wa Wizara hiyo, kwa kutoa ufafanuzi uliohitajika wakati wa Vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu, Chuo cha Diplomasia, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini na Chuo cha Ulinzi wa Taifa kwa maoni yao mazuri waliyoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao mizuri na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

MWENYEKITI: Mheshimiwa huna muda nenda moja kwa moja kwenye hitimisho 4.4. Umebakiwa na dakika tatu tu.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA (K.n.y. MHE. EDWARD N. LOWASA-MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia.

MWENYEKITI: Mimi ndiyo nakwambia, una dakika tatu tu.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA (K.n.y. MHE. EDWARD N. LOWASA-MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna Abdallah Mjumbe; Mheshimiwa John Z. Chiligati, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Muhammed Seif Khatib, Mjumbe; Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mjumbe; Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mjumbe na Mheshimiwa Eugene E. Mwaiposa, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mjumbe; Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Muhammed Ibrahim Sanya Mjumbe, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe; Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mjumbe na mimi Anastazia Wambura, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Ndugu Athuman Hussein na Ramadhani Issa,

Makatibu wa Kamati hii, wakisaidiwa na Ndugu Gaitana Chima kwa kuratibu vema shughuli za Kamati. Nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuridhia kujiunga na Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Pamoja na Wakala wa Kidiplomasia (*Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, including Diplomatic Agents, 1973*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

MHE. VINCENT J. NYERERE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni Hotuba ya Msemaji Mkuu, Kambi Rasmi ya Upinzani, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi kwa Kutumia Nyuklia (*International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunijalia mimi na familia yangu afya njema na kuniwezesha kusimama hapa kutoa msimamo wa Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio lililopo mbele yetu. Aidha, nachukua fursa hii pia, kuwatakia heri

na Baraka za mwaka mpya bila kuwasahau wananchi wa Jimbo langu la Musoma Mjini na Makamanda wote wa CHADEMA popote walipo katika nchi yetu. Kipekee nawashukuru viongozi wote wa CHADEMA kwa shughuli mbalimbali za chama wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza wanachama wote wa CCM kwa kutimiza miaka 36 ya kuanzishwa kwa chama chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo ni Chama Tawala, kinachoongoza nchi, lakini inasikitisha kwamba, kimesahau hata tarehe ya kuzaliwa kwake na hivyo kufanya sherehe za kumbukumbu ya kuzaliwa kwake tarehe 3 Februari badala ya tarehe 5 Februari. Hii ni dalili kwamba, chama hicho kimeanza kupoteza kumbukumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutafakari suala la kuuridhia mkataba huu wa Kimataifa ni vyema kwanza tukaitazama Katiba yetu na hasa kuhusiana na tafsiri ya neno “DOLA”, kwani kwa mujibu wa mkataba huu ibara ya (1) ni kuwa, tafsiri ya Dola ni pamoja na maafisa wanaofanya kazi kwenye Mashirika ya Kimataifa katika kutimiza majukumu yao ya kikazi: *“State or Government Facilities include; ...officials of an International Organization in connection with their official duties”* [Ibara ya 1(5)].

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inataka kujiridhisha kuwa Tanzania tunakubaliana na tafsiri hii mpya ya neno Dola katika msingi wa kuufanya Mkataba huu uweze kutekelezeka kikamilifu? Aidha, ni muhimu kujiridhisha kama Katiba yetu inawiana na tafsiri hiyo ama laa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema vile vile kujua mkataba huu unahusiana vipi na mkataba wa kuzuia ugaidi pamoja na sheria ambayo imetungwa na Bunge hili baada ya mashambulizi ya kigaidi yaliyofanyika mwaka 2008 kwenye Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania na Kenya na yale mashambulizi ya kigaidi yaliyofanyika huko Marekani kwenye jengo la *World Trade Centre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8 ya mkataba huu, inatoa mamlaka kwa Tume ya Kimataifa kutoa mapendekezo ya kufanya uchunguzi wa athari zilizopo katika nchi juu ya matumizi ya nyuklia kwa namna yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali, kutoa mapendekezo kwa Umoja wa Mataifa juu ya umuhimu wa sisi kama nchi, kutumia vyombo vyetu vya ndani kupata ufumbuzi wa athari za nyuklia na sio kusubiri Tume ya Umoja wa Mataifa kuja kuchunguza matukio yaliyotokea katika nchi yetu. Pia, kuwasomesha vijana wa Kitanzania walio tayari ambao wapo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, nchi yetu inayo Tume ya *Atomic* ambayo ina uwezo na uhalali wa kuchukua hatua juu ya athari zinazotokana na nguvu za Atomiki, ingekuwa ni busara Tume yetu ikapewa jukumu hilo ili kutoa ufumbuzi wa haraka wa tishio lolote la kinyuklia katika mazingira ya dharura kuliko kusubiri Tume ya Kimataifa wakati tatizo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 9(1)(b) ya Mkataba huu, inaeleza wazi kuwa kosa linaweza kutendwa na

chombo ambacho, ama kimesajiliwa kwenye nchi moja au wakati makosa yanatendeka kinakuwa kikipeperusha bendera ya Taifa husika wakati huo:

“The offence is committed on board a vessel flying the flag of that state or an aircraft which is registered under the laws of that state at the time the offence is committed” [Ibara ya 9(1)(b)].

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Agosti 2012, meli zipatazo 36 zilikuwa zikipeperusha bendera ya nchi yetu, wakati zilikuwa ni mali ya Taifa la Iran. Jambo hili lilitia nchi yetu doa, kwani ilionekana kama vile tunashiriki katika biashara za magendo na au vitendo vingine vya kiharamia au ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inauliza, hivi kweli, Serikali, imeliandaa vipi Taifa kukabiliana na hali kama hiyo kuhusiana na masuala haya ya Nyuklia kabla ya kuridhia mkataba huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 9 kifungu cha 2(a) inazungumzia suala la uwanda wa mamlaka ya ndani ya nchi kushughulikia masuala ya kijinai yanayofanywa ndani ya nchi kwa nchi husika: kwenye mapendekezo ya Serikali, haioneshi ni vipi Serikali, imejiandaa kutumia fursa ya kutatua matatizo yake nchini. Ni vema Serikali, sasa ikarejea Sheria zilizopo nchini na kuweza kuzitumia kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali, kuhakikisha kuwa, katika kutekeleza ibara ya 9, kifungu cha 3 inaweka bayana kuwa Sheria zitakazotumika kwa watakaobainika kuyatenda makosa ni Sheria zetu za

ndani zilizotungwa na Bunge hili, kama zilivyofanya nchi nyingine mbalimbali kama vile Ujerumani ambao wameweka bayana kuwa watatumia Sheria yao ya mwenendo wa makosa ya jinai. Zipo pia nchi nyingine kama Jamhuri ya watu wa Czech, Georgia, Nigeria, Urusi na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkataba huu kuwa na lengo la Kudhibiti Vitendo vya Ugaidi kwa kutumia Nyuklia na kutoa haki ya kila nchi kutumia na kuendeleza rasilimali za Nishati ya Nyuklia nchini mwake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusesitiza kwamba, ni vema kurejea Kauli yake katika wasilisho la hotuba ya Maliasili na Utalii ya Mwaka 2012, juu ya Uchimbaji wa Madini ya Urani nchini, kwa kurejea taarifa za mikataba iliyokwishasainiwa na Serikali na Makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kambi ya Upinzani kwamba, tunahitaji kupanga matumizi ya rasilimali zetu kama Taifa na sio kusubiri kushawishiwa na Mataifa makubwa juu ya matumizi ya rasilimali zetu. Kinyume na hapo ni kuidhihirishia Jumuiya ya Kimataifa kwamba, bado hatujajitawala na kwa maana hiyo hakuna haja za kuwa na sherehe za uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji na uchimbaji wa *Uranium* nchini, hususan katika Taifa changa kama Tanzania, ni hatari kwa maisha ya binadamu na ustawi wa nchi. Kwa kurejea historia ya hivi karibuni takribani miaka miwili iliyopita kwa nchi zilizoendelea na kuwa na teknolojia kubwa na madhara yaliyopatikana kutokana na matumizi ya *Uranium* katika kuzalisha nishati, ni vema kama Taifa tukasita kuingiwa na tamaa ya kutumia kila rasilimali

tulizonazo pasipo kujiandaa katika kuweza kukabiliana na madhara na matokeo ya matumizi yake. Badala yake tuelekeze nguvu na maarifa katika umeme wa gesi kuliko matumizi ya urani ambayo yanaweza kuwa hatari kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maazimio ya Serikali katika Mkataba huu yanaeleza mafanikio ya Kimkataba kwa nchi pasipo kuainisha wazi, ili Wabunge waweze kupata uelewa zaidi na kujiridhisha na mafanikio yaliyopo. Pamoja na kutoweka bayana juu ya hayo mafanikio, pia athari zake hazijawekwa bayana katika mkataba huu na ni jinsi gani kama nchi, itaathirika kwa kuingia katika Mkataba huu wa Kimataifa; kwa mfano, ni vema kusoma kwa makini, kujadili na kukubaliana msimamo wetu kama Taifa kuhusu ibara ya 23 kifungu (1), (2) na (3) kabla ya kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali, kutoa ufafanuzi pamoja na kuazimia kutofungwa na kifungu hicho. Ni vema tukawa na uelewa mpana juu ya vipengele vyote vyenye madhara mabaya kwa nchi kabla ya kuridhiwa kwa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, imefuatilia kwa muda mrefu sasa kuhusiana na jinsi ambavyo mikataba hii ya Kimataifa inavyoingwa na kusainiwa na kugundua kuwa, wawakilishi wetu kwenye Umoja wa Mataifa kwa miaka ya karibuni, wamepoteza ule umakini wa kufuatilia na kushughulikia masuala ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatokana na ukweli kuwa, wakati Umoja wa Mataifa unaunda Kamati ya Muda kwa ajili ya kujadili na kupokea mapendekezo mbalimbali kuhusiana na azimio hili, katika azimio lake namba 54/110 la Disemba 1999, waliamua kuridhia kuwa, Azimio Namba 51/210 la tarehe 17 Disemba, 1996 Kamati iliyokuwa imeundwa chini ya Uenyekiti wa *Mr. Rohan Perera* wa Sri Lanka, ikutane kuanzia tarehe 14 – 18 Februari, 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania, haikuwasilisha mapendekezo yoyote kuhusiana na azimio hili. Hali hii ipo kwenye Maazimio mengine kadha wa kadha ambayo, hatuonekani tena tukiongoza Afrika katika Diplomasia ya Kimataifa kama ilivyokuwa wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere; ule weledi wetu umekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru. Huo wa pili?

MHE. VINCENT J. NYERERE – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hii ni Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa Pamoja na Wakala wa Kidiplomasia wa Mwaka 1973; (*Convention on the Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons, Including Diplomatic Agents, 1973*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwatakia heri na Baraka za mwaka mpya Waheshimiwa Wabunge wenzangu na pia wananchi wote wa Jimbo langu la Musoma Mjini na makamanda wote wa CHADEMA popote walipo katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania. Aidha, natoa shukrani na pongezi kwa viongozi wa ngazi zote wa CHADEMA kwa kufanikisha kumalizika kwa mkutano wa Baraza Kuu la CHADEMA mwezi uliopita na kwa harakati mbalimbali za kukiimarisha chama zinazoendelea nchi nzima zenye lengo la kuweka mikakati na mipango madhubuti ya kujiandaa kuchukua dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza wanachama wote wa CCM kwa kutimiza miaka 36 ya kuanzishwa kwa chama chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Japo ni chama tawala, kinachoongoza nchi, lakini nasikitika kwamba, kimesahau hata tarehe ya kuzaliwa kwake na hivyo kufanya sherehe za kumbukumbu ya kuzaliwa kwake tarehe 3 Februari badala ya tarehe 5 Februari. Hii ni dalili kwamba, chama hicho kimeanza kupoteza kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani haina pingamizi la kuridhiwa kwa Mkataba huu ambao ulizinduliwa tangu mwaka 1973. Hii ni kwa sababu ya lengo lake zuri la kuwalinda viongozi wa Kiserikali na Kisiasa wanaotembelea nchi nyingine na wale wanaofanya kazi au kuziwakilisha nchi zao katika Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutambua umuhimu wa kuwalinda watu wenye kinga za Kimataifa na Wakala wa Kidiplomasia, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini

baadhi ya upungufu katika mkataba huu; mosi, ni kwamba, mkataba huu haumtambui raia mwingine wa kawaida, ambaye hana hadhi ya kidiplomasia, anayeishi au kufanya kazi katika nchi nyingine katika masuala ya ulinzi na usalama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu kwa umma wa Watanzania kwamba, je, Watanzania wengi wanaosoma, kufanya kazi au biashara nje ya nchi, ambao ndio waliowapigia kura na kuwapa viongozi hadhi ya kidiplomasia na hivyo kustahili kulindwa Kimataifa, wao hawahitaji kulindwa pia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Serikali, itajibu swali hilo kwa uaminifu, ni dhahiri wataona kwamba, mkataba huu una asili ya utabaka kwa maana ya kwamba, unabagua kati ya watawala (Wakubwa) na watawaliwa katika masuala ambayo hayahitaji mjadala hata kidogo (*non-negotiable matters*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia uhalifu dhidi ya binadamu ni haki ya kila binadamu na si haki ya viongozi au Wanadiplomasia peke yao. Hivyo kutoa haki ya ulinzi na kutoa adhabu kwa uhalifu dhidi ya wenye hadhi ya kidiplomasia peke yao ni kwenda kinyume kabisa na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948 ambalo linatambua usawa wa binadamu katika haki za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelezo hayo, Kambi ya Upinzani inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na kikao cha Kamati ya Ufundi (*IMTC*) kuwa tujiunge na Mkataba huu kwa Shaka, ili tusiweze kufungwa na Masharti ya Ibara ya 13(1) ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazingira mengine ambayo yanaweza kusababisha ulinzi kwa wale wote wanaotakiwa kupewa ulinzi kwa mujibu wa mkataba huu kuwa magumu. Kwa mfano, ikiwa hawa wenye hadhi ya kidiplomasia wanafanya makosa ya kijinai kama vile kubaka au kufumaniwa na mke au mume wa mtu na nguvu ya umma ikachukua mkondo wake. Au kujihusisha na biashara haramu kama vile madawa ya kulevya na mwisho wa siku wakadhulumiana na hivyo kulipiziana visasi na kuumizana au hata kuuana, katika mazingira kama hayo ni nani anatakiwa kuchukuliwa hatua au Serikali, inatakiwa kusimama upande gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazingira mengine ambapo Wanadiplomasia na Mawakala wa Kidiplomasia wanajihusisha na vitendo ambavyo ni kinyume cha Mikataba ya Kimataifa na hivyo, kuishia kukamatwa na kutiwa mbaroni na vyombo vya dola kwenye nchi husika. Matendo hayo ni pamoja na Wanadiplomasia hao kujihusisha na vitendo vya kijasusi (*espionage*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalisema hili kutokana na uzoefu wa Kimataifa ambao tayari unaonesha kwamba, kuna kesi mbalimbali zilizofunguliwa kwenye Mahakama za Kimataifa kuhusiana na Wanadiplomasia walivyojijihusisha na uhalifu katika nchi za ugenini. Mfano mzuri hapa ni kesi iliyofunguliwa na Marekani katika Mahakama ya Haki ya Kimataifa dhidi ya Iran kwa kuwashikilia wananchi wake waliokuwa na hadhi ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kesi hii ya *“The United States Diplomatic and Consular Staff in Tehran case”* (I.C.J.

Reports, 1980) ni kwamba, Iran iliwakamata Wanadiplomasia na Watumishi katika Ubalozi wa Marekani ulioko Tehran kwa kufanya ujasusi Iran kinyume na sheria za nchi ya Iran. Kwa hiyo, Marekani ilifungua mashtaka dhidi ya Iran kwa kutumia Mkataba wa Vienna (*Vienna Convention 1969*) kwa kuwakamata raia wake wenye hadhi ya Kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ya hivi karibuni kabisa ya aina hiyo ni ya Uganda dhidi ya *Congo DRC*, ambapo *Congo DRC* imeshtakiwa kwenye Mahakama ya Haki ya Kimataifa kutokana na Wanajeshi wake kuvamia Ubalozi wa Uganda uliopo Kinshasa na kuwaweka chini ya ulinzi Watumishi wa Ubalozi huo “*The case concerning armed activities on the territory of the Congo (Democratic Republic of the Congo v. Uganda) I.C.J. Reports 2005.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inajiuliza kuingia kwenye Mkataba huu kutatuathiri vipi kama Taifa katika kuwashughulikia wale wote ambao wana hadhi za Kidiplomasia na Uwakala wa Kidiplomasia na kutumia kinga zao katika kufanya mambo ambayo ni kinyume na Sheria zetu za ndani na ambavyo vinaathiri usalama wa Taifa letu? Je, bado tutakuwa na haki za kuwashughulikia ama ndio tunakwenda kujifunga mikono katika kushughulikia wahalifu ambao wana kinga za Kidiplomasia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Vienna wa mwaka 1969 tayari ulikwishatambua majukumu makubwa yanayotekelezwa na Wakuu wa Nchi na Mawaziri wake wa Mashirikiano ya Kimataifa katika Mahusiano ya Kimataifa. Hivyo, Mkataba huu kwa nchi yetu, hauna tofauti na Mikataba hiyo ya Vienna, cha ziada ni kuongeza ubaguzi

na kukinzana na Kanuni ya Utendaji kazi wa Jeshi la Polisi inayosema kuwa:

“Ulinzi wa maisha na mali za raia ni kazi muhimu za Jeshi la Polisi na hii ni katika kuhakikisha Sheria za Nchi nzima zinafuatwa bila ubaguzi. Hivyo basi, ni jukumu la kila mtumishi wa Jeshi la Polisi kuhakikishia wananchi kuwa kuna usawa wa Sheria pasipo kuangalia au kujali madaraja na vyeo vya jamii, maoni ya kisiasa na uchumi, kwa kuwatendea watu wote kwa utu na heshima”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni hiyo, ni dhahiri kuwa Bunge kuridhia tuingie kwenye Mkataba huu kwa Shaka (*with reservation*) ni jambo jema kwa kuwa, Mkataba huu unaweka madaraja ya ulinzi kwa wananchi na unakinzana na Kanuni hii ya utendaji wa Jeshi la Polisi. Tukumbuke kuwa, nchi yeyote haikatazwi kutoridhia Mkataba wowote ule kama unakinzana na Misingi ya Sheria za Ndani ya Nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania bado haijasaini Mkataba huu wa Kimataifa kama Ibara ya 17 ya Mkataba inavyosema kuwa:

“This Convention shall enter into force on the thirtieth day following the date of deposit of the twenty-second instrument of ratification or accession with the Secretary-General of the United Nations”. Kwa kuwa, *“Implementation Kits for the International Counter – Terrorism Conventions”* inaonesha kuwa, hadi mwezi Septemba 2002, Mkataba ulikuwa tayari na wanachama 121 ambao kati ya hao nchi za Jumuiya ya Madola zilikuwa ni 24 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kusaini Mkataba ndiyo hatua ya kwanza kabisa katika utaratibu mzima wa kutaka kujiunga na Mikataba ya Kimataifa, *“Signing the instrument does not create a binding legal obligation but does demonstrate the State’s intent to examine the treaty domestically and consider ratifying it. While signing does not commit a State to ratification” (UNICEF 2005).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali, bado haijaweka saini katika Mkataba huu, au kama tayari imesaini, Kambi ya Upinzani inalishawishi Bunge hili kuwa, liazimie kuwa, tuingie kwenye Mkataba huu kwa “kujiunga kwa shaka” (*with reservation*), ili kuhakikisha kuwa hatutafungwa na Masharti ya Ibara ya 13(1) inayoweka Masharti kuwa migogoro baina ya nchi wanachama kuhusu tafsiri au matumizi ya Mkataba huu itatatuliwa kwa njia ya majadiliano na usuluhishi. Kama nchi wanachama zitashindwa kuafikiana, nchi mojawapo inaweza kupeleka mgogoro huo katika Mahakama ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

Michango! Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kifungu cha 68(7), kinachosema:

“Halikadhalika Mbunge, anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika, atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika, yatatolewa papo hapo au baadaye, kadiri atakavyoona inafaa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kilichonisimamisha pia ni 64 (a), kinachosema: “Mbunge, hatatoa ndani ya Bungeni taarifa ambazo hazina ukweli.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliyemaliza kuongea muda mfupi uliopita, amefanya jambo la kistaarabu sana kuwapongeza CCM kutimiza miaka 36 tangu kuzaliwa. Lakini baadaye amesema maneno yafuatayo, nayanukuu ambayo ni ya uwongo:-

“Mheshimiwa Mwenyekiti, japo ni Chama Tawala kinachoongoza nchi, lakini nasikitika kwamba, kimesahau hata tarehe ya kuzaliwa kwake na hivyo kufanya sherehe ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwake kuwa tarehe 3 Februari badala ya 5 Februari. Hii ni dalili kwamba, chama hicho kimeanza kupoteza kumbukumbu.”

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa wala simtaki afute usemi, wala simtaki aombe radhi, nataka kumpa

darasa tu kwamba, enzi ya Chama Kimoja tarehe 5 Februari...

WABUNGE FULANI: Aaaaah.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:
Naomba, niacheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea na wewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, endelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa ni kumwomba ndugu yangu apokee Taarifa kwamba, Chama cha Mapinduzi, kinafahamu kuzaliwa ni tarehe 5 Februari. Lakini pia, Chama cha Mapinduzi, kinaheshimu Taratibu kwamba, sasa tuko katika Mfumo wa Vyama Vingi; inapoangukia tarehe 5 Februari, siku ya kazi huwezi ukaacha watu wasiende kazini, wanafanya sherehe. Ni sawasawa na kwamba, mtu anaweza akawa na tarehe yake ya kuzaliwa, ikiangukia siku ya kazi, anaweza kuisogeza, akaifanya siku nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba tu Mheshimiwa Mbunge, ustaarabu tu, kupokea maelezo haya. Aelewe kwamba, sisi wenye chama tunaelewa tarehe kiliyozaliwa, tulifanya makusudi kwa akili zetu timamu. *(Makofi)*

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyerere, hebu kaa chini kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, maneno anayosema Waziri wa Nchi ni sahihi. Kama ulikuwa na lengo la kueleza kwa njia ya *humour*, humu ndani sio sehemu yake. Inafahamika kabisa sherehe, na sio mwaka huu miaka mingi, Chama hiki kinaheshimu muda na tarehe za mapumziko. Kwa vile, amekuomba upokee Taarifa, huna haja ya ku..., kama umeipokea ipokee, la kama hujaipokea, sema tuendeleo na shughuli zetu.

Habari lakini imefika.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei Taarifa kwa sababu, kumbukumbu zinaonesha tarehe ya kuzaliwa kwa CCM ni tarehe 5 Februari.

MWENYEKITI: Haya, kaa chini. Tunaendelea na mjadala. Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa!

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Maazimio haya mawili ambayo ni Azimio la Bunge la Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, kuhusu kuridhia kujiunga na Mkataba wa Kuzuia Kuadhibu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa pamoja na hili Azimio la Bunge kujiunga na Mkataba wa Kimataifa Kuzuia Vitendo vya Ugaidi kwa Kutumia Nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema kwamba Maazimio haya yalipitishwa tarehe 13 Aprili 2005 huko Umoja wa Mataifa kwa *Resolution* ile namba *ARES 59/290*, huu ni mwaka wa nane. Katika Maazimio hayo katika *Article* ya 24 ilitolewa nafasi kwa Nchi zote Wanachama

kuanzia tarehe 14 Septemba, 2005 hadi tarehe 31 Desemba 2006, kuridhia kwa kusaini ule mkataba. Bahati mbaya nchi ambazo zimesaini ni 141 kati ya nchi za Umoja wa Mataifa zinazojulikana mpaka leo 192.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kusema kwamba, kuna nchi 51 bado hazijatia sahihi, lakini leo mnaleta hapa ili Bunge liridhie wakati Tanzania yenyewe haikutia sahihi au unaweza kusema haijaamini mkataba huu. Sasa hiki ni kitu ambacho kidogo kinatushtua Wabunge kwa sababu mara nyingi sana Bunge hili linaridhia au lina-*ratify*, hapa baada ya Tanzania kusaini. Ni mara nyingi sana tunachelewa kusaini na tunasema kwamba pale nchi inapochelewa inakuwa labda inatafakari vile vipengele vyenye utata au kwa sababu fulani fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kuomba hapa Bungeni kwamba pale Tanzania inapokuwa haisaini Mkataba wowote wa Kimataifa likakaa miaka 15, 20 ni vyema basi Serikali inapokuja hapa Bungeni iwe inatueleza, walikaa muda wote huo kwa sababu kulikuwa na sababu moja, mbili, tatu ili na sisi Wabunge yale mambo ya ndani ya Kiserikali tuweze kuyafahamu kwa nini ilichelewa kusaini. Halafu Wabunge tutakaporidhia tunaridhia kwa kuelewa nchi yetu ilichelewa kwa sababu kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote mpaka sasa hivi hayajatendeka, lakini itakuwa hii ni *fashion* ya kwanza, ni ya aina yake, kwamba Tanzania inaleta hapa Mkataba wa Kimataifa tuuridhie wakati yenyewe haikusaini, hapa pananipa wasiwasi. Mikataba yote miwili hii Tanzania haijasaini, lakini huu wa pili naweza nikazona sababu. Huu wa mwanzo labda ndiyo kila wakati tunafanya kazi kwa

zimamoto kwa sababu Tanzania imepatikana *Uranium*, kwa hiyo sasa ndiyo tunaleta hapa kuridhia kwa muda wote ule hatukuona maana au namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo haya ni mambo ambayo Serikali ilipaswa itueleze. Sasa kitu kimoja ambacho naona Serikali bado haijatupatia tafsiri neno ugaidi, gaidi na ugaidi ni neno ambalo lina tafsiri pana, ni neno ambalo lina *perception* (dhana) inayotegemea itikadi, inategemea silka, mila wakati mwingine inategemea hata mambo ya dini. Sasa ile tafsiri halisi ya ugaidi na gaidi bado hatujapatiwa. Ni vema kwanza Serikali ingejiridhisha, huyu anayeitwa gaidi ni nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais mstaafu wa Afrika Kusini Nelson Mandela aliwahi kuitwa gaidi na nchi za Magharibi wakati ule kwa vitendo vyake vya mapambano ya kupigania uhuru, lakini baadaye akaja akawa Rais wa Afrika Kusini. Sasa hii tafsiri ya gaidi na ugaidi ni nini. Siyo hivyo tu, Rais Bush aliivamia Iraq kwa kusema kuna magaidi, kuna silaha za maangamizi na nini ambazo hazikuonekana, alitafuta sababu ya kuvamia hiyo ambayo ni hiyo ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tafsiri ya gaidi na ugaidi duniani ni nini hasa. Kuna mtu mmoja mama yake walimpa jina la Jose lakini umaarufu wake ni *Carlos the Jackal*. *Carlos the Jackal* alifanya ugaidi mkubwa sana duniani. Alivamia majengo mengi sana duniani, akaua sana na mwisho Wafaransa wakamkamata Sudan lakini kwa kuwa hakukuwa na ule mkataba wa namna gani ya kukabidhiana, ikabidi atekwe nyara. Lakini kwa mtazamo mpana hakuvuma ugaidi wake wala hazikutungwa sheria

za ugaidi kwa wakati huo alipokuwa anafanya vitendo hivyo, lakini vimetungwa alipokuja huyu anayeitwa Osama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hili neno ugaidi linahitaji tafsiri pana na ili tuelewe ugaidi ni nini na ni namna gani. Tusije tukatumbukia katika kupitisha hapa Azimio halafu likaja likatubana wenyewe kwa sababu ya *uranium* ambayo imeonekana huku Tanzania. Katika hili ningeomba tuwe waangalifu sana ili tusije tukajitumbukiza katika sehemu ambazo zitatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya pili ya Azimio hili kuna kauli umiliki wa zana za nyuklia lakini kasoro kubwa ya Ibara hii ni pale mkataba huu unaposhindwa kuweka bayana mtu mhalifu kwani inaishia tu kusema anayemiliki dhana kwa nia ya kusababisha kifo au madhara mengine. Haijafafanua zaidi katika Ibara hii, sasa wasiwasi wangu tusije tukaridhia halafu sisi wenyewe tunapotaka kununua zana za kijeshi mkataba huu ukatubana, kwa sababu ufafanuzi haujafafanua vizuri Ibara hii ya pili, au wale wenye *department* ya fizikia wasije wakatafuta vifaa fulani, ikaja ikatubana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inaonekana sasa hapa pana matatizo kidogo na inawezekana ndiyo zile sababu ambazo zimepelekea tumekaa miaka mingi sana Tanzania haikusaini. Kwa hiyo, ni vitu ambavyo vya kutazama na si vyema kuvamia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo mfupi, lakini naomba hayo yazingatiwe. Asante sana.
(Makofi)

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia mchana wa leo katika Maazimio haya mawili. Moja kwa moja nitakwenda katika suala zima la Azimio moja la Kuzuia Ugaidi kwa Kutumia Nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani imepita miaka saba kila mtu ameshazungumza hapa, leo hii Mikataba hii ndiyo inakuja hapa Bungeni kwa ajili ya kuridhia. Lakini naomba sana tukae na tathimini pana hasa tunapofanya mijadala yetu hii. Kwa sababu nina imani mikataba mingine ina maslahi kwetu, lakini Mikataba mingine ina maslahi kwa wachache na nina wasiwasi sana hasa hii Mikataba ya Kimataifa, mara nyingi utakuta katika nchi za wenzetu zilizoendelea jambo lolote linafanywa kwa ajili ya kuweka maslahi ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napata wasiwasi hasa katika suala zima la ushirikiano na nchi mbalimbali tulizokuwa nazo. Naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri akija hapa naomba atufafanulie wazi kwamba, je, tunaporidhia Mkataba huu leo kwa mfano nchi moja iliyoendelea inapokwazana na nchi nyingine katika maslahi yao ya kiuchumi, kwa mfano, nchi iliyoendelea inapokwazana na Iran au Korea ambao sisi tuna mahusiano ya Kibalozi na nchi yetu, tunaathirika vipi wao wanapokuwa wanapambana wenyewe kwa wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi sana kwamba, isije kufikia muda mara baada ya kuridhia na sisi Tanzania tukawa tumeingia kitanzini. Inawezekana kuna nia njema kabisa, lakini naomba tuwe na tafakari pana hapa kwamba, je tutaathirika vipi? Kwa hiyo, lazima tujue kuhusu

kuridhia kwetu na mahusiano mbalimbali tuliyonayo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, tuangalie raia wetu, inawezekana ikafika muda baadhi ya nchi mbalimbali duniani huenda zikataka kuja kwa ajili ya kukwazana na taasisi au na watu binafsi hapa wakachukuliwa kwamba ni magaidi wa nyuklia na hapa katika suala zima la kubadilishana hawa raia ambao wanafanya ugaidi au kushukiwa, je, kama nchi tutasimama wapi katika maeneo hayo? Isije ikatokea kwamba, tumeridhia Mkataba huu kesho na kesho kutwa kuna watu wana nia yao nyingine tofauti wakaja hapa kuvamia baadhi ya taasisi wakiziita kwamba hizi taasisi zinashirikiana na mambo ya ugaidi wa nyuklia. Inawezekana tukafanya dhuluma kubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema inawezekana kuna madhumuni mazuri sana, lakini naomba kwa sababu kuna mashaka ndani yake, hata Kamati yenyewe imekuja kuwasilisha kwa kuonesha kwamba, kuna mashaka. Kwa hiyo, hapa kama viongozi inatakiwa tuwe na tafakari pana sana kwamba nini athari za kuridhia mkataba huu kama nchi. Lakini hali kadhalika kama wananchi wetu kwa sababu tunaona wazi kuna wananchi wengine, katika suala zima la sheria ya kiugaidi, walikamatwa tu na kutekwa na kupelekwa nchi nyingine mbalimbali kwa kushukiwa magaidi bila kupata ushahidi wa kutosha. Hili jambo tuna kila sababu ya kujifunza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isije ikatokea kwamba watu wanatengeneza *agenda* zao, halafu wanakuja kutengeneza katika maeneo ya mazingira ya nchi yetu,

nadhani tutakuwa tumeleta migogoro mikubwa sana katika nchi yetu. Kwa hiyo, nasema kwamba, Mkataba ni vyema kuuridhia, lakini je tumejiridhisha. Kwa sababu inaonesha kwamba, kuna vipengele vingine bado tuna shaka navyo, hapa inaonekana kwamba bado kuna mahali pengine hapajakuwa pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni la rasilimali. Tanzania yetu sasa hivi tuna rasilimali za kutosha, nina wasiwasi kwamba, kutokana na wingi wa rasilimali yetu hii tuliyokuwa nayo hasa suala zima la gesi na mambo ya madini, wasije watu wengine wakaja kutubambikizia Tanzania, kwamba Tanzania imewahifadhi watu wanaofanya ugaidi wa nyuklia, wakaja kuvamia lengo ni ku-*destabilise* hali halisi ya utulivu wa nchi yetu kwa ajili ya kuchukua rasilimali zetu kuzipeleka katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wazi hata walioingia Iraq, lakini mwisho wa siku kwamba, mafuta ya Iraq yanaondoka katika nchi zao, kuna jambo la kujifunza, leo hii gesi tuliyokuwa nayo kuna watu wanaweza wakaleta chokocho aina yoyote na wakasema kwamba kuna vikundi vya kigaidi vya nyuklia hapa. Wakaja kuhodhi nchi yetu na kuchukua uchumi wetu wote kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tutathmini kwa kina sana na tunaona wazi hata sehemu nyingine nchi zinavamiwa. Tuliona hili hata Libya watu wamekaa katika vikao huku wakaja kuivamia Libya, leo hii uchumi wote wa Libya unakwenda katika nchi zao tu. Tusiongopeane hili jambo liko wazi. Kwa hiyo, kama viongozi tumepewa majukumu ya nchi, kama Wabunge humu tunatakiwa kweli

turidhie kwa kujiridhisha tusiwe *rubber stamp* ya kupitisha vitu ambavyo vitaleta madhara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujitafakari kwa kina kwa nini tumechelewa kuridhia, kwa nini hata kuweka *signature* tulisita kwa muda muafaka. Maana yake ndani hapa kuna mashaka, naomba niwaambiwe ndugu zangu, Tanzania yetu kuna rasilimali nyingi sana na rasilimali hizi tutaweza kuzilinda sisi Watanzania wenyewe. Inaweza ikapitishwa kupitia katika Mkataba wa Kimataifa miaka kumi na tano ijayo Tanzania hii rasilimali zote zitakwenda kwa wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wazi kwamba kuna wababe, mnamuona hata Rais wa nchi fulani hapa alisimama katika vyombo vya habari akasema kesho naenda kuipiga Mali hata kuweka muafaka hakuna. Tunaona ilikuwa kwa Libya, haiwezekani kushindikana kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chokocho zozote zinaweza zikafanya hapa Tanzania ikaonekana ni nchi mbaya, inahifadhi magaidi, ikaja kuvamiwa na rasilimali zake zote zikaondoka. Mwisho wa siku tunajikuta tumeingia katika kitanzi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo, ni kama maangalizo, kwangu mimi au ndani ya nafsi yangu naona kwenye Mkataba huu kuna mashaka makubwa sana. Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kazi iliyopo mbele yetu

inahitaji karibu nusu saa nyingine tumalize, naomba kwa kutumia Kanuni ya 28, kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ili Bunge liendeleo hadi saa saba na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kutengua Kanuni ili Bunge liendeleo hadi saa 7.30 ilipitishwa na Bunge)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza Mikataba kama hii kuipitisha pitisha kwa nusu saa bila watu kupewa muda wa kutosha kuchangia ni kuwaumiza Watanzania, na naanza kwa kusema ningekuwa mimi ndiye naongoza nchi hii kama Rais, hii mikataba tusingeipitisha, hii mikataba bado. Kwanza Wabunge tulipaswa tupewe semina ya kutosha kwenye Mikataba hii, tuichunguze kwa undani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo taarifa ya Kamati yenyewe ina *doubts*, inapendekeza baadhi ya *provisions* ziende kurekebishwa, halafu tunajadiliana kitu nusu saa kinapita, kitu ambacho kinaweza kuathiri vizazi na vizazi, *what does it mean?* Tuwe *serious* na nchi hii na hiki kitu nadhani mmeona akileta Waziri wa Nishati na Madini tutahoji sana, mkaona alete Waziri wa Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kuchangia, cha kwanza, naomba kuchangia kuhusu huu Mkataba wa *Convention on Prevention and Punishment of*

Crimes Against Internationally Protected Persons including Diplomatic Agents.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Mwalimu Nyerere na Mwinyi na Mkapu ambao walichelewa sana kusaini Mkataba huu na sababu zao ni za msingi. *International Law* imekuwa inatuathiri sana nchi za Kiafrika, watu tumekuwa tunaingia kwenye vitu hovy hovy, wenzetu wanakuwa makini. Leo tunapitisha huu Mkataba unaotoa *immunity* kwa hawa *Diplomatic People*, ni kitu ambacho si cha kawaida kawaida, ni kitu ambacho kinatengeneza *doubts* nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa wafanyakazi wa Kibalozi na watu ambao watakuwa na kinga za kidiplomasia tutakuwa hatuwezi kuwakamata, tutakuwa hatuwezi kuwaingilia ingilia tu kuwa-*prosecute* kirahisi ndiyo kitu ambacho tunapitisha. Wale watu wanafanya usalama wa Taifa wa Kimataifa, wanakuja huku kuchunguza namna gani ya kutuibia mali zetu, leo tunawapa kinga wasikamatwe wawe huru, tunapunguza *state sovereignty* kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiki kitu binafsi sijakubali na naamini kama Wabunge tungepewa semina ya kutosha kwenye mikataba yote hii miwili wa kwanza huu wa *Diplomatic* na wa pili huu wa *Nuclear* tusingeweza kupitisha Mikataba hii kwa haraka. Sasa nataka kujua mtadhibiti vipi hawa watu ambao watakuja kwa kujifanya ni wana diplomasia halafu wanafanya vitendo ambavyo siyo sawa kwa nchi yetu.

Baada ya kuridhia Mkataba huu, mtakuwa na mbinu zipi za kuwakamata watu ambao watakuja kufanya uchakachuaaji kupitia Mkataba huu, ambao watatumia kinga hii kuja kutuathiri Taifa; mtawakamata namna gani kwa sababu mmejitoa? Binafsi kwa kweli sioni kama kulikuwa na haja ya kupitisha Mkataba huu kwa hivi sasa.

Ukiangalia wanaposema Wakuu wa Nchi na Taasisi, Balozi zetu sisi ndiyo wamezoea kutupokea pokea tu pale tukienda kutembea na nini hata kutangaza Utalii hawawezi. Hawa Balozi zao *they are doing business*, hawako pale kupokea pokea tu Marais wao wakija huku kama sisi. Hawa mnawawekea kinga, wala hii kinga sisi kule haitusaidii, huu Mkataba haupo kwa ajili eti ya Balozi wa Tanzania aliyeko Marekani. Huu Mkataba upo kwa ajili ya Mabalozi na *Diplomatic Agents* walioko huku Afrika, kwa ajili ya malengo yao mbalimbali siyo kwa ajili yetu. Mabalozi wetu kule wanafanya nini; vitu gani vipya ambavyo wanavifanya kule ambavyo sisi hatuvijui? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli jambo hili limenisikitisha sana. Nimesoma hii Taarifa ya Kamati kwenye Mkataba huu mwingine wa *Nuclear*, nimeona una *doubts* nyingi; na pia nilitaka kupata majibu ya Serikali, licha ya kutotupatia semina ya kutosha Wabunge ili tuweze kuridhia Mkataba huu tukiwa na amani baadhi yetu. Nilitaka kujua kwa nini huu Mkataba umeletwa sasa hivi kwa haraka haraka na kuna mijadala mingi ya *nuclear* hapa katikati na *uranium* na muda huo uliopita mlikuwa hamjauleta?

Pia kama nimesoma vizuri Taarifa ya Kamati, inaonekana Ibara ya 26 ya Mkataba inasema, *State Party*, inaweza ika-*propose amendment* na zikawa *circulated*.

Sasa nilikuwa nataka na mimi nipate ufafanuzi kuhusu hizi *additional* ambazo Nchi Wanachama wa Mkataba huu wanaweza kuzi-*circulate* kwenye *State* na sisi zitakuwa zinatu-*affect* namna gani? Napenda kupata ufafanuzi.

La mwisho, nilitaka kujua kwa sababu Serikali imekwisha kusaini na Kamati ya Bunge imeonesha kuwa na wasiwasi na Mkataba huu na mimi nakiri kabisa kwamba, ningekuwa nimejiandaa vizuri sana kuuchangia huu Mkataba, ningechangia mambo mengi sana, lakini nimeupata kwa haraka sikuweza kuupitia lakini nimeuelewa. Nataka kupata majibu; Kamati imeleta *doubt* na imejaribu kutoa wazo la baadhi ya vipengele kwenye Mkataba, kitu ambacho hakiwezekani. Sasa nini nafasi ya Bunge, kwa sababu Bunge linaridhia, lakini Kamati iliyokuwa inafanya kazi ya Bunge imeonesha kuwa na shaka na vifungu vya Mkataba huu; sasa tunaaridhia Mkataba huu kwa vigezo vipi wakati Bunge lina-*doubt*? Kamati ambayo tumeituma kufanya kazi ina mashaka na vifungu vya Mkataba huu; tunaupitisha kwa vigezo vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini binafsi nina mashaka makubwa na Mikataba hii yote miwili na hata kama itapitishwa ipitishwe lakini ninashauri kwamba, tusiiridhie kwa muda huu kwa sababu ya hizi *pressure* za watu wa nje. Nakushukuru sana. (Makofi)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia Mkataba kwa ajili ya kinga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyerere, hebu hamia kwenye *microphone* nyingine.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze na huu Mkataba wa Kinga kwa Watu wanaofanya kazi nje ya nchi zao. Jambo la kushangaza, tuko hapa tunazungumzia Azimio kwa Ajili ya Kinga ya Watu hao wakati sisi wenyewe kama Taifa, tumeshindwa kuonesha mfano wa kuwapa kinga Wananchi wetu wenyewe hususan wale wanaofanya kazi nchi za nje. Kwa mfano, kuna watu wako kwenye Balozi zetu nje hawapelekewi pesa kwa wakati mwafaka, matokeo yake wanakuwa ombaomba na wanashindwa ku-*focus* na kazi ambayo imewapeleka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kawaida kabisa kama ukitaka kuwa muungwana kufanya mambo yaliyo mema hata kama hakuna mtu yeyote ambaye anakuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Azimio la *Nuclear Terrorism*. Jambo la kushangaza, tunazungumzia Azimio hili ndani ya Bunge wakati *the majority Tanzanians* hawajui hata maana ya *Nuclear Terrorism*. Napendekeza kama tunataka kufanya kazi zetu kwa ufanisi kama Taifa ni lazima tujiandae kutoa elimu kwa Watanzania. Mtanzania gani anayejua madhara ya *nuclear* ukiacha sisi Wabunge ambao mmetupa haya Maazimio tena dakika ya mwisho; hakuna! Inataka uelewa wa ziada hata kuweza kuyachambua haya Maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua madhara yasababishwayo na *nuclear* pamoja na kwamba wenzetu wanatumia *nuclear* kutengeneza mafuta, wenzetu wametumia *nuclear* kutengeneza silaha, wenzetu

wametumia *nuclear* kutengeneza *radioactive material* ambazo zinaweza zikatumika kumuua binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutambua madhara makubwa haya, tunakuja hapa Bungeni kama Taifa, tunakiri kwamba tumekuwa tukifanya mazungumzo na jirani zetu wakiwemo Wakenya, Waganda na Wananchi wa *DRC*. Sioni kama tuko *serious* katika tatizo la *nuclear terrorism*, ni tatizo la Kimataifa, ni tishio la Kimataifa, huwezi ukasema kwamba utatatua tatizo hili kwa kuongea na jirani zako tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima sasa tuwe na utayari wa kuzungumzia tatizo hili kubwa na la hatari zaidi Kimataifa pamoja na Wananchi wengine wote Duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupate tahadhari ya kutosha ni lazima pia tujiandae kuwa na Wataalam wetu. Ninasema hivyo kwa sababu ni lazima tuwe na Wataalam ambao wanajua masuala ya *nuclear*, wanaweza waka-*detect threat* ya *nuclear* hata kutokea hapa Tanzania na waka-*detect* hiyo *threat* hata kama inatoka nchi nyingine yoyote ile Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jambo jema ambalo linaweza likafanyika bila ku-*invest* pesa. Sisi Watanzania tumekuwa waoga sana wa ku-*invest* ili upate unachokitaka, tumekuwa wepesi sana wa kutamani vitu bila ku-*invest* pesa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *nuclear terrorism* ni kubwa kuliko tunavyofikiria hapa. *Nuclear power* ina *threat*

Dunia nzima, inamaliza viumbe vingi tu kwa nukta chache na hamuwezi kusubiria eti ku-*prosecute* waharifu ambao watakuwa *involved* kwenye hii *Nuclear Terrorism*, kwa sababu *by the time* ana-*commit* hiyo *crime*, wewe utakuwa umemalizika, kwa hiyo, hutakuwa na nafasi ya ku-*prosecute*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tunatakiwa tuzungumzie *prevention; how do we protect, how do we prevent ourselves* kutokana na hii hatari ya *nuclear terrorism*. Ninaomba Serikali yetu iachane na wazo la kufikiria kwamba, eti tuta-*prosecute* wale wote ambao watahusika na uharifu huu. Tukifikiri hivyo tunajidanganya na tunafikiri hivyo kwa sababu hatujui maana ya *Nuclear Terrorism*, tunafikiri hivyo kwa sababu hatujui hata maana ya *nuclear power*. Tungetambua maana yake, tungejikita sasa kwenye mazungumzo na nchi ambazo zimeendelea. Tungejikita kwenye mazungumzo kuwabana wale walioendelea ambao wanadhani *nuclear power* ni *solution* wakati ni hatarishi kwa kiumbe chochote kile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuiuliza Serikali katika bajeti zenu kwa miaka yote ya fedha mmewahi kutenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya ku-*prevent nuclear power* au *nuclear threat*? Nataka nipate hayo maelezo, kwa sababu hatuwezi kuendelea na *lip service*, ni lazima sasa tuanze kufanya kwa vitendo na kuonesha kwa vitendo. Suala hili la *Nuclear Terrorism* ni hatarishi na ndiyo maana sisi kama Wabunge, hatuwezi tena kuendelea kufanya mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii adimu na mimi naomba niweke mchango wangu mezani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kupongeza Azimio hili na kusema kwamba, Nchi yetu ya Tanzania siyo kisiwa kwamba tunakaa pembeni peke yetu, lazima tuingie katika mashirikiano ya Umoja wa Kimataifa. Sisi ni sehemu ya nchi ambazo ni miongoni mwa Umoja wa Kimataifa na mimi nitajikita katika Azimio moja tu linalohusu *Prevention and Punishment of Crimes Against Internationally Protected Persons*. Kwa hiyo, namna ya kuwa-protect hawa *diplomats* na kadhalika.

Moja kwa moja niende kwenye jambo la msingi sana kwamba, nchi yetu imeshasaini na sasa imeleta hapa kuridhia, baada ya kuridhia Mikataba hii hauwezi ukaitumia moja kwa moja hadi pale ambapo Sheria zetu za Ndani (*Domestic Laws*), tutakapokuwa tumezirekebisha ili ziendane na Mikataba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, isije ikawa tumeridhia halafu tunasahau kurekebisha Sheria za Ndani. Kurekebisha Sheria ya Ndani ndiyo inaitwa *domestication*, baada ya *ratification* unaenda kwenye *domestication*, otherwise, any International Convention can not become part of the law of the United Republic of Tanzania. Hivyo ndivyo Sheria yetu inavyosema. Kwa hiyo, suala la ku-domesticate tusikawie kama tulivyokawia huko nyuma.

Sasa nina ushauri kwa baadhi ya Taasisi au Vitengo; ushauri wangu wa kwanza unaenda kwa Bunge na mimi ndiyo Mwenyekiti ninayesimamia *Vote 42* ya Bunge. Kamati

yetu sisi ya Katiba na Sheria, Mikataba mingi tumesaini na wakati mwingine tunapitisha, lakini tuna tatizo, haya Maazimio tunayo-*ratify*, hatuna *documentation* kuona mpaka mwaka huu wa 2013 nchi yetu ime-*ratify* Mikataba mingapi na ime-*domesticate* mingapi. Hatuna *matrix*, kwa hiyo, tunahitaji *a proper filing system* ambayo *any Professor or Academician can come in our library* na kusema ni Maazimio mangapi tumeridhia.

Otherwise, leo hii lazima tuingie kwenye *Hansard*, lazima tutafute, vitu haviko so *transparent* au vinginevyo uende kwenye Wizara husika kama ni Mkataba unahusiana na masuala ya mambo ya ndani au masuala ya Wizara fulani, lazima uende ukajiulize hivi ule Mkataba tumesaini, tume-*ratify* na baada ya ku-*ratify* kuna *reservation!* So, *it takes a lot of time*. Kwa hiyo, huo ni ushauri moja kwa moja kwa Bunge tunahitaji utekelezaji haraka. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, niende kwenye masuala ya *reservation*, Ibara ya 13(1), ambayo Tanzania tumekubali kuuridhia Mkataba huu lakini kifungu cha 13(1) tumesema kwamba, hatukikubali na hicho kinahusiana na matatizo mbalimbali kuyapeleka kwenye Mahakama ya Kimataifa (*International Court of Justice*), maana kuna *International Court Of Justice* na *International Criminal Court* wanaita ICC.

Mimi naungana na mawazo haya ya Kamati pamoja na Wizara, kwa sababu zipo nchi ambazo ni miongoni mwa *United National Security Council* lakini hadi leo hazijakubali masuala yake yawe yanakwenda *International Court of Justice*. Kwa hiyo, tunahitaji kulinda mamlaka ya nchi, tuna *sovereignty of the country*. Kwa hiyo, masuala yetu yasiwe

yanakwenda huko kama ambavyo tumesema. Kwa hiyo, tunaridhia lakini tunaridhia kwa kuweka *reservation* katika kifungu hicho cha 13(1). Kwa hiyo, ni muhimu sana *otherwise*, Mikataba hii ni muhimu.

Ibara ya (2) inaelezea makosa fulani fulani yako pale. Ningeomba sana makosa yaliyoelezewa kwenye Ibara ya (2) ya Mkataba huu yaangaliwe na pale inapowezekana basi nchi yetu tuweze kuona namna gani tutashauri *the Secretariat* kama tulivyoambiwa kwamba, unaweza ukatoa *amendment in future*. Haya makosa nadhani kwa wakati wa sasa hayakidhi lazima tuyaangalie na ni namna gani tunaweza tukaongeza makosa ya muundo huo ambayo yako kwenye Ibara ya (2).

Nichukue nafasi hii kutoa ushauri kwa Waziri wa Mambo ya Nje, ambaye anaonana sana na hawa *diplomats* katika nchi yetu. Baadhi ya *diplomats* pamoja na kinga waliyokuwa nayo, hawatutendei haki katika nchi yetu. Tumeshuhudia kuna *diplomat* mmoja alikuwa amesimamishwa na *traffic*, lakini alimtemea *mate traffic*. Nadhani wote mnakumbuka suala hilo na tunashukuru Wizara husika ilimrudisha ndani ya saa 24. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wakati mwafaka sasa tunapopitisha kinga, isiwe sababu ya *diplomats* kuwa *rough* kwenye nchi yetu. Tunaelewa kwamba, hata *diplomats* wetu ambao wako kwenye nchi nyingine, lazima waendane na Sheria hizi, lakini kuheshimu Sheria za Nchi ni jambo la msingi siyo kwa kuwa wana kinga. (*Makofi*)

Jambo hili liende sambamba hata namna ya kuwa-*treat* Watanzania. Nimeshuhudia baadhi ya Ofisi za

Diplomats, unakuta walinzi pale wanawa-*treat* Watanzania kwa namna tofauti kabisa. Mtu anakwenda kwenye Ofisi ya Ubalozi, yule mlinzi anavyom-*treat* huyo Mtanzania, tena yamkini ni Mbunge, utadhani siyo Mwananchi. (Makofi)

Kwa hiyo na hili Azimio *we are giving a warning* kwamba, licha ya *immunity* ambayo ipo, sisi ni watu wa amani, ni watu wa utaratibu, tumewapa ardhi tunajua wakishaweka bendera maana yake lile eneo ni *jurisdiction* ya ile nchi lakini *so long as* wapo Tanzania, tunaomba *respects*. Wao *Diplomats* wanapokuja kwenye Ofisi zetu Bungeni na maeneo mengine, wanapokelewa vizuri na kadhalika. Kwa hiyo, na Watanzania wanapoenda kwenye ofisi zao kwa sababu moja ama nyingine, kwa ajili ya *International Relation* na vitu kama hivyo, wawapokee *with kindness and humbleness*. (Makofi)

Kwa hiyo, tunaomba sana, siyo kwamba wakiwa na *immunity* basi Watanzania wanakuwa *treated* tu tofauti. Hiyo kwa kweli tungeomba tuiangalie maana tumefanya *research* za kutosha, *the way* Watanzania wanavyokuwa *treated* katika maeneo haya ya ofisi, hayapendezi. Wakati mwingine *of course* yanafanywa na watu wa *security* wale wanaolinda pale, lakini wakati mwingine wanapewa *guidance*. Kwa hiyo, tunaomba *respect and humanity, must be observed*.

Kwa kweli nilikuwa nataka nichangie hapo, kwa asilimia mia moja ninaunga mkono kutoridhia kifungu hiki cha kutumia Mahakama hii ya Kimataifa, bado sisi tuna Mahakama za kutosha, lakini pia tunazo hata Mahakama za Afrika, kunapokuwa kuna jambo lolote tuna Mahakama inayohusu matatizo ya *East African Community*, tuna

Mahakama inayohusu masuala ya Afrika ya Rwanda iko pale Arusha na kadhalika.

Kwa hiyo, kama ambavyo nchi ambazo ni Wajumbe wa *Security Council* ya *United Nations* hawakuridhia hiki kifungu, kwa hiyo na sisi tusubiri baada ya wao kuridhia na sisi sasa tuseme tutakwenda kwenye *International Court of Justice*. (Makofi)

Tuna ushahidi mzuri kabisa, kuna nchi nyingi sana za *Security Council*, *they are not Members of the International Court of Justice* wala *International Criminal Court*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na nitaunga mkono hoja nitakapopata ufafanuzi wa baadhi ya maeneo ambayo nimeomba *clarification*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, dakika kumi zitakutosha?

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja zilizopo mbele yetu. Naungana na wasemaji waliotangulia kwamba, wasiwasi mkubwa unaoonekana juu ya matatizo ya Maazimio haya, ni kwamba, mara nyingi inaonekana Maazimio yanaletwa kutokana na shinikizo la Mataifa makubwa, ambayo yanataka kujenga maslahi yao ndani ya nchi yetu. Huo ndiyo wasiwasi wetu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati husika, lakini pamoja na hayo ambayo Mheshimiwa Felix Mkosamali ameyaeleza, ni kweli mambo haya makubwa

yatolewe semina kwa Wabunge wote ili kuweka upeo na uwazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri akiwasilisha Azimio la Diplomasia alieleza kwamba, kuna kuridhia kwa shaka kifungu namba 13(1). Mkataba wote, hauoneshi utaratibu wa kupendekeza mabadiliko ya nchi, kama kuna tatizo hapa kuna kipengele unasema unaridhia kwa shaka, lakini mapendekezo ya kufanyia mabadiliko huwezi. Hapa kuna matatizo kidogo ambayo naomba yawekwe sawa. Je, ni kwa kiasi gani sisi kama nchi, tunaweza kupeleka mapendekezo yakafanyiwa kazi au tunaridhia tu kwa shaka kama kuna tatizo fulani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo ni tatizo. Mtazamo huo katika hali ambayo inaonekana ya Mkataba huu wa Diplomasia kwenye Article (7) nanukuu: *“The State Party in whose Territory the alleged offender is present shall, if it does not extradite him, submit, without exception whatsoever and without undue delay, the case to its competent authorities for the purpose of prosecution, through proceedings in accordance with the laws of the State.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufahamu wangu ni kwamba, mtuhumiwa anachukuliwa hatua katika vyombo husika pamoja na kutoa nyaraka za ushahidi na nchi nyingine zimeazimia kutotoa nyaraka hizo. Sasa hili likitokea kwamba nchi husika haitaki kutoa nyaraka, katika maelezo ya Serikali, sikuona wakieleza jambo lolote kutokana na kipengele hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi mkubwa wa mambo haya ni uwazi na ukweli, lakini kilio kikubwa kinaonekana

kwenye hili la Nyuklia na *Uranium* zaidi. Kwa kuwa nchi yetu kama alivyosema Waziri, nanukuu maelezo yake anasema kwamba: “Kugundulika kwa *Uranium* Tanzania, nchi yetu inaweza kulengwa na magaidi.” Hii ni kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akiwasilisha hoja. Sisi kama nchi, tumejiandaa vipi kuwaelimisha watu wetu walio katika maeneo ambayo Taarifa ya Serikali inasema tayari *Uranium* imegundulika. Kwa mfano, kule Namtumbo, Mwananchi wa Namtumbo Kijijini ambaye haelewi jambo lolote juu ya sheria hii, ni kiasi gani tumetoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu hapa inawezekana akakutwa na kipande kidogo cha Madini ya *Uranium*, lakini kutokana na kutokuwa na elimu sahihi akaingia hatiani. Kwa kuwa jambo hili litafanyika huko Namtumbo na maeneo mengine hivi karibuni, Serikali mmejiandaa kiasi gani kutoa elimu au tunasubiri yale yale ya Mtwara baadaye mkitaka msemu kuna jambo hili na lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu pia kuna taarifa na kuna swali nakumbuka Naibu Waziri alijibu mara moja hapa Bungeni akasema ni kweli taarifa tunayo, Madini ya *Uranium* yamegundulika kule Bahi. Bahi ni eneo kubwa; je, mmeandaa mazingira gani ya kuwaelimisha Wananchi wa Bahi, Kigwe, Chanisanga, Chikola, Chimendeli, Chipanga na Nzasa? Ni maeneo yao, sasa unasema tu kwamba, keshokutwa tunataka kwenda kuchimba, yasije yakatokea kama yale ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje juu ya hili; Kigwe, Chanisanga, Chikola, Chimendeli, Chipanga na Nzasa huko Bahi wanataka kujua haki zao? Je, Serikali

mnasemaje juu ya hili? Katika hali isiyo ya kawaida, mara nyingi yanapotokea matatizo mbalimbali, tumekuwa tukipeana taarifa, lakini kitu cha kushangaza, bado huwa hakifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua tu, yale Mataifa makubwa, ikitokea Tanzania inaingia Mkataba na Nchi kama Irani katika uchimbaji wa madini, na kwa sababu Uranium ambayo tunayo sisi na Irani wanachimba na Irani siyo mwema kwa baadhi ya Mataifa hayo ya mabosi wakubwa; hatuoni katika utaratibu huo tunajiingiza katika matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kutafakari hili, kwa sababu Mataifa makubwa na baadhi ya Mataifa mengine ambayo yote yanaonekana hayaendi vizuri, lakini Nchi kama Tanzania ikiingia Mkataba na nchi ambayo haipendezewi na nchi kubwa; je, hili tunaliona vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukae makini, tutafakali kwa upeo, isionekane tunakwenda tu. Mimi nakubali kabisa, sisi kama Wajumbe wa Kamati ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Felix Mkosamali pale, nakubaliana naye kabisa kwamba, elimu zaidi inahitajika katika maeneo ambayo utaratibu huu utaweza kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, nakushukuru sana, nilikupa dakika kumi tu na ulizikubali.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, nashukuru kwa michango yote. Nilitaka kuzungumzia hoja hii ya mashaka ya Mheshimiwa Felix Mkosamali, Kamati zote pamoja na

Kambi ya Upinzani. Kambi ya Upinzani inalishawishi Bunge hili liazimie kuwa tuingie kwenye Mkataba huu, kwa kujiunga kwa mashaka. Sasa mashaka haya, si mashaka kutoka nje, kukumbana na mafuriko au mamba au mashaka ya ajali. Kwenye Lugha ya Kidiplomasia, hii ni *reservation* na huwezi ukapeleka *reservation* zako bila kuwa Mwanachama. Kwa hiyo, siku unapokwenda kuingia kwenye uanachama, kwa kuridhia hii, una-*register* mashaka yako, kama hapa Kambi ya Upinzani imesema vizuri namba 13(1), ambayo Serikali yetu, itakapokwenda ku-*register*, inakwenda ku-*register* na *reservation* zetu ni hizi.

Baadaye tutakusaidia kitabu cha nchi ambazo zimeingia kwenye Mikataba hii miwili na *reservations*. Maeneo ambayo Mahakama kama nchi. Pili, suala la hawa watu wa diplomasia, Mkataba huu hauwapi fursa ya kufanya makosa na kutoa *passport* ya kidiplomasia aka-*go away with it, no*, sheria za nchi zita-*apply* pale anapofanya jinai ndani ya nchi. Nilitaka kulisema hilo tu, kwa sababu mimi ndiyo nilihusika kwenye suala hili na ndiyo fani yangu kubwa sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Moses Machali.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja dogo tu; mmepewa *Schedule of Amendment* za *Miscellaneous*, nafikiri mnazo, Serikali imetangaza kuzi-*withdraw*. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa kwenu. Wachangiaji walikuwa tisa, wamechangia sita, jioni tutamruhusu Mheshimiwa Waziri ahitimishe hoja yake.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni. Nawashukuru sana.

*(Saa 7.30 mchana Bunge lilisitishwa
Mpaka saa 11.00 jioni)*

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mchana tuliongezea muda kwa kutegemea tupate Wajumbe wa kutosha kuchangia na Serikali ipate kutoa majibu jioni hii ili tuingie kwenye Mswada wa *Miscellaneous*. Mswada huu hauingii tena jioni hii, kwa maana hiyo sasa natoa nafasi kwa mchangiaji aliyebakia, Mheshimiwa John Mnyika, aweze kuchangia ili baadaye Serikali ihitimishe.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mikataba hii miwili.

Nianze na Mkataba kuhusu Uhalifu Dhidi ya Watu Wenye Kinga ya Kimataifa, pamoja na Wakala wa Kidiplomasia. Neno la msingi sana hapa ni uhalifu dhidi ya watu wenye kinga, kwa sababu tayari kwa mujibu wa Mikataba mingine ambayo nchi yetu ilikwisharidhia huko nyuma ikwemo Mkataba wa Viena, tayari tulikwishatoa kinga. Kama ilikuwa sahihi au laa, lakini kinga ilikwishatolewa, sasa tunakwenda kuongeza kinga dhidi ya uhalifu kwa watu ambao tayari walikwishapewa kinga, kwa maneno mengine wasifanyiwe uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata maelezo kwa kweli ya kina sana, huu Mkataba ulisainiwa kwa maana ya Kimataifa mwaka 1973, leo ni mwaka 2013, miaka 40 imepita toka Mkataba huu ulipotungwa, kwa mara ya kwanza ndiyo unaletwa kwenye Bunge hili, kwa kweli ni aibu ya Kimataifa kuwa na Mkataba huu wa miaka 40. Maelezo pekee ambayo yanaweza kutolewa yakaridhisha ni ama Serikali ieleze kwamba kulikuwa na vifungu kwenye Mkataba huu, ambavyo kwa kweli kwa miaka yote 40 kama Taifa tuliona hakuna sababu ya kuuridhia huu Mkataba. (*Makofi*)

Kinyume chake, basi Serikali ieleze kwamba kulikuwa na uzembe mkubwa sana, toka mwaka 1973 Mkataba kutungwa lakini haujaletwa Bungeni mpaka hivi sasa, ni kati ya mambo mawili tu, lakini nasikitika, ukiangalia maelezo yaliyotolewa na Serikali ukurasa wa nne, Serikali imelizungumza jambo hili kama jambo jepesi tu, imelizungumza kwa mstari mmoja tu na ninaomba ninukuu, Serikali inasema: “Kama nilivyotangulia kueleza hapo awali, Mkataba huu uliundwa mwaka 1973, tangu muda huo Tanzania haikuwahi kutia saini au kujiunga. Kwa hiyo, Tanzania kwa miaka 40 haijawahi kutia saini wala kujiunga, lakini Serikali haielezi jambo hili ni kwa sababu gani; ni uzembe au ni tulikuwa hatuna sababu ya kuridhia huu Mkataba?

Kama hatuna sababu inashangaza ni kwa nini! Kifungu pekee ambacho tunakiridhia na angalizo ama tunakiridhia na katazo au tunakiridhia na ukomo kwa maana ya *reservation* ni kifungu cha 13(1) pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo linahitaji maelezo ya kina sana kutoka kwa Serikali. Tuliwahi kupendekeza huko nyuma, turekebishe utaratibu wetu wa uletaji wa hii Mikataba, hii Mikataba pamoja na kuwa ni *Convention*, Mkataba, siyo Itifaki kwa maana ya *Protocol*, pamoja na kwamba tutahitaji kuingiza kwenye Sheria zetu kwa maana ya *domestication*, lakini hii Mikataba ina mwelekeo wa kisheria. Kwa mujibu wa taratibu zetu za utungaji wa sheria kama nchi, tukiletewa Miswada ya ndani ya Sheria, kwanza, Wabunge tunapewa siku 21 kabla, tunapewa Muswada kama ulivyochapwa kwenye Gazeti la Serikali, tunakuwa na fursa ya kuupitia.

Pili, kunakuwa na mchakato wa hatua mbalimbali, lakini inapokuja masuala ya Mikataba, tunaletewa harakaharaka ndani ya Ukumbi, huku tunatakiwa tujadili na tunatakiwa turidhie. Jambo hili linahitaji kubadilishwa kwa sababu litakuwa na athari sana siku zijazo.

Tulipendekeza na ni vizuri Serikali ikatolea kauli jambo hili, Viongozi wetu wanapokwenda nchi za nje, iwe wamesaini Mikataba au wamekataa kusaini, lakini wameshiriki kwenye Mikutano ambayo kuna Mikataba yenye tija au yenye athari, ambayo imepitishwa. Kuwepo utaratibu, kama tunavyoanza Mikutano ya Bunge, tunaambiwa kwamba katika kipindi hiki kuna nyaraka hii na hii, iwe ni magazeti ya Serikali, tunawekewa hapo kwamba kuna hati za kuwasilishwa Mezani, kuna jambo hili na hili. Ili Wabunge tuweze kuifuatilia na kuisimamia Serikali kuhusu Mikataba hii ya Kimataifa, kabla hata hatua ya kuletewa kuridhiwa, tuletewe taarifa mapema tuweze kufuatilia.

Nalisema hili kwa sababu Serikali hii imekuwa na kawaida ya kuchagua Mikataba ambayo ama kuna shinikizo la Kimataifa inaletwa harakaharaka au ina maslahi kwa Serikali inaletwa harakaharaka. Mikataba yenye maslahi kwa Umma, ambayo pengine inaweza ikawa na athari kwa Serikali au kwa Chama kinachotawala, huwa inawekwa kabatini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano tu, huu ni Mkataba wa *African Charter on Democracy Election and Governance*. Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala, nchi yetu ilishiriki kwenye Mkutano mwaka 2007, Mkataba ukapitishwa, lakini toka 2007 Mkataba huu haujawahi kuletwa kwenye Bunge letu Tukufu kwa ajili ya kuridhiwa. Mkataba huu peke yake, kama ungeletwa na kuridhiwa maana yake ni kwamba, Tanzania ingelazimika kubadili mifumo yake ya uchaguzi, kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki, lakini kwa sababu masuala kama haya, hayana maslahi ya moja kwa moja kwa Serikali, hayana maslahi ya moja kwa moja kwa Chama kinachotawala, inabaki kuwa siri hailetwi huku Bungeni.

Kwa hiyo, ni vizuri Mkataba huu nao, Serikali itoe kauli ni lini Mkataba huu utaletwa. Nilikuwa nafuatilia mkutano uliopita wa *APRM* ambapo nchi yetu ilikwenda kuwasilisha Ripoti yake. Mkataba huu, una kifungu ambacho kinatoa masharti kwa nchi yetu kuhusiana na masuala ya Utawala Bora na kuhusu masuala ya *APRM*, kwa sababu hatujaridhia Mikataba kama hii. Ni rahisi kwa Serikali kwenda kwa jamii ya Kimataifa na kutoa maelezo potofu kama ilivyotokea kwenye Mkutano wa *APRM*, Serikali inaeleza wenzetu kwamba, kwa mfano, Gazeti la Mwanahalisi limefungiwa eti kwa sababu linachochea uasi wa Wanajeshi. Taarifa

ambazo hazikuwa za kweli, lakini kwa sababu hatujaridhia Mikataba, hatuna namna ya kufuatiliwa, hatuna namna ya kusimamiwa, rai yangu ni kwamba, Mkataba huu nao uletwe uweze kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kwenye Mkataba ambao unajadiliwa hapa unaohusu masuala ya ugaidi wa kutumia *nuclear*. Nchi yetu inapita katika wakati ambao ni tete kidogo, kuna msukosuko wa Kikoloni Mamboleo, kuna msukosuko wa Ubeberu na msukosuko huu unaongezeka zaidi nchi yetu inapokuwa katika hatua za utafutaji wa Madini nyeti kama ya Urani, ambayo yamegombanisha Mataifa mengine. Kitendo cha Mkataba huu kuletwa harakaharaka, wakati nchi ikiwa katika mivutano ya ushindani wa Kimataifa, upande mmoja Nchi za Australia, Nchi za Marekani, Nchi za China, wote wanajipenyeza kwa namna moja au nyingine kwenye nchi yetu kwenye masuala ya Urani; ni vizuri Serikali ikaeleza kwa uwazi sababu za kuleta Mkataba huu kwa harakaharaka ni nini katika mazingira kama haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha Ugaidi wa *Nuclear*, pamoja na kuwa na Mikataba ni vizuri Serikali ikaonesha, kwa mfano, kusimamia Utawala wa Sheria, Waziri Kivuli wa Ardhi na Waziri Kivuli wa Nishati na Madini, tumekuwa tukiihoji Serikali kuhusu Kampuni ya *Game Frontiers*, ambayo ilipewa Leseni ya Uwindaji, badala yake ikachakachua ikaenda kutoa kwa Makampuni ya uchimbaji wa Urani katika mazingira ya ukiukwaji wa Sheria. Katika mazingira kama haya, ni wazi tumeachia mianya, ni rahisi sana kwa nchi yenye Urani katika mazingira ya utawala wa sheria kuwa legelege, katika mazingira ya

ufisadi, ni rahisi watu kujipenyeza na kuanza kufanya ugaidi uwe ni wa *Nuclear* au ugaidi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuridhiwa Mikataba kama hii, ni muhimu tuiridhie kwa maangalizo na huu Mkataba wa *Nuclear*. Sisi tunakwenda kuweka angalizo kwenye kifungu cha 23 peke yake kinachohusiana na mashtaka kupelekwa kwenye Mahakama za Kimataifa.

Nchi za wenzetu zenye kutaka kulinda nchi zao, zimekwenda mbali zaidi; Cuba, kwenye Mkataba huu wa ugaidi dhidi ya *Nuclear*, wameweka angalizo, wameweka masharti mpaka kwenye kifungu cha nne. Misiri, wameweka masharti kwenye kifungu cha nne na wameweka masharti kwa sababu kifungu kile kilivyo, kinaweza kutoa mwanya kwa ugaidi wa aina nyingine.

Ukiusoma huu Mkataba unazungumzia zaidi ugaidi wa Taasisi kwa Taasisi, ugaidi wa mtu kwa mtu, lakini kumeanza kujitokeza wimbi la ugaidi wa Dola Duniani, yaani *State Terrorism*, yaani Dola ya nchi moja, inakwenda kufanya ugaidi kwenye nchi nyingine. Sasa kifungu cha nne kwa namna kilivyo hivi sasa, kama nchi yetu itaridhia Mkataba huu bila angalizo, tunafungua mianya ya ugaidi wa Dola kutokea katika nchi yetu. Kwa kuwa sasa tumeanza Namtumbo na maeneo mengine kushughulika na masuala ya Urani, patakapojitokeza migogoro kati ya nchi kubwa na Makampuni makubwa kwenye Sekta nyeti kama ya Urani, ni rahisi mianya kama hii ikatumika kufanya Ugaidi wa Dola, kwa maana *State Terrorism* dhidi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali itoe maelezo ya kina sana kwa sababu mimi nikiitazama

Mikataba yote miwili ina mwelekeo zaidi wa shinikizo la kuileta kutoka nje kuliko shinikizo la ndani. (*Makofi*)

Serikali haijaweza kutoa maelezo ya kina hapa Bungeni, manufaa ya ndani ya sisi kama Taifa kukimbilia kuridhia Mikataba hii, Serikali haijatoa hayo maelezo. Kwa hiyo, kama kuna sababu nyingine za ziada za sisi kukimbilia kusaini Mikataba hii, iwe ni sababu za nje au za ndani, ni vizuri Serikali ikalieleza Bunge lako Tukufu ili tunapokwenda kufanya uamuzi, tufanye uamuzi tukiwa na taarifa sahihi.

Tulisema huko nyuma kwamba, tunapoletewa Mikataba hii, kama imesainiwa isije bila kutokuwa na saini. Mikataba iliyoletwa sasa hivi yote haina saini, mmoja tumeelezwa wazi kwamba Nchi yetu ilikuwa haijausaini na mwingine maelezo bayana hayajatolewa. Nasema hivyo kwa sababu katika hatua ya kusaini, kama tulikuwa na maaangalizo tuliyaweka katika hatua ya kusaini ni vizuri maangalizo hayo yakajitokeza hapa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na namna Maazimio yalivyoandikwa, kwa sababu mazingatio au makatazo ama *reservations*, zimewekwa kwenye sehemu ya kwa kuwa, yaani kwenye sehemu ya maelezo, lakini kwenye sehemu ya kuridhia sasa Azimio lenyewe, kwa pendekezo lililoletwa hapa Bungeni kwa Maazimio yote mawili ni kwamba, kama mtu anachukua Azimio peke yake la kuridhia, Bunge linakuwa limelipitisha hili Azimio kama *blank cheque* bila *reservation*.

Kwa hiyo, ni vizuri sana maelezo ya maangalizo, maelezo ya makatazo, maelezo ya ukomo, ya *reservation* kwenye Mikataba yote miwili, yakaingizwa moja kwa moja

kwenye Azimio la Bunge ili hata Serikali itakapokwenda kusaini hiyo Mikataba ambayo haijaisaini bado, kwa sababu inakwenda kusaini na kwenda kuridhia moja kwa moja, isije ikaenda tofauti na ambavyo Bunge limeazimia, hili jambo ni muhimu sana kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusainiwa na kuridhiwa kwa Mkataba ni jambo moja, kutekelezwa kwa Mkataba ni jambo lingine tofauti sana. Tumekuwa na kawaida ya kuridhia Mikataba bila ya ukomo wa muda kwa upande wa Serikali wa kufanya marekebisho ya msingi katika kuwezesha utekelezaji wa Mikataba. Tukitumia mfano wa mchakato unaoendelea Kenya hivi sasa baada ya Katiba mpya ya Kenya, wanaridhia wanapitisha sheria na hata katika Katiba yenyewe kuna sheria ambazo zimetaja na muda wake wa ukomo wa marekebisho ili kweli Serikali ilazimishwe kutekeleza kwa wakati.

Sasa wakati umefika kwa Tanzania katika wakati huu ambao tunaletewa Mikataba mingi, tunaletewa Itifaki nyingi, lakini mwisho wa siku zinakwenda kuishia makabatini. Mimi nasema haya kwa sababu Bunge hili lilipitisha Mkataba wa Vijana Afrika, tukapeana matumaini sana kuhusiana na ule Mkataba kwamba, Mkataba utatekelezwa, kutaundwa Baraza la Taifa la Vijana, halijaundwa mpaka leo, Mkataba ule haujatekelezwa. Kwa hiyo, tunaweza tukawa tunasaini Mikataba inaishia makabatini, ni muhimu sana tunaposaini Mikataba tuweke na ukomo vilevile wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa John Mnyika.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na wachangiaji tisa, mchangiaji mmoja ambaye ni Mheshimiwa David Silinde, alijitoa, wengine wote wamepata nafasi ya kuchangia. Sasa namwita mjibu hoja. Una dakika 60, una mengi ya kuelimisha, Wabunge waelewe, ili waridhie na wajue nini umekileta Mezani. Karibu Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kujibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza katika mjadala huu wa Maazimio haya mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii, kukushukuru wewe na Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kambi ya Upinzani na Wabunge wote kwa ujumla, waliochangia kwa mdomo na kwa njia ya maandishi.

Naomba kuwatambua Wabunge waliochangia hoja kwa njia ya mazungumzo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mbunge wa Mhambwe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile na Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo.

Pia naomba kuwatambua na kuwataja Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mbunge wa Mfindi Kusini, Mheshimiwa Athumani R. Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hamadi Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa David E. Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe waliochangia kwa maandishi na baadhi waliochangia kwa kuongea, pamoja na mambo mengine, wametoa ushauri ambao kwanza, naomba nikiri kwamba, tumeupokea na jitihada zitafanywa kuhakikisha kwamba, ushauri wao tunaufanyia kazi kwa kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa tunayalinda na hatuwezi tukayatelekeza. Nawashukuru sana kwa ushauri na kwa ahadi hii, nafikiri tunaweza kuendelea kuangalia namna gani tutatekeleza hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja zilizotolewa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwanza, walipenda tuzingatia Ibara ya (3) ya Mkataba ili kuzipa uwezo Mahakama kushughulikia makosa katika Mkataba, kufanyia kazi sheria za kubadilishana wakosaji na nyinginezo kabla ya kuiingiza nchi kwenye wajibu ambao umeelezwa kwenye Ibara ya (8) ya Mikataba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii pia ilishauri kwamba, kwenye Mkataba wa ugaidi tuufanyie kazi utata

ulioonekana kwenye matumizi ya neno *Lawful* katika Ibara ya (1) na pia kurekebisha Sheria ya Ugaidi ili kuingiza makosa yanayoundwa na Mkataba. Pia, walitoa angalizo kuhusu hatari za kuweka hatiani watu ambao hawana makosa, utaratibu wa kubadilishana wakosaji pia tuuzingatie na kuepuka kusigana kwa utata wa Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niende kwenye hoja ya kwanza, ambayo imezungumzwa na watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba, Tanzania haijaridhia Mkataba huu au Mikataba hii kwa muda mrefu sana na sababu ambazo ni miongoni mwa hayo ni kwamba, dunia ilikuwa ni sehemu nzuri ya kuishi lakini usalama unamong'onyoka taratibu. Kwa hiyo, inawezekana ikawa wakati mwingi Serikali ilikuwa imeridhika na sheria ambazo tulikuwa nazo na pengine haikuona uharaka wa kuridhia Mikataba hii kama ilivyo sasa. Wakati wa katikati hapo nchi hii ilipitisha Sheria ya Ugaidi mwaka 2002, ambayo kwa wakati huo ilionekana inaweza ikakidhi haja.

Kuongezeka kwa *complexity* ya masuala ya ugaidi, lakini pia kuonekana kwa Urani Nchini Tanzania, kumetuweka kwenye ulazima wa kuona kwamba tunajiweka vizuri kuhakikisha kwamba, Tanzania haiwi Kondoo wa muhanga katika hili na wenyewe tunajidhibiti ipasavyo katika kuhakikisha kwamba, Tanzania tunailinda kupitia Mkataba huu. Mikataba hii yote miwili haitukoseshi kitu isipokuwa inatuongezea uimara wa ulinzi wa *security* yetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama tulikuwa hatujafanya na tumefanya leo, nafikiri *better late than never* na ni vyema tukakubaliana kwamba ni jambo ambalo sasa hivi tusilizungumze isipokuwa tuipitishe Mikataba haraka ili tuweze kujihifadhi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya vifungu hivi vya 13 (1) na 23 (1) kwa Mkataba wa Nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa ya kuweka *reservation* ni fursa ambazo kila nchi imepewa na kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), walihisi kwamba pengine isingekuwa lazima kuitumia, lakini nafikiri lazima niseme kwamba, kuiacha fursa hii tusiweke *reservation* ya hatari kwa sababu bado wenzetu ambao tunaweza kuingia nao kwenye mgogoro, watakuwa na fursa ya kutumia kama ilivyo kwenye Mkataba na wanaweza wakatupeleka *International Court of Justice* bila ya sisi wenyewe kujua. Kwa hiyo, *reservation* inatupa nafasi ya kuweza kuendelea na hatua za majadiliano kabla hatujafanya uamuzi wa lazima wa kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kambi ya Upinzani, walikuwa wanazungumzia suala la kuangalia tafriji ya neno Dola na baada ya kuangalia inaonekana hakuna tofauti kati ya hii na ambayo ipo kwenye Katiba yetu. Uhusiano wa Mkataba huu na Sheria yetu Dhidi ya Ugaidi kama nilivyosema hapo mwanzo, *infact* Mkataba wa Ugaidi unachofanya ni kuimarisha *instruments* ambazo tayari tunazo na si vinginevyo. Kwa hiyo, kupitishwa kwa Azimio hili, inatupa fursa zaidi ya kujizatiti katika kuhakikisha kwamba, nchi yetu haiwi muhanga wa rahisi wa

mashambulio ya Nyuklia au rahisi kuhusika katika mambo hayo.

Pia, kulikuwa na hoja kwamba kuna haja ya kuhakikisha kwamba, vyombo vya ndani vinatumika kuliko kutegemea vyombo vya nje. Naomba kutoa taarifa kwamba, Mikataba hii ina sehemu ambayo vyombo vya nje vinaweza vikahusishwa lakini vitahusishwa na vyombo vya ndani. Kwa hiyo, utaratibu uliokuwepo ni zaidi kutumia vyombo vya ndani katika masuala mengi na ni sisi wenyewe ambao tutahusika kama ni taarifa au mambo mengine kutoa kwenye vyombo hivyo vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba, Mkataba huu unahusianaje na matumizi ya Urani. Mkataba huu unahusu utumiaji wa Urani ili isije ikaangukia kwenye mikono ya wahalifu, inaweza kutuletea maafa kwa kutumia Urani ambayo pengine ime-source au imeasili kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu athari za kujiunga na Mkataba huu ni zipi. Baada ya kuangalia Serikali haioni kwamba kuna athari za waziwazi na kama ilivyoshauriwa na baadhi ya watu, kwa sababu kwa upande wa ndani tutafanya *domestication* na kuweka sheria ambazo zitasaidia katika utekelezaji wa Sheria hii. Pia kwa upande wa nje tuna nafasi ya kupendekeza marekebisho pale ambapo tutahisi kuna *article* moja au mbili zinaweza zikaleta utata. Lazima niseme kwamba, hatuwezi kupeleka marekebisho kama bado hatujajiunga. Kwa hiyo, tujiunge na kutakuwa na hiyo fursa tunaweza tukatoa hayo marekebisho. (*Makofi*)

Hata hivyo, pamoja na *possibility* ya kutoa marekebisho hayo ni muhimu kuhakikisha kwamba, tunajiridhisha na nataka niwahakikishie kwamba, Serikali imejiridhisha kuhusu Mkataba wa Nyuklia kwamba, hauna mgogoro na Sheria zetu na kwa sababu zitabadilika basi lazima ziendane na zitufanye tuwe na ulinzi bora kuliko mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kusema kwamba, hawa ambao wanakusudia kulindwa kwenye Mkataba au Azimio la Diplomasia au Kinga za Diplomasia, kulikuwa na wasiwasi kwamba hawa wakifanya makosa ya jinai au ya madai tutawafanyaje. *In fact*, sheria zetu bado zitafanya kazi kikamilifu kuwashughulikia hawa lakini pia wigo utaongezeka kwa kujiunga na Mkataba huu, kwa sababu tutahakikisha pia Watanzania ambao wana sifa kama wao wanapata heshima huko ambako wanatumikia Taifa lao. Kwa hiyo, Mkataba huu utakuwa unatuongezea kwa vyovyote uwezo wa kuwalinda Watanzania, lakini pia kushiriki sisi wenyewe katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza wajibu wetu wa Kimataifa wa kuhakikisha kwamba na wale ambao wapo hapa wanalindwa ipasavyo na kwa upande wa makosa ambayo yatakuwa yanafanyika yatashughulikiwa kwa sheria tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, ambaye alitaka kujua kuhusu neno ugaidi. Sisi Tanzania tuna Sheria rasmi ya Ugaidi ambayo ilitungwa mwaka 2002 na kwenye Sheria hiyo ugaidi umetafsiriwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mnyaa, *ai-consult* hiyo Sheria na atajua kwamba hilo suala limekuwa *covered* vizuri na *discussion* kuhusu hilo imekaa sawa. Kama kutakuwa na hoja ya kuwa

pengine tuna marekebisho basi yanaweza yakauangana na marekebisho ya Sheria hiyo na tukayapitisha kama Bunge kwa ajili ya kutumika Tanzania.

Kuna hoja kwamba kuna uwezekano wa kubanwa watu wa kawaida kwenye vifaa hivi vya matumizi ya vifaa vya Nyuklia. Kiasi cha uhalali wa kumiliki vitu katika ibara ya pili iliyoelezwa kama ilivyoeleza makosa chini ya Mikataba hii kipo wazi na wakati wa kupitisha Sheria yetu ya ndani tutahakikisha kwamba, tunaweka maelezo ambayo yataepusha Wananchi kuweza kukamatwa au kudhalilishwa hovy kwa kutumia mwanya wa Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo kwamba, pengine Mkataba huu utazi-expose resources zetu na alitaka tahadhali ichukuliwe ili kuhakikisha rasilimali za Watanzania zinalindwa pamoja na kupitisha Mkataba huu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Sheria hii haizi-expose resources zetu ambazo zinalindwa zaidi na Mkataba huu, lakini pia na sheria za ndani katika kulinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkosamali, alizungumzia kuhusu mbinu za kuwadhibiti Wanadiplomasia watakaotumia Kinga za Kimataifa ili kufanya makosa. Nilisema hapa mwanzoni kwamba, sheria zetu kama tuna wasiwasi nazo kwamba haziwezi kumdhibiti mtu yeyote basi tuzirekebishe, lakini hivi tulivyo sheria zetu zitachukua hatua katika kutuhakikishia kwamba hawa wahalifu wa Kimataifa wenye kinga wakifanya makosa ya jinai basi kuna taratibu za kuwashughulikia na gravity ya kosa pia linaweza likasababisha hata Mwanadiplomasia huyo kuondolewa

nchini kwa amri wala hakuna wasiwasi wa kuwa hiyo kinga isivuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na mapendekezo ya Mheshimiwa Mendrad Kigola, anashauri kwamba, tuhakikishe tunajiunga haraka. Nafikiri baada ya Bunge kupitisha Azimio hili la Diplomasia na pia *Nuclear Terrorism*, basi tutachukua hatua za haraka kuhakikisha tunapeleka *instruments* kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili tuweze kuhakikisha kwamba tunajiunga kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya Mheshimiwa Pindi Chana, ambaye alitaka tusichelewe baada ya kuridhia Mikataba hii. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, tunaridhia kujiunga na Mikataba hii na haitatusaidia sana kama hatukufanya *domestication* ya Sheria na tukaiwezesha kuweza kutumika katika nchi yetu. Hili tutalifanya na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa hili.

Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumzia suala la elimu na pengine wasiwasi hasa kwa upande wa Azimio la *Nuclear Terrorism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Wajumbe wako kwamba, katika utekelezaji wa Sheria na Mkataba huu, tutahakikisha kwamba elimu itatolewa ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa Wabunge kupitia kwenye semina hasa wakati wa kupitisha Sheria ya *Domestication*. Kabla ya wakati huo, kwa leo nawaomba Waheshimiwa Wabunge, waniamini na waiamini Serikali kwamba, Mikataba hii haina matatizo kwa Taifa na tuiridhie ili baadaye tupate elimu ya namna ya kuitekeleza.

Mheshimiwa Leticia Nyerere, naye alizungumzia kuhusu elimu na kutaka itolewe kwa Wananchi wa maeneo mbalimbali ambayo kuna Urani au wanahitaji kujua kuhusu Maazimio haya na utekelezaje wake ili nao waweze kuona kwamba, hiki kitu kinachofanywa na Serikali ni kitu ambacho kina manufaa kwao na si vinginevyo.

Kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Silinde, naye alikuwa na wasiwasi kwamba kunaweza kukafanywa makosa na Wanadiplomasia ambao tunaongeza wigo wa kuwalinda. Kama nilivyosema, ni kwamba, Sheria tunazo za kutosha za kuhakikisha kwamba, makosa yote ya jinai na mengine ya jinai hapa nchini tunaweza tukayashughulikia na kama itatokea Mwanadiplomasia ambaye tunampa kinga ndiye atakayevunja, basi kuna taratibu ambazo tunaweza tukazishughulikia na tukamuweka katika sheria ambazo tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja na hasa hii ya kuchelewa kuridhia. Maelezo nimeyatoa na nataka niwahakikishie Watanzania kwamba, Tanzania kama nchi au kama Taifa, linahakikisha kwamba hili suala halichelewi tena na ndiyo maana ikaleta hii ili kuhakikisha kwamba tunapata ridhaa ya Bunge na tuweze kutumia *opportunities* hizi ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la kuwa hatujasaini na kwa nini tunataka turidhie; naomba nitoe taarifa kwamba, katika Mikataba hii ya Kimataifa kuna njia tofauti za kutaka kuwa mdau au kuwa *part to*, ni aidha unasaini halafu unaweza uka-*ratify* au ukaridhia, lakini pia unaweza ukaamua ku-*approve* au baadaye uka-*accede*

kama tunavyofanya sisi. Ni kwamba, katika Sheria ya Viena ya *Laws of Treaties, Article 11* na *15, Article 11* inatupa nafasi hizo za kuweza kujiunga bila ya kuweka saini ya awali, lakini pia *Article 15* inatuonesha vipi tunaweza kufanya *accession* kama tunavyoweza kufanya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa hatukusaini isiwe tatizo, nafikiri pia ni njia ambayo tumechagua pengine au tumelazimika tuitumie katika kujiunga na Jumuiya ya Kimataifa katika masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimtaje Mheshimiwa John John Mnyika katika orodha ya waliochangia kwa maandishi na baada ya hayo naomba nitoe hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri mtoa hoja na sasa nakuomba uhitimishe kwa kutoa hoja moja moja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji ...

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *quorum!*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, nakuomba ukae na ufuate taratibu za Kiti na Bunge.

Katibu naomba unipe akidi!

(Hapa kengele ililia)

MWENYEKITI: Hiyo ni kengele ya kuwarudisha Wabunge ndani.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Tunahesabu watu kwanza.
Waheshimiwa Wabunge, tunaomba mtulie kwenye viti vyenu, sasa mkihama hama tutawahesabu mara mbili mbili.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nilitaka niwathibitishie Bunge hili linaendeshwa kwa Kanuni kama ilivyoainishwa na kama tulivyokubaliana, hakuna mjadala kwenye Kanuni ya Bunge hili. Bado ninazo dakika tano za kufanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 77(5) inasema: “Endapo Spika ataridhika kwamba bado idadi ya Wabunge waliomo ndani ya Ukumbi wa Bunge haifikii akidi inayohitajika, basi ataahirisha Shughuli za Bunge hadi muda mwingine atakaoutaja.”

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi Mheshimiwa Salvatory Machemli, alipingana na kauli ya Waziri wa

Mambo ya Ndani ya Nchi, kutokana na yeye kuwa nao ushahidi wa kutosha kuwa maneno yaliyosemwa na Waziri hayakuwa sahihi. Mwongozo wangu ni kama ufuatao: Kwa vile Mheshimiwa Mbunge anao ushahidi, naomba achukue ushahidi huo aupeleke kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aifanyie kazi. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, atakuja kulitaarifu Bunge hili. Huo ndiyo Mwongozo wangu.

Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.55 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 7 Februari, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*